**16 FEBRUARI, 2024**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

**Kikao cha Kumi na Nne – Tarehe 16 Februari, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na: -

**MHE. BALOZI LIBERATA R. MULAMULA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2023.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge maswali, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 225

### Kuzuia maafa yatokanayo na mvua

**MHE. SYLVIA F. SIGULA** aliuliza: -

Je, Serikali imejipanga vipi kuzuia maafa zaidi katika kipindi hiki cha mvua nyingi zinazonyesha sehemu mbalimbali nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Ummy Nderiananga, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ili kuzuia maafa zaidi katika kipindi cha mvua nyingi zinazonyesha sehemu mbalimbali nchini Serikali imetekeleza shughuli zifuatazo: -

(i) Kutekeleza Mpango wa Taifa wa Dharura wa Kukabiliana na Madhara ya *El Nino* kwa kipindi cha Septemba, 2023 mpaka Juni, 2024;

(ii) Kuzijengea uwezo Kamati za Usimamizi wa Maafa kwenye mikoa 18 nchini;

(iii) Kutoa elimu kwa jamii kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kuhusu uelewa na uwezo wa

kuzuia, kujiandaa, kukabili na kupunguza madhara yanayotokana na maafa;

(iv) Kufuatilia mwenendo wa majanga, kutoa tahadhari kwa umma kupitia Kituo chetu cha Operesheni na Mawasiliano ya Dharura; na

(v) Kutekeleza mikakati na mikataba ya Kikanda na Kimataifa ikiwemo Mkakati wa Kimataifa wa Sendai wa Upunguzaji wa Athari za Maafa (2015-2030) na Mkataba wa Makubaliano wa Kuanzisha Kituo cha Huduma za Kibinadamu na Operesheni za Dharura cha Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu naomba kutoa rai kwa wananchi kuchukua tahadhari ikiwemo kuepuka kuishi katika maeneo hatarishi kama vile mabondeni, maeneo yanayopitiwa na maporomoko ya udongo, kuacha kukata miti hovyo, kuepuka kufanya shughuli za binadamu kandokando ya vyanzo vya maji, kutodharau nguvu ya maji na kufuatilia taarifa zinazotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini ili kuweza kujikinga na maafa, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Sylvia Sigula, swali la nyongeza.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninaipongeza Serikali kwa majibu yake mazuri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kufuatia upepo mkali uliovuma katika Bonde la Rukwa maeneo ya Ilemba, Sakalilo, Mtoisa na Isare umeleta athari kubwa kwa wananchi, mazao yameharibika na nyumba zimebomoka. Ilemba pale zimebomoka nyumba 16 na Sakalilo nyumba 44; je, nini kauli ya Serikali kwa wananchi hawa ambao hawajui wafanye nini, hawana chakula wala hawana sehemu ya kuishi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kutokana na hali inavyoendelea barabara huko vijijini hazipitiki, mawasiliano yamekatika, wanafunzi wanashindwa kwenda shule au

wanaenda kwa tabu; nini mpango wa Serikali wa dharura wa kuokoa tatizo hili? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Sylvia, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpe pole sana Mheshimiwa Mbunge kwa maafa hayo ambayo yamejitokeza katika eneo lake, lakini nimpongeze kwa ufuatiliaji wa karibu.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo aliyotoa na maafa ambayo yamewapata wananchi niendelee kuwapa pole wananchi wa Rukwa, lakini nitumie fursa hii kumuagiza Mkuu wa Mkoa wa Rukwa aandike taarifa hiyo ailete kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Waziri wa Nchi au vilevile anaweza kumtumia *RAS, RAS* akaandika kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu tutaipokea na tutaifanyia kazi kwa uharaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mpango wa dharura kwenye swali lake la pili naomba niendelee kuzielekeza Wizara zote na sekta zetu zote ndani ya Serikali ziendelee kuchukua hatua za haraka jinsi inavyowezekana kwa ajili ya kuendelea kuwasaidia wananchi kwenye maeneo mbalimbali nchini, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 226

**Ujenzi wa Kituo cha Afya Galapo – Babati**

**MHE. DANIEL B. SILLO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Galapo – Babati?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Jimbo la Babati Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya tathmini ya vituo vya afya vikongwe vinavyohitaji ukarabati. Hadi kufikia mwaka 2023 jumla ya vituo vya afya 202 chakavu vimeainishwa kote nchini kikiwemo Kituo cha Afya Galapo ambapo vitatengewa bajeti kwa awamu kwa ajili ya ukarabati.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuona uwezekano wa kutenga bajeti kupitia Programu ya Benki ya Dunia kwa ajili ya upanuzi wa Kituo cha Afya Galapo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, swali la nyongeza.

**MHE. DANIEL B. SILLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa kuwa ukarabati wa kituo hiki cha afya ni ahadi ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Mheshimiwa Naibu Waziri mwenyewe alikuja tukafanya mkutano wa hadhara na wananchi wanasubiri kwa hamu sana ujenzi huo uanze.

Je, nini *commitment* ya Serikali kuhakikisha kwamba ujenzi huu unaanza mara moja?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; wakati wa ziara ya Mheshimiwa Rais Mkoani Manyara mwaka 2022 Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI aliahidi shilingi milioni 100 kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa Kituo cha Afya cha Bashnet; ni lini ahadi hii itatimizwa ili kituo kile kiweze kutoa huduma kwa wananchi wetu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Mbunge ni kweli tulifanya ziara pamoja katika Kituo cha Afya cha Galapo na tuliahidi kupitia Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwamba tutapeleka fedha kwa ajili ya ukarabati wa kituo kile ambacho ni chakavu. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Wananchi wa Jimbo la Babati Vijijini kwamba Serikali iko katika hatua za mwisho za kutafuta fedha kupitia Mfuko wa Benki ya Dunia kwa ajili ya kwenda kukarabati Kituo cha Afya cha Galapo. Kwa hiyo, wakati wowote kuanzia sasa fedha hiyo ikishapatikana tutahakikisha tunapeleka pale kwa ajili ya ukarabati.

Mheshimiwa Spika, pili; kuhusu shilingi milioni 100 ambayo pia ni ahadi ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa ajili ya ukarabati wa Kituo cha Afya cha Bashnet, nikuhakikishie tayari tumeshakiweka kituo hiki kwenye mpango wa vituo vinavyotafutiwa fedha na ikipatikana mapema iwezekanavyo tutaileta kwa ajili ya ukarabati wa Kituo cha Afya cha Bashnet, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Zaytun Swai, swali la nyongeza.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kina mama wa Ngorongoro wana changamoto kubwa ya kutafuta huduma za afya; je, ni lini Serikali itajenga jengo la mama na mtoto katika Kituo cha Afya Loliondo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, tulishaweka utaratibu na mpango mkakati wa kuainisha vituo vya afya ambavyo vina upungufu wa majengo na Kituo cha Afya cha Loliondo katika Halmashauri hii ya Ngorongoro ni moja ya vituo ambavyo vimeainishwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nitumie fursa hii kwanza kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inalitambua hilo na italifanyia kazi, lakini nimwelekeze Mkurugenzi wa Halmashauri hii ya Ngorongoro kutenga fedha kwa awamu kupitia mapato ya ndani kwa ajili ya kuanza ujenzi wa jengo la mama na mtoto wakati Serikali Kuu inatafuta fedha kwa ajili ya ukamilishaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Twaha Mpembenwe, swali la nyongeza.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na ahadi ya muda mrefu kutoka Ofisi ya Rais, TAMISEMI kupitia Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI kipindi Mheshimiwa Ummy Mwalimu kupewa fedha shilingi milioni 200 kwenye Kata ya Bungu kwa ajili ya kuweza kumalizia kile kituo cha afya; wapigakura wangu wa Bungu wanataka kujua lini fedha hizi zitapatikana? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali yetu hii sikivu ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais msikivu inatekeleza ahadi zake kila mara ikishaahidi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba nikuhakikishie kwamba ahadi ambayo ilitolewa itatekelezwa na Wananchi wa Jimbo la Kibiti wawe na amani Serikali ipo kazini, tutahakikisha tukipata fedha hiyo tunaileta shilingi milioni 200 kwa ajili ya kazi ya kituo hicho cha afya, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge maswali mafupi nenda moja kwa moja kwenye swali.

Mheshimiwa Amandus Chinguile, swali la nyongeza.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru; ni lini Serikali itapeleka fedha kumalizia ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kassim Majaliwa kilichoko Kata ya Chiola kwenye Jimbo langu la Nachingwea? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Chinguile alishafuatilia suala la ujenzi wa kituo cha afya ambacho kimepewa jina la heshima la Mheshimiwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa na mimi nimhakikishie kwa heshima ya Mheshimiwa Waziri Mkuu mapema iwezekanavyo tumeshakubaliana na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa tutapeleka fedha hiyo kituo cha afya kikamilike, wananchi waanze kupata huduma. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Midimu, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Kata ya Luguru, Wilaya ya Itilima haina kituo cha afya wala haina zahanati; je, ni lini Serikali itajenga zahanati katika kata hiyo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, utaratibu ambao umewekwa katika ujenzi wa vituo vya afya na zahanati katika kata za kimkakati kwanza halmashauri husika inatakiwa kutambua kwamba kata ile ni kata ya kimkakati kwa kuzingatia idadi ya wananchi katika eneo husika, umbali kutoka kituo cha jirani cha kutoa huduma, lakini pia na hali ya kijiografia ya kata husika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kuleta hoja ya Kata ya

Luguru kukosa kituo cha afya na zahanati. Nitumie fursa hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kumkumbusha na kumsisitiza Mkurugenzi atekeleze wajibu wake wa kufanya tathmini, lakini ahamasishe wananchi waanze na atenge fedha za mapato ya ndani na sisi Serikali Kuu tutakwenda kuunga mkono pale wakishaanza kujenga kituo hicho au zahanati hiyo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaenda swali namba 228, kwanza halafu tutarejea swali namba 227.

Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 228

**Kuimarisha huduma katika zahanati, vituo vya afya na hospitali – Mara**

**MHE. GHATI Z. CHOMETE** aliuliza:-

Je, nini mpango wa kuhakikisha upatikanaji wa dawa muhimu, *x-ray*, *ultrasound* na maji kwenye zahanati, vituo vya afya na hospitali – Mara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha huduma za afya zinazotolewa katika ngazi ya afya ya msingi. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali ilitoa shilingi bilioni 66.7 kwa ajili ya kununua vifaa na vifaatiba. Aidha, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali imetenga shilingi bilioni 117.3 kwa ajili ya kununulia vifaa na vifaatiba katika ngazi ya afya ya msingi.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Januari, 2024 jumla ya mashine za *x-ray* 407 na *ultrasound* 425 zilinunuliwa na kufungwa katika vituo kote nchini, ikiwemo *x-ray* 15 na *ultrasound* 24 zilizofungwa katika vituo vya Mkoa wa Mara.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha usafi na upatikanaji wa maji vituoni, Serikali kupitia fedha za Benki ya Dunia na mapato ya ndani inatekeleza Programu ya Utoaji wa Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini katika mikoa 25 ukiwemo Mkoa wa Mara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024 jumla ya shilingi bilioni 27.8 zimepelekwa kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya maji, vyoo bora na vifaa vya kunawia mikono katika vituo vya kutolea huduma za afya 615 kote nchini, vikiwemo vituo 28 katika Mkoa wa Mara vilivyopelekewa jumla ya shilingi bilioni 1.43.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ghati Chomete, swali la nyongeza.

**MHE. GHATI Z. CHOMETE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kwanza nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutujengea vituo vya afya, zahanati, hospitali na hospitali za mkoa katika Mkoa wa Mara; tuna vituo vya afya 53 tumepokea *x-ray* 15, tuna upungufu wa *x-ray* 38; lakini pia tumepokea *ultrasound* 24, tuna upungufu wa *ultrasound* 29. *(Makofi)*

Je, ni lini Serikali itakamilisha kupeleka vifaa hivyo katika vituo vya afya vilivyobaki ili kusogeza huduma kwa wananchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutuletea vifaa katika Mkoa wetu wa Mara. Changamoto tuliyonayo ni watoahuduma kwa maana ya wataalam wa afya kada mbalimbali.

Je, ni lini Serikali itapeleka wahudumu au wataalam wa afya katika Mkoa wetu wa Mara ili kusogeza huduma pia kwa wananchi? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwanza nipokee pongezi za Mheshimiwa Mbunge kwa Serikali ya Awamu ya Sita na kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, lakini nimhakikishie tu kwamba kazi ya kupeleka vifaatiba tunaipeleka kwa awamu. Tulishapeleka mashine hizo za *x-ray* na anasema kuna upungufu wa *x-ray* 15 lakini pia *ultrasound* 29.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie kwamba kiutaratibu safari ni hatua, tumeanza na safari ya ujenzi wa vituo, tumepeleka watumishi, tumepeleka hivi vifaa na tutaendelea kufanya hivyo katika bajeti na ndiyo maana bajeti ya mwaka huu ni shilingi bilioni 117 kwa ajili ya vifaa hivyo. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba jambo hilo linafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, pili; kuhusiana na upungufu wa watumishi, Serikali hii imeshaajiri watumishi 18,718 wa sekta ya afya ndani ya miaka hii mitatu na Mkoa wa Mara ni moja ya mikoa ambayo imepewa kipaumbele cha watumishi hao. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kutoa kipaumbele katika Mkoa wa Mara, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Angeline Mabula swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, na mimi naomba kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya Buzuruga wakati kinaanzishwa kilikuwa kinahudumia watu 38,000 na kwa sasa kinahudumia watu zaidi ya 135,000; je, nini mpango wa Serikali kuongeza huduma ya dawa, vifaatiba na mengine ili kukidhi mahitaji ya idadi kubwa ambayo imeongezeka katika kituo hicho? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ni kweli kwamba Kituo cha Afya cha Buzuruga kwa sasa kinahudumia wananchi wengi sana na kinahudumia wananchi wengi sana baada ya kuboresha miundombinu, tumejenga majengo ya kisasa, lakini pia kuwezesha watumishi kuwepo pale. Nafahamu kwamba Mheshimiwa Mbunge amefuatilia sana kuhusiana na ongezeko la bajeti ya dawa na vifaatiba na sisi Ofisi ya Rais, TAMISEMI tulishawasiliana na Wizara ya Afya kwa ajili ya kuongeza mgao wa dawa na vifaatiba katika Kituo cha Afya cha Buzuruga.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inaendelea kulifanyia kazi hilo na sisi Ofisi ya Rais, TAMISEMI tutafuatilia kwa kushirikiana na Wizara ya Afya ili wananchi wapate dawa za kutosha, lakini pia vifaatiba vya kutosha, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Kassinge au na nani? Mheshimiwa Charles Kajege swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, mashine ya *ultrasound* iliyofungwa katika Kituo cha Afya cha Kisolya ni nzee (imezeeka) na haifanyi kazi; je, ni lini Serikali italeta mashine mpya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, vifaatiba ambavyo vimepelekwa katika vituo vyetu vya afya kikiwemo hiki kituo cha afya ambacho kimepelekewa *ultrasound,* moja ya kipaumbele ni kuhakikisha kwamba kwanza kunakuwa na matengenezo ya mara kwa mara ya vifaatiba hivyo na ndiyo maana tuna *Biomedical Engineers* katika mikoa yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba nitumie fursa hii kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Bunda kuhakikisha kwamba yule *engineer* wa *biomedical* aende akafanye tathmini ya *ultrasound* hiyo na aitengeneze, kama haitengenezeki basi tutenge fedha kwenye bajeti iwe mapato ya ndani au *central government* kwa ajili ya kupata *ultrasound* nyingine, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, Mbunge wa Mpanda Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 229

**Kada ya Askari Wanyamapori katika Halmashauri**

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI** aliuliza:-

Je, lini Kada ya Askari wa Wanyamapori katika Halmashauri itaangaliwa kama ilivyo kwa Askari wa *TAWA?*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, Mbunge wa Jimbo la Mpanda Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka 1998 Serikali ilianzisha programu ya Maboresho kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa madhumuni ya kuhamisha rasilimali na madaraka kutoka Serikali Kuu kwenda ngazi ya msingi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa lengo la kupeleka madaraka kwa umma.

Mheshimiwa Spika, kufuatia programu hiyo ya maboresho, Mamlaka za Serikali za Mitaa zilipewa uwezo wa kuajiri na kusimamia watumishi wa umma wa kada mbalimbali ikiwemo

Kada ya Usimamizi wa Wanyamapori kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo ya utumishi wa umma iliyopo.

Mheshimiwa Spika, hadi tarehe 31 Desemba, 2023 mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zina jumla ya watumishi 245 wa Kada za Usimamizi wa Wanyamapori. Aidha, maendeleo ya watumishi hawa yanasimamiwa na Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma pamoja na nyaraka mbalimbali zinazotolewa na Idara Kuu ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma kama ilivyo kwa kada nyingine.

Mheshimwa Spika, kwa kutambua majukumu ya wataalam hao, Ofisi ya Rais, TAMISEMI itaendelea kuzingatia sheria, kanuni na miongozo iliyopo katika usimamizi wa watumishi wa umma katika ngazi za Serikali za Mitaa wakiwemo wa kada ya usimamizi wa wanyamapori ili kuwa na motisha inavyostahili, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Sebastian Kapufi, swali la nyongeza.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, ninalo swali moja tu la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, linapotokea tishio la wanyama waharibifu na wakali ndipo umuhimu wa silaha unapojitokeza; Serikali inasema nini kwa maana ya kuwapatia vitendea kazi askari hawa ikiwa ni pamoja na kuboresha stahiki zao? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kama alivyouliza kwamba Serikali inatambua sana kazi na mchango mkubwa unaotolewa na maafisa hawa na ndiyo maana tumeweka utaratibu wa kuwapa motisha, lakini pia kuwawezesha kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa zaidi. Kwa hiyo,

naomba nimhakikishie kwamba tumelichukua hili suala la kuwapa vitendea kazi na tutawasiliana na Ofisi ya Maliasili na Utalii na Wizara nyingine zinazohusika ili tuweze kuona uwezekano wake, lakini pia na utaratibu unaoweza kutumika kuwawezesha kufanya kazi vizuri zaidi, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa George Mwenisongole atauliza swali kwa niaba ya Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza.

Na. 227

**Utekelezaji wa Mradi wa *TACTIC* – Halmashauri ya Mji wa Tunduma**

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE K.n.y. MHE. JULIANA D. SHONZA** aliuliza:-

Je, lini utekelezaji wa Mradi wa *TACTIC* katika Mji wa Tunduma utaanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Deo Ndejembi, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, zabuni za kupata wasanifu wa kundi la tatu *(Tier 3)* lenye miji 18 ikiwemo Halmashauri ya Mji wa Tunduma zitatangazwa mwishoni mwa mwezi huu wa Februari, 2024. Wasanifu watakapopatikana watasaini mikataba mwezi Juni, 2024 na kuanza usanifu mwezi Julai, 2024 kwa mikataba ya usanifu kwa miezi nane. Baada ya kukamilisha usanifu, zabuni za

kuwapata wakandarasi na washauri elekezi kwa pamoja zitatangazwa mwezi Aprili, 2025. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa George Mwenisongole, swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri ya Mbozi kuna Mji wa Mlowo ambao ni mji mdogo, lakini mapato yake ni makubwa karibu shilingi bilioni moja; nini mkakati wa Serikali wa kuuingiza huu mji katika Mpango wa *TACTIC?*

Mheshimiwa Spika, hapo hapo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi kuna Mji wa Vwawa na umekuwa ukipata bajeti ndogo ya *TARURA* kwa sababu wanasema upo kwenye Mpango wa *TACTIC.* Sasa nilitaka Mheshimiwa Waziri ututhibitishie; je, Mji wa Vwawa nao upo kwenye Mpango wa *TACTIC,* na lini ujenzi wa barabara za lami utaanza katika mji huo? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, nikijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mwenisongole; la kwanza hili juu ya Mji wa Mlowo pale Mbozi utaingizwa lini katika Mpango wa *TACTIC.*

Mheshimiwa Spika, mpango huu wa *TACTIC* kwenye *Tier 1* ilikuwa ni kwenye majiji pekee kote nchini; kwenye *Tier 2* ilikuwa ni kwenye manispaa; na *Tier 3* ni halmashauri za miji ambazo ni 18 hapa nchini. Kwa hiyo, Mji wa Mlowo utaingizwa kwenye mpango huu pale ambapo wao wataupadisha hadhi na kuwa ni Halmashauri ya Mji wa Mlowo.

Meshimiwa Spika, nikienda kwenye swali lake la pili, Vwawa ipo katika mpango huu wa *TACTIC Tier 3* na pale tu zabuni zitakapoanza kutangazwa maana yake na zile ambazo

zinahusika na Mji wa Vwawa na zenyewe zitakuwemo katika mpango huu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Abubakari Asenga, swali la nyongeza.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshmiwa Spika, nakushukuru na naishukuru Serikali kwa kutuletea Mkurugenzi wa Halmashauri Bi. Zahara Michuzi katika Halmashauri ya Ifakara.

Naomba kuuliza kwamba niliomba mradi wa soko, stendi na lami katika Mradi wa *TACTIC* katika Mji wa Ifakara; je, miradi hiyo ni lini itaanza?

**SPIKA:** Sehemu ya mwanzo umesema Mkurugenzi kafanyaje?

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, nimesema naishukuru Serikali kwa kutufanyia mabadiliko ya Mkurugenzi wa Halmashauri na kutuletea Mkurugenzi mpya mbunifu Bi. Zahara Michuzi anafanya kazi nzuri na ameanza vizuri, tunamuombea kwa Mwenyezi Mungu.

Swali langu...

**SPIKA:** Siyo sehemu ya swali.

Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, soko, stendi na barabara katika halmashauri ya Mji wa Ifakara na zenyewe zipo katika *Tier 3* ya Mradi huu wa *TACTIC* ambao kama nilivyosema kwenye majibu ya msingi inaenda kutangazwa mwishoni mwa mwezi huu wa Februari kuweza kupata wale ambao watafanya *design* ya mradi huu.

Mheshimiwa Spika, niwatoe mashaka Waheshimiwa Wabunge ambao wanatoka katika halmashauri za miji hii 18 ni jana tu ambapo Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu aliitisha kikao kati yetu sisi Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Wizara ya

Ujenzi pale Hazina na alizungumzia suala zima la kuona ni namna gani tunaweza tuka-*fast track* mradi huu ukaanza kabla hata ya mwaka 2025. Kwa hiyo, niwatoe mashaka Waheshimiwa wote ambao wanaguswa na mradi huu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Cosato David Chumi, swali la nyongeza.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, mradi huu ni muhimu sana na kwa namna fulani utaipunguzia *TARURA* mzigo kwa sababu unatekelezwa katika miji 47 likiwemo hata Jiji la Mbeya na Mji wa Mafinga.

Swali langu kwa Serikali, huu usanifu mpaka Aprili, 2025; je, hamuwezi kukaa na Benki ya Dunia kwa sababu huu ni mkopo mkarudisha mazungumzo nyuma mradi huu ukaanza kwa mapema kwa sababu ni mkopo na wala si msaada na tutaulipa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, kama...

**SPIKA:** Naona Waziri wa Fedha amesimama baada ya kusikia neno malipo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, majibu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa, lakini nimpe majibu Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake zuri kwamba tayari tumeshaanza mazungumzo hayo na Benki ya Dunia na Wizara ya Fedha kwa niaba ya Serikali tulishaandika barua kwa wenzetu wa Benki ya Dunia kwa ajili ya kutekeleza kuomba mapendekezo kama haya anayoyaleta Mheshimiwa Mbunge. Tunatarajia tarehe 19 tuwe na kikao sisi Wizara ya Fedha, Wizara ya TAMISEMI pamoja na wenzetu wa Benki ya Dunia kwa ajili ya kujadiliana utekelezaji wa ombi tulilolipeleka. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Chikota, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, Serikali iliahidi ku-*fast track* mradi huu kwa halmashauri zilizopo *Tier 3* na *Tier 2* na hapo umesema kwamba ujenzi utaanza mwaka 2025; je, Serikali haiwezi kurudisha muda tukaanza ujenzi mwaka 2024 kwa sababu Nanyamba tunajenga soko na stendi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nilisema hapo awali *Tier 2* tayari mikataba ilisainiwa tarehe 16 Disemba, 2023 na usanifu wake tayari umekwishaanza na tunatarajia mpaka itakapofika mwezi Juni basi kazi hizi zitatangazwa katika zile manispaa ambazo zipo kwenye *Tier 2.*

Mheshimiwa Spika, kwenye *Tier 3* amezungumza hapa Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba tarehe 19 Februari, 2024 atakutana na wenzetu wa *World Bank* kuona ni namna gani tunaweza tuka-*fast track* mradi huu ili nao uweze kuanza haraka zaidi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Japhet Hasunga, swali la nyongeza.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi, kwa kuwa Mji wa Vwawa tayari ulikuwa kwenye hiyo miji 18 ambayo ni ya kimkakati na hatua ya kwanza sisi tayari tulishaikamilisha; je, ni lini sasa Serikali itaanza kutoa hizo fedha ili tuanze ujenzi wa soko pamoja na stendi ya mkoa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, nirejee katika majibu yangu ya msingi kwamba mwisho wa mwezi huu wa Februari, 2024 ndiyo zabuni zile zitatangazwa kwa

ajili ya kuanza kufanya *design* ya miradi hiyo na itachukua miezi nane kwa ajili ya *design* halafu baada ya hapo ndiyo watatafutwa sasa wakandarasi kwa ajili ya kuanza kutekeleza kazi hizo, lakini kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba tunaangalia ni namna gani bora ya ku-*fast track* mradi huu badala ya kusubiri mpaka mwaka 2025 ili uweze kuanza haraka zaidi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Mji wa Tarime ni kati ya miji iliyopata miradi hii ya *TACTIC* ambapo wamepata miradi mbalimbali ikiwemo ujenzi wa stendi ya mabasi.

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa stendi ya mabasi ikizingatiwa ni takribani miaka mitano sasa tangu halmashauri isitishe mkataba na wananchi ambao walikuwa wamelipia maduka 100 kuzunguka stendi kwa shilingi 480,000 kwa kila duka?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, ni kweli Halmashauri ya Mji wa Tarime ipo katika kundi hili la tatu *(Tier 3)* ya mradi huu wa *TACTIC* na zabuni za kupata wasanifu wa kundi hili la tatu zitatangazwa mwishoni mwa mwezi huu wa Februari.

Mheshimiwa Spika, jumla kwenye mradi huu katika hii miji 18 una zaidi ya kilometa 71 za lami ambazo zitajengwa kwenye maeneo yote ya halmashauri ya miji ambayo ipo katika mradi huu. Vilevile, kuna stendi na masoko ambayo yatajengwa kulingana na uhitaji wa halmashauri zile za miji. Kwa hiyo na Tarime vilevile wamo katika kundi hili na tutakapoanza utekelezaji tu basi Wananchi wa Tarime watafaidika na mradi huu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge Wa Chumbuni, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle.

Na. 230

**Kutangaza miradi inayotekelezwa nchini**

**MHE. EDWIN E. SWALLE K.n.y. MHE. USSI SALUM PONDEZA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutangaza miradi mikubwa inayotekelezwa nchini ili wananchi ikiwemo wa vijijini waweze kufahamu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara kwa niaba ya Waziri wa Mipango na Uwekezaji Mheshimiwa Exaud Kigahe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Chumbuni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatumia njia mbalimbali zilizoainishwa katika Mkakati wa Mawasiliano wa Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/2022-2025/2026) katika kutangaza utekelezaji wa miradi mikubwa inayotekelezwa nchini. Njia hizo ni pamoja na vyombo vya habari vya runinga kupitia vipindi maalum kama vile Tunatekeleza *(TBC)* na Kurunzi ya Reli *(Reli Online TV),* redio na mitandao ya kijamii, maonesho mbalimbali ya biashara ya Kimataifa kama Sabasaba na Maonesho ya Kilimo maarufu Nanenane.

Mheshimiwa Spika, aidha nitumie nafasi hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kutumia mikutano yenu na wananchi

majimboni kutoa elimu na uelewa kwa jitihada zinazofanywa na Serikali katika utekelezaji wa miradi hii mikubwa kwa kuwa ni jukumu letu sote, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, swali la nyongeza.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya maswali mawili madogo ya nyongeza.

Swali la kwanza, Mkoa wa Njombe ni kati ya mikoa ambayo ina ardhi nzuri ambayo inafaa kuwa na miradi ya kimkakati; je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha Mradi wa Soko la Kimataifa kama mradi wa kimkakati Mkoani Njombe?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, sisi kama Bunge na wananchi tunafahamu kwamba ipo miradi mingi ya kimkakati nchini ikiwemo Bwawa la Mwalimu Nyerere na hili bwawa sisi kama Wabunge tunajua kwamba Serikali ya Awamu ya Sita imekuwa inafanya kazi kubwa huu mradi ufike mwisho; na kumekuwa na taarifa nyingi mtandaoni pengine Serikali leo hii tarehe 16 Februari wangeweza kuzindua mashine mbili za mradi huu wa Mwalimu Nyerere; je, ni ipi kauli ya Serikali juu ya Mradi wa Mwalimu Nyerere? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, ni kweli Mkoa wa Njombe ni moja ya mikoa ya kimkakati kwa maana ya swali lake la kwanza ambako ndiyo sehemu kubwa tunategemea kwenye sekta ya kilimo na tayari Serikali ina mkakati wa kujenga Soko la Kimataifa pale Makambako ambapo kuna zaidi ya shilingi bilioni nne iliyowekwa kwa ajili ya ujenzi na eneo limepatikana. Kwa hiyo, tutajenga Soko ya Kimataifa pale Makambako ambao ni Mkoa wa Njombe ambalo litasaidia kwa masoko ya mikoa hii ya Iringa, Mbeya na Njombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake la pili la mradi huu mkubwa wa Mwalimu Nyerere wa uzalishaji umeme naamini

Serikali kama ambavyo imetoa taarifa mara nyingi, uzalishaji utaanza na tunaendelea kutoa taarifa kadiri ambavyo hatua mbalimbali za kuanza uzalishaji umeme katika bwawa hilo la Mwalimu Nyerere hatua mbalimbali zitakavyokuwa zinafikiwa tutawataarifu na kuwajulisha wananchi, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati naona umesimama.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante na namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri kwenye swali la pili la nyongeza, lakini napenda kuongezea maelezo hayo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Mwalimu Nyerere ni mojawapo ya miradi ya kimkakati ambayo inatekelezeka kwa weledi mkubwa sana. Wote tunafahamu mwezi wa sita mwaka huu ndipo ambapo tulitegemea kuwasha mtambo namba tisa kwa mara ya kwanza, lakini kwa jitihada za Serikali na wakandarasi tuliweza kusogeza ratiba ya kuwasha mtambo huu namba tisa mpaka mwezi huu wa pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nilifahamishe Bunge lako Tukufu kwamba jana tarehe 15 Februari tumefanikiwa kufanya majaribio kwa ukamilifu kwenye mtambo namba tisa na tumeutembeza mpaka kwa uwezo wake wa mwisho (megawati 235). Majaribio kama ambavyo tulisema ratiba ya awali kwamba majaribio yatakamilika tarehe 16 Februari, kwa siku ya jana tumefanikisha majaribio hayo kwa kiasi kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi wataalamu wetu wanaendelea na *final fine tuning* pamoja na kuweka ulinzi wa mtambo kwa ajili ya kuweza kuendelea kwenye ratiba ya uzalishaji. Tuliahidi mwezi huu wa pili tuna ratiba ya kuzindua mtambo huu na ratiba hii kwa kadri ambavyo tulisema iko pale pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa uvumilivu na kwa kuendelea

kutuvumilia. Tunataka tuwahakikishie ratiba ambayo tulisema ya uzinduzi wa mradi ipo kama ambavyo tulikuwa tumeipanga.

Mheshimiwa Spika, habari ya mwisho ni kwamba mtambo namba nane tuliahidi Mwezi wa Tatu na wenyewe utaanza kuzalisha umeme na ratiba ipo pale pale, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, swali dogo; mgao wa umeme unaisha lini Mheshimiwa? Tukishazindua mwezi huu au tukizindua wa Mwezi wa Tatu?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, matumizi ya umeme yanategemeana na matumizi ya kila siku, lakini tukizalisha mwezi huu mgao kwa kweli utakuwa umepungua kwa kiasi kikubwa, lakini kwa sababu ni megawati 235 na Mwezi wa Tatu ni megawati 235, ni megawati 470. Uhakika ni kwamba kufikia Mwezi wa Tatu mgao utakuwa umeisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu tunarudi hapa Mwezi wa Nne, msije mkaanza na swali; umeme ulisema Mwezi wa Tatu, acha tuipe Serikali muda; kwa maana ipi? Wao walijipanga Mwezi wa Sita wakarejesha nyuma Mwezi wa Pili, tunawapongeza sana Serikali na mmerejesha mpaka mwezi wa tatu kwa hizo mashine zote kukamilika.

Bunge linawapa mpaka Mwezi wa Sita ili Mwezi wa Sita ule Bunge linapokuwa hapa mgao uwe umeisha, kwa sababu ninyi mmerudisha ratiba nyuma na tunawashukuru na tunawapongeza sana kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kuliko watu waambiwe Mwezi wa Tatu halafu kukawa na siku mbili tatu za kusogea mbele basi tusogeze Mwezi wa Sita halafu mambo yakae vizuri. *(Makofi)*

Tunawatakia kila la kheri na ahsanteni sana kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Ally Mchungahela.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kumekuwa na ucheleweshaji wa maamuzi katika miradi mbalimbali ambapo wawekezaji wanakuja kutaka kuwekeza na mfano halisi, Mradi wa Magadi Soda Engaruka, mradi huu kuna mwekezaji alishajitokeza tangu mwaka 2021 huko, ameonesha nia zote za kuhakikisha kwamba anawekeza na pesa ya kuwekeza ipo, lakini kumekuwa na ukimya usiokuwa na ulazima.

Je, Serikali inaona sawa kweli kuwachunia wawekezaji namna hii hata pale ambapo wao wana uwezo wa kufanya shughuli hizi pasipokuwa na changamoto zozote zile?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, ni kweli Mradi wa Engaruka wa Magadi Soda ni moja ya miradi ya kimkakati ambayo Serikali tumeweka kuitekeleza katika mpango ule wa miaka mitano, Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa. Serikali kwa ujumla tumeshafikia hatua nzuri ikiwa ni pamoja na kufanya tathmini ya kulipa fidia katika eneo lile ili baada ya hapo tukikamilisha tuweze kuutangaza.

Mheshimiwa Spika, nasema mbele ya Bunge lako kwamba hoja ya Mheshimiwa Mchungahela ya kuona namna gani tutashirikisha sekta binafsi kwa maana ya *PPP* nalo pia lipo kwenye mipango yetu. Tuko kwenye hatua nzuri na tutakapokamilisha tathmini hiyo tutaweza kuutangaza na wadau wote ambao wanataka, kama tutakuwa tumeamua kuingia *PPP* au wengine ambao tutakuwa tumeshalipa sisi kama fidia watashindanishwa, halafu tutapata mwekezaji mzuri ambaye ataweza kufanya kwa faida ya Taifa hili kwa maana ya ile *win-win situation.*

Mheshimiwa Spika, Serikali inafanya tathmini hatua za mwisho ili tuweze kutangaza mradi huo mkubwa pamoja na miradi mingine, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Fedha naona umesimama.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu swali kikamilifu isipokuwa nataka kuongeza na kuweka kumbukumbu sawa kwenye eneo moja ambalo Mheshimiwa Mbunge amesema Serikali inachunia wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali haichunii wawekezaji isipokuwa ina wajibu wa kulinda maslahi mapana ya nchi yetu. Kwa hiyo, pale ambapo tunaona maslahi ya nchi bado hayajatimia tunakuwa na muda wa kuweza kuitafuta hiyo *win-win situation* ili maslahi mapana ya nchi yetu yawe yamelindwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Seif Khamis Said Gulamali, Mbunge wa Manonga, sasa aulize swali lake.

Na. 231

**Mawasiliano ya simu - Manonga**

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI** aliuliza:-

Je, lini vijiji vya Ncheli, Matinje na Mwakabuta – Manonga vitapata mawasiliano ya simu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Nape Nnauye, majibu.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Seif Khamis Said Gulamali, Mbunge wa Manonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote yaani *UCSAF* ilikijumuisha Kijiji cha Matinje Kata ya Mwashiku katika zabuni ya Mradi wa Tanzania ya Kidigitali na kumpata mtoa huduma Kampuni ya Vodacom. Aidha, ujenzi wa minara ukiwemo huu wa Mradi wa Tanzania ya Kidijitali unaendelea.

Mheshmimiwa Spika, Serikali kupitia *UCSAF* itafanya tathmini ya kubaini mahitaji halisi ya Kijiji cha Ncheli Kata ya Sungwizi na Kijiji cha Mwakabuta Kata ya Ugaka na hatimaye kuviingiza katika orodha ya miradi itakayotekelezwa kulingana na upatakanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Seif Gulamali, swali la nyongeza.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri juu ya utekelezaji wa minara, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, tumejenga minara pale Imalilo pamoja na Choma, Mnara wa Imalilo hata ukiwa Imalilo pale pale haushiki, lakini Mnara wa Choma ni miaka sita leo haujawashwa, ni mnara wa Halotel; je, ni lini minara hii itaweza kuwashwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, katika Kata ya Mwisi kuna minara ya mitandao mingi ikiwemo Vodacom, Airtel pamoja na Tigo; je, ni lini tutapata huduma ya *4G?*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Seif Gulamali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mnara wa Choma ni mnara ambao ulijengwa na Halotel bila ya fedha za Serikali, ulijengwa kwa

mahitaji yao kama Halotel na kwa bahati mbaya baada ya kuujenga nadhani walifika mahali wakaona hauna biashara kwa hiyo wakaacha kuendelea nao.

Mheshimiwa Spika, nawaagiza *UCSAF* waende wakaangalie mahitaji na kama yapo basi tutenge fedha kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote tuwaongezee Halotel ili mnara huu uwashwe na uanze kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, Mnara wa Imalilo ambao umejengwa na *TTCL*, kuna minara 99 maeneo mbalimbali nchini ambayo ilijengwa na *TTCL* kwa kushirikiana na Kampuni ya *Parallel Wireless*, minara hii bahati mbaya sana teknolojia iliyotumika inasumbua ufanyaji kazi wake na baadhi ya Wabunge watakuwa wanajua.

Mheshimiwa Spika, tumekubaliana na wajenzi waliojenga hii minara na wameanza kurekebisha, kasi yao ni ndogo lakini wameanza kurekebisha kwa kuondoa teknolojia iliyotumika na kuweka teknolojia ambayo inalingana na maeneo yako, maeneo ya Ruvuma, Kigoma na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la mwisho la Eneo la Mwisi ambapo anaomba tuongeze uwezo wa minara iliyopo maeneo yale na hili nawaagiza watu wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote kwenda kufanya tathmini ya mahitaji ya kupandisha hadhi minara hiyo, na tutatenga fedha kadri itakavyopatikana na tutaongeza uwezo wa minara ya eneo husika. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nimewaona, maswali mafupi moja kwa moja kwenye swali na majibu mafupi.

Mheshimiwa Shally Raymond.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, ni lini Kijiji cha Shinga katika Kata ya Uru Kusini ambacho nimeshawahi kukueleza Mheshimiwa Waziri kitapatiwa mawasiliano ya simu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, nilishawahi kupokea maombi kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge juu ya kijiji hiki na nilimuahidi na naomba kuahidi Bunge lako Tukufu kwamba tunayo minara karibu 670 ambayo iko kwenye mchakato sasa hivi na mnara mmoja tutapeleka kwenye Kijiji cha Mheshimiwa Mbunge alikouliza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante, Wahadzabe uliwaahidi watajengewa mnara katika vijiji vyao vya Dumanga; je, ni lini utapeleka mnara pale?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa vijiji alivyovitaja havikuingia kwenye Mradi wa Tanzania ya Kidigitali, minara inayofuata hii 600 imelenga ku-*cover* maeneo yote ya Waheshimiwa Wabunge ambayo hayakupata mgao kwenye mradi wa Tanzania ya kidigitali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Mtinga, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Kikonda, Kata ya Kikonda na Kijiji cha kule Kata ya Mwangeza vilikuwa kwenye vijiji 700 lakini mpaka sasa ujenzi haujaanza, ni lini ujenzi utaanza katika vijiji hivi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Francis, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba minara 758 imeanza kujengwa, lakini haiwezi kuanza kujengwa kwa wakati mmoja kwa nchi nzima. Kwa hiyo, kuna upande ambao tayari imeshaanza kujengwa, lakini kuna mahali najua na Wabunge wengi

wamekuja na wakaniuliza, yako maeneo mengi ambayo haijaanza kujengwa, lakini tumeshakamilisha hatua za awali za kupata vibali, maeneo na kuwalipa wakandarasi, isipokuwa wanajenga kwa awamu ndiyo maana inawezekana vijiji alivyovitaja havijafikiwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Almas Maige, swali la nyongeza.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana; je, ni lini Vijiji vya Mbeya, Umbo na Busenda katika Kata ya Igulungu vitapata mawasiliano ya simu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maige, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya iliyotokea na hii ni kwa Wabunge wengi, wakati tunagawa minara kwenye Mradi wa Tanzania ya Kidigitali wataalam wetu waligawa minara wa kuzingatia Wilaya badala ya majimbo na ndiyo maana yako majimbo ambayo kwa kweli hayakupata mgao unaoridhisha. Ninawaahidi Waheshimiwa Wabunge kwamba, kwenye hii minara 600 na kitu ambacho tunaendelea nacho sasa hivi tutasawazisha tatizo hili na kwa hiyo, hata wale wengine ambao hawakupata minara kwa mujibu wa mgao wa majimbo tutahakikisha jambo hili linazingatiwa kwenye mgao unaofuata. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Mchafu, swali la nyongeza.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Tengerea, Kata ya Tengerea Wilayani Mkuranga hakuna mawasiliano ya simu; ni ipi kauli ya Serikali juu ya kadhia hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, nawaagiza *UCSAF* waende wakafanye *survey* kwenye eneo husika ili kama kuna uwezekano

wa kuongeza nguvu mnara wa karibu ukahudumia kijiji hichi ufanyike na kama haiwezekani basi tuweke utaratibu wa kujenga mnara mpya kwenye eneo alilolitaja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Josephat Kandege, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa mujibu wa majibu ya Mheshimiwa Waziri ni kwamba maeneo mengi ambayo Halotel wamejenga kuna minara haifanyi kazi ikiwa ni pamoja na Eneo la Kipanga; nini kauli ya Serikali kuhusiana na hiyo minara ambayo haifanyi kazi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, siyo kweli kwamba minara mingi iliyojengwa na Halotel haifanyi kazi, isipokuwa nilichokisema hapa ni kwamba, kuna baadhi ya minara ambayo kwa kweli ilikuwa inasimamiwa na *TTCL* ilijengwa na Kampuni ya *PW* ambao walitumia teknolojia ambayo uwezo wake unasumbua kwenye baadhi ya maeneo na hasa yale maeneo ambayo hayana umeme na wameweka *solar,* mnara unafanya kazi masaa manne badala ya masaa 24. Tumezungumza nao tufanye mabadiliko ya teknolojia iliyotumika ili minara ifanye kazi masaa 24 ikiwemo eneo ambalo Mheshimiwa Mbunge amelitaja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Michael Mwakamo, swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Spika, Jimbo la Kibaha Vijijini tulikuwa kwenye orodha ya minara 730 mwaka jana, hadi sasa wakandarasi hawajafika kwenye maeneo yetu; nini kauli ya Serikali ili wakandarasi hao waje kufanya kazi kwenye maeneo hayo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, eneo alilolitaja Mheshimiwa Mbunge ni katika maeneo ambayo tumeshakamilisha hatua zote za awali kwa maana ya kupata eneo, kuingia mkataba na wenye eneo, kulipa malipo ya awali na kupata vibali. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, wakati wa Sherehe za Muungano, tarehe 26 Aprili, 2024 tutawasha minara mingi, karibu nusu ya minara ambayo imeanza kujengwa itakuwa imefikia wakati mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunataka tutumie Sherehe za Muungano kuwasha minara mingi ambayo itakuwa tayari na ile ambayo itakuwa bado basi tusukumane nayo. Lengo letu ni kwamba tunapoelekea mwisho wa mwaka huu kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa, minara hii iwe imeanza kutoa huduma ili irahisishe utekelezaji wa shughuli za maendeleo kwenye maeneo husika. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani, Mbunge wa Tandahimba, sasa aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 232

**Kulipa madeni ya wazabuni wa pembejeo za kilimo**

**MHE. KATANI A. KATANI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kulipa madeni ya muda mrefu ya wazabuni wa pembejeo nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa David Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani, Mbunge wa Jimbo la Tandahimba, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kulipa madai ya wazabuni wa pembejeo za kilimo nchini. Katika msimu wa mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara imelipa jumla ya shilingi bilioni 154.4 kwa wazabuni mbalimbali waliosambaza pembejeo katika msimu wa mwaka 2015/2016. Vilevile, Serikali imelipa jumla ya shilingi bilioni 112 kwa wazabuni waliosambaza pembejeo za zao la korosho.

Mheshimiwa Spika, madeni ya wazabuni wa pembejeo za ruzuku kwenye zao la korosho hulipwa mara baada ya mauzo ya korosho ghafi kukamilika mwezi Aprili, 2024.

**SPIKA:** Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani, swali la nyongeza.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ucheleweshwaji wa fedha hizi huwasababishia wazabuni riba kubwa kwenye mabenki; je, Serikali iko tayari kukaa na wazabuni kwa ajili ya kuwalipa fidia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa *export levy* ipo kwenye korosho pekee, Serikali iko tayari kuachia fedha hizi za *export levy* zibaki kwenye korosho ili ziweze kuwalipa wazabuni fedha zao zote? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, natambua swali la msingi la Mheshimiwa Mbunge kuhusu kulipa fidia suala hili kidogo lipo kimkataba na niseme tu kwamba kama jambo lipo kimkataba Serikali imekuwa ikilipa fidia, lakini kama halipo kimkataba Serikali imekuwa ikilipa kulingana na makubaliano. Kwa hiyo, kwenye jambo hilo Serikali itandelea kuzingatia makubaliano ambayo wazabuni na Serikali wameingia kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu fedha ambazo ni za *export levy* kutakiwa zirudi Bodi ya Korosho; jambo kama hili nilishajibu katika Bunge hili Tukufu, ni kwamba Wizara ya Kilimo pamoja na Wizara ya Fedha bado tupo kwenye majadiliano ya pamoja kuona namna bora ambayo hizi fedha tunaweza tukazirudisha na kuzipeleka Bodi ya Korosho ili ziweze kusaidia kuendeleza zao la korosho. Kwa hiyo, bado mchakato unaendelea na tukishakamilisha tutatoa taarifa, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, swali la nyongeza.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya swali la nyongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kusikitisha kwamba Wakulima wa Urambo waliuza tumbaku yao kwa muda mrefu, lakini inasikitisha hadi leo hawajalipwa zaidi ya shilingi milioni 539; je, Serikali inasema nini kuhusu kuhakikisha wakulima hawa wanapata fedha zao? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, bahati nzuri swali kama hili nilishalijibu wiki iliyopita ndani Bunge lako Tukufu na sehemu ya majibu yangu ni kwamba na Mheshimiwa Mbunge anatambua kwamba, jambo hili lilikuwa limepelekwa Mahakamani; wale wazabuni wote waliotakiwa kuwalipa wakulima. Sisi kama Wizara tumeji-*commit* kurudi na kukaa mezani na wale wazabuni ili kuhakikisha tunaharakisha mchakato ili waweze kulipa. Kiukweli jambo hili mpaka muda huu ninavyozungumza liko Mahakamani, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, swali la nyongeza.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Spika, mwaka 2018/2019 Serikali ilisimamia zoezi la kununua korosho katika Ukanda wa Kusini, kuna baadhi ya wafanyabiashara waliosafirisha korosho kutoka vijijini kwenda kwenye maghala makuu walikuwa hawajalipwa na mpaka leo wasafirishaji hawa hawajalipwa.

Je, ni lini Serikali itawalipa wasafirishaji hawa kwa malipo yale ambayo walitakiwa walipwe? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, suala la Mheshimiwa Mbunge la wasafirishaji waliotoa korosho kutoka kwa wakulima kwenda katika maghala makuu ni sehemu ya yale madai ambayo wanadai wazabuni hao. Kwa hiyo, kuna sehemu wameshalipwa na kuna baadhi bado hawajalipwa na mchakato unaendelea. Sisi kama Wizara kupitia Bodi ya Korosho tunaweza tukawa-*guarantee* tu kwamba watu hao wote watalipwa kwa kadri ambavyo sisi tunaendelea kufuatilia nafikiri kabla ya msimu wa mwaka huu wa korosho, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 233

**Mpango wa kuendeleza kilimo nchini**

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA K.n.y. MHE. MWANTUMU DAU HAJI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza kilimo nchini?

**SPIKA:** Aliyeuliza swali kwa niaba ya Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, ni Mheshimiwa Maimuna Mtanda.

Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na utekelezaji wa mipango na mikakati mbalimbali ya kuendeleza sekta ya kilimo

nchini ikiwemo Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Ajenda 10/30 ambayo inalenga kuchochea ukuaji wa kilimo kufikia asilimia 10 ifikapo mwaka 2030. Utekelezaji wa programu hizo unaenda sambamba na Sera ya Taifa ya Kilimo ya mwaka 2013, Sera ya Taifa ya Umwagiliaji ya mwaka 2010 na Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa mipango hiyo kuna malengo ya kimkakati ambayo Wizara imejiwekea ikiwemo kujitosheleza kwa mahitaji ya chakula ndani ya nchi na kuuza ziada nje ya nchi, kuongeza mauzo ya mazao nje ya nchi kutoka Dola za Kimarekani bilioni 1.2 hadi Dola za Marekani bilioni tano ifikapo mwaka 2030, kuongeza idadi ya mashamba makubwa, kuongeza eneo la umwagiliaji kutoka hekta 727,280.6 mwaka wa fedha 2022/2023 kufikia hekta milioni 8.5 sawa na ongezeko la asilimia 50 ya eneo lote linalolimwa nchini ifikapo mwaka 2030 ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo kupitia kilimo cha umwagiliaji kutoka asilimia 10 hadi asilimia 50.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mikakati hiyo inaendelea vizuri ambapo hadi sasa mafanikio mengi yamepatikana yakiwemo nchi kujitosheleza kwa chakula kwa asilimia 127, kuongezeka thamani ya mazao ya kilimo kwenda nje kutoka bilioni 1.2 mwaka 2020 hadi bilioni 2.3 mwaka 2023, ukamalishaji wa miradi ya umwagiliaji ya hekta 95,000 zilizoanza mwaka wa fedha 2022/2023 kuendelea pamoja na kuanza miradi mipya kwa mwaka 2023/2024 yenye hekta 95,000, kuweka mifumo bora ya upatikanaji wa pembejeo pamoja na kutoa ruzuku za mbolea na mbegu kwa baadhi ya mazao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna Mtanda, swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, pamoja na majibu mazuri ya Serikali naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kumekuwa na changamoto ya upatikanaji wa sukari hapa nchini kwa muda mrefu, lakini tunayo mabonde mazuri ambayo yanaweza kufaa kwa kilimo cha miwa, kitu ambacho kinaweza kuongeza uzalishaji ikatukwamua katika hali

hii. Kwa mfano, tunalo Bonde la Kitere kule Mtwara ambalo ni zuri kwa kilimo cha miwa. Upi mkakati wa Serikali kwenda kuwekeza kwenye Bonde la Kitere ili kuzalisha miwa ambayo itakuja kuzaa sukari baadae?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kumekuwa na anguko la uzalishaji wa zao la korosho hapa nchini kwa misimu mitatu mfululizo; ukianza na msimu wa 2020/2021 – 2022/2023, ukiangalia uzalishaji ni kati ya tani 210 – 182 wakati tulishafikia tani 300 huko nyuma ya uzalishaji.

Naomba kuiuliza Serikali, imeshafanya utafiti wa kubaini anguko la uzalishaji wa korosho hapa nchini linasababishwa na jambo gani? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, jambo la kwanza, Mheshimiwa Mbunge ameuliza maswali ya msingi, kwa mfano katika swali lake la kwanza, anataka kujua mkakati wa Serikali kwenye mabonde na amejikita zaidi katika zao la miwa.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie tu kwamba Wizara ya Kilimo moja ya mikakati yetu mikubwa tuliyonayo sasa hivi ni kuhakikisha yale mabonde yote yanayofaa kwa ajili ya kilimo cha miwa, kwa ajili ya sukari, tukatumia kwa ajili ya kufanya hivyo na baadhi ya mabonde ambayo mpaka sasa hivi yameshapata Wawekezaji likiwemo Bonde la Mto Rufiji, kuna mwekezaji pale *Lake Agro* ambaye anawekeza kiwanda pale kwa ajili ya kulima miwa, lakini vilevile atatengeneza sukari kutokana na miwa ile.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika Eneo la Kasulu pale, kuna *Mufindi Paper Mills* na wenyewe vilevile wanawekeza katika bonde kule katika upande wa Kasulu. Kwa hiyo, huo ni mchakato ambao tunaendelea nao ili kuhakikisha tunakidhi adha ya sukari nchini ambayo imekuwa ikijotokeza mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kupungua kwa uzalishaji katika zao la korosho, kumekuwa na sababu nyingi na wala siyo sababu

moja na miongoni mwa sababu ni pamoja na *variation* ya bei. Bei imekuwa inafanya baadhi ya wakulima kushindwa kuendelea kuwekeza katika zao la korosho, upatikanaji hafifu wa pembejeo na wakati mwingine pembejeo kuchelewa kufika kwa wakati. Mbegu ambayo tumekuwa tukitumia ni ile ile ya asili ambayo uzalishaji wake umeendelea kushuka kutokana na muda.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kuna sababu mbalimbali tumezibaini na Bodi ya Korosho chini ya Wizara ya Kilimo, tumeendelea kuhakikisha kwamba katika mikakati tuliyonayo, ni kuhakikisha tunalifufua upya zao hili na ndiyo maana utaona tumetambua maeneo mengi nchini, mikoa zaidi ya 17 kuongeza upandaji wa korosho, kutumia mbegu ya kisasa ili tuongeze uzalishaji katika zao la korosho. Kwa hiyo, mikakati ipo na tumedhamiria kwamba jambo hili tunaliweza na tutalimaliza kwa wakati, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali mafupi, shukrani kwangu nimeshazipokea tayari. Mheshimiwa Ritta Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, Serikali iliahidi kuwapatia wakulima ruzuku mbegu ya parachichi wakiwemo wa Mkoa wa Iringa, je, lini ahadi hiyo itatimia? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo, imekuwa ikitoa ruzuku ya mbegu za parachichi kwa wakulima katika maeneo mbalimbali. Changamoto ambayo tunaipitia sasa hivi ni kwamba uzalishaji wa mbegu kidogo umekuwa uko chini, kwa hiyo, hata zile zinazozalishwa bado haziwatoshelezi wakulima wote na hii yote inatokana na suala la kibajeti. Kwa hiyo, sisi tutaendelea kuongeza fedha ili tuhakikishe ruzuku katika mbegu ya parachichi inafikia wakulima wote nchini, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Tunza Malapo, swali la nyongeza.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Spika, miongoni mwa matatizo ya kilimo nchini kwetu ni kukosa tija, mtu analima eneo kubwa, lakini anavuna kidogo; nataka kujua mkakati wa Serikali ukoje kuongeza tija ya kilimo hapa nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, jukumu letu kama Wizara katika kuongeza tija, ndiyo maana umeona sasa hivi tunaongeza Maafisa Ugani kwa ajili ya kuwaelimisha wakulima wetu kote nchini ili waweze kulima kilimo cha kisasa, chenye tija, watumie eneo dogo, wapate mavuno makubwa, lakini vilevile waweze kuongeza thamani, badala ya kuuza mazao ghafi, waweze kuuza mazao ambayo yameongezwa thamani ambayo yataongezea kipato kikubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuongeza kipato cha mkulima, maana yake unaongeza Pato kwa Taifa na maana yake tutakuwa tumesaidia wote kwa ujumla. Kwa hiyo, mikakati tuliyonayo ni mingi na tutaendelea kuelimisha wakulima kwa ukaribu zaidi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Salim Alaudin Hasham, Mbunge wa Ulanga, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Dennis Londo.

Na. 234

**Barabara ya Liwale – Mahenge**

**MHE. DENNIS L. LONDO K.n.y. MHE. SALIM A. HASHAM** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani kujenga barabara ya kiwango cha lami kutoka Liwale hadi Mahenge kuunganisha Mkoa wa Morogoro na Mikoa ya Kusini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salim Alaudin Hasham, Mbunge wa Ulanga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 2 Januari, 2024 Serikali kupitia *TANROADS* ilitangaza zabuni ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Barabara ya Nachingwea – Liwale – Ilonga – Mwaya hadi Mahenge. Taratibu za manunuzi zinaendelea na zinatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilika kwa kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na kwa kuzingatia matokeo ya taarifa ya athari za mazingira kwani sehemu kubwa inapita ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Selous, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hiyo, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tupunguze sauti kidogo, tupunguze sauti kidogo.

Mheshimiwa Dennis Londo.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Hifadhi hiyo ya Selous, Mikumi na Ruaha zimepata zaidi ya Dola za Kimarekani milioni 150 kukuza utalii Kanda ya Kusini. Kama ilivyo umuhimu wa Barabara ya Kilosa kuja Mikumi ndivyo ulivyo umuhimu wa barabara hii ambayo ninaitaja.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kushirikiana ama kuunga mkono jitihada za Wizara ya Uchukuzi na Maliasili na Utalii katika kukuza utalii kwa kuzikamilisha barabara hizi kwa wakati?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, Serikali ina mpango gani wa kuunganisha...

*(Hapa Mheshimiwa Waziri alipita mbele ya Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, tafuta kiti ukae, anayezungumza yuko huko mbele. Mheshimiwa Dennis Londo.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kuunganisha Mkoa wa Morogoro na Mkoa wa Dodoma kwa Barabara ya kutoka Ruaha Mbuyuni kupitia Malolo – Uleling'ombe – Kibakwe hadi Mpwapwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana katika mwaka huu wa bajeti, kutokana na umuhimu kama alioutaja wa uwekezaji uliofanyika, ndiyo maana katika bajeti yetu ya Wizara, tulitenga fedha kwa ajili ya kuanza usanifu wa barabara hiyo na tuna hakika kama tulivyosema kwenye jibu la msingi, kama hakutakuwa na changamoto yoyote ya kimazingira pamoja na wenzetu hawa ambao tunashirikana nao, nina hakika barabara hii itaanza kujengwa baada ya matokeo ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya pili aliyoisema ya Ruaha Mbuyuni kuja kuunganisha na Mkoa wa Dodoma, kama ilivyo kwenye swali la kwanza, naomba kutoa maelekezo tu kwa Meneja wa Mkoa wa Morogoro, Iringa na Dodoma chini ya *TANROADS* Makao Makuu waweze kufanya *reconnection survey* ya barabara hii ili kuona kama itaweza kuanza kujengwa, ahsante.

**SPIKA:** Narejea tena, maswali mafupi, moja kwa moja kwenye swali, shukrani mimi nimeshazipokea.

Mheshimiwa Subira Mgalu, swali la nyongeza.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi; je, Serikali imefikia wapi kwenye mpango wa usanifu wa barabara mpya ya Chalinze – Rufiji kama ambavyo iliridhiwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja sasa hivi tunaendelea nayo, iko kwenye mpango na mwaka huu taratibu zote za kutangaza *tender* zinaendelea kufanyika kuanza kuisanifu hiyo barabara, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Oliver Semuguruka, swali la nyongeza.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Kyaka – Katoro – Ibwera hadi Kyetema; barabara hii inaunganisha Wilaya mbili Misenyi na Bukoba Vijijini? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja ina umuhimu wake na tuliiweka kwenye bajeti. Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii tutaanza kuijenga kwa awamu tukianza na kilometa 10 bila kusahau daraja ambalo ni korofi sana, Daraja la Kalega, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Amar, swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri, Wana-Nyang'hwale wanasubiri majibu kutoka kwako kama ulivyoahidi kwamba barabara yao upembuzi yakinifu utakamilika Mwezi wa Nne, je, Mwezi wa Nne kweli upembuzi yakinifu utakamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kama nilivyokuwa nimeahidi, tulitegemea iwe hivyo na sijafuatilia kama itakamilika Mwezi wa Nne, lakini mpango ni kuikamilisha Mwezi wa Nne kama tulivyokuwa tumeahidi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Malleko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami Barabara ya Loa kutoka Holili hadi Tarakea - Rombo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, tumeshakamilisha usanifu wa kina na tumeweka kwenye mpango ili ianze kujengwa kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph George Kakunda, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuiuliza Serikali, je, ni lini itaanza ujenzi kwa kiwango cha lami Barabara ya Ipole – Rungwa ambayo ni sehemu ya *trunk road number* nane?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja ya kutoka Ipole – Rungwa, ni pamoja na Barabara ya Itigi – Rungwa kwenda Makongorosi ambayo Mheshimiwa Rais wakati yuko Singida aliitolea maelekezo ili iweze kujengwa yote kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, swali la nyongeza.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, ni lini Barabara ya Bugene – Nkwenda mpaka Isingiro itaanza kujengwa baada ya kuahidiwa kwa muda mrefu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kuna vijiji sijavisikia vizuri.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, Barabara ya Bugene – Rwabwere - Nkwenda mpaka Murongo kwa kupitia ukanda siyo tena wa unaoujua wa Uganda kupitia ukanda wa pili ambao ni barabara inayounganisha Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa lakini pia na Wilaya ya Karagwe. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ...

**SPIKA:** Umesema siyo anayoijua, kwa hiyo, hiyo uliyotaja haijui?

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, huwa anaongelea Barabara ya Murongo ikiunganisha Uganda pamoja na Tanzania, lakini sasa naongelea barabara ya pili ambayo inatoka Bugene, inakuja Rwabwere, inakuja Nkwenda, inakuja Halmashauri inaenda mpaka Isingiro.

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, labda tu niweke suala hili vizuri, barabara zote mbili zinatokea Murongo, ipo moja inapita Nkwenda na nyingine inapita upande mwingine, kwa hiyo, zote zinaenda Murongo. Barabara aliyotaja Mheshimiwa Mbunge, kilometa 50 tunategemea kusaini, kuanza na kilometa 50 na tayari tulishapata mkandarasi tunasubiri *signing* kilometa 50, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aleksia Kamguna, swali la nyongeza.

**MHE. ALEKSIA A. KAMGUNA:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itajenga barabara ya kuanzia Lupilo – Malinyi hadi Namtumbo kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, barabara aliyoitaja ipo kwenye mpango ule mkubwa wa *EPC + F* na anafahamu kwamba tulishasaini mkataba na wahandisi wako uwandani kukamilisha taratibu ili iweze kuanza kujengwa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa George Natany Malima, sasa aulize swali lake. Mbunge wa Mpwapwa.

Na. 235

**Ujenzi wa Daraja la Godegode - Mpwapwa**

**MHE. GEORGE N. MALIMA** aliuliza: -

Je, nini tamko la Serikali juu ya ujenzi wa Daraja la Godegode – Mpwapwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa George Natany Malima, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitangaza zabuni kwa ajili ya ujenzi wa Daraja la Godegode lililoko Wilaya ya Mpwapwa tarehe 8 Juni, 2022 na zilifunguliwa tarehe 3 Agosti, 2022 lakini hakupatikana mzabuni aliyekidhi vigezo. Hali hii ililazimu zabuni kutangazwa upya tarehe 23 Mei, 2023 na kufunguliwa tarehe 18 Julai, 2023 kwa mara ya pili. Taratibu za manunuzi zinatarajiwa kukamilika mwezi Machi, 2023.

Mheshimiwa Spika, samahani ni Machi, 2024 na mkataba wa ujenzi unatarajiwa kusainiwa mwishoni mwa mwezi Juni, 2024, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa George Natany Malima, swali la nyongeza

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, je, Serikali ina mpango gani wa dharura mfano kuwajengea daraja la muda wananchi wa Kata ya Godegode? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, Mheshimiwa Waziri, ni lini utafuatana na mimi ili ukajionee mwenyewe adha inayowapata watu wa Kata ya Godegode? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nikianza na swali la pili, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge tutaambatana na mimi kwenda kwenye hili daraja, lakini pia Mheshimiwa Mbunge anafahamu kwamba nilishafika kwenye hili daraja wakati tunafanya utangazaji wa hili daraja. Kwa hiyo, nitakwenda na Mbunge baada ya Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ujenzi wa daraja la dharura, ni kweli kwamba kuna adha kubwa sana kwenye Kata ya Godegode, lakini Bunge lako tu Tukufu lijue na wananchi kwamba daraja hili ni kati ya madaraja makubwa sana, ni zaidi ya mita 100 na ni daraja ambalo linapitisha maji mengi sana kiasi kwamba tukisema tunaweza tukajenga daraja la muda, ni lazima litaoshwa tu.

Kwa hiyo, tumeshawaagiza wenzetu wa Mkoa wa Dodoma kuwepo pale kwa ajili ya kutoa huduma hasa pale ambapo maji yanakuwa yanapungua ili kuweza kupitisha magari madogo, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, Serikali iliahidi kujenga barabara ya Kilwa kipande cha kutoka Rangi Tatu hadi Kongowe umbali wa kilometa 3.8 katika mwaka huu wa fedha... *(Makofi)*

**SPIKA:** Swali.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, tumebakiza miezi minne...

**SPIKA:** Swali.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, hatuoni dalili zozote za ujenzi; je ni lini Serikali itajenga barabara hii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli tuliahidi na tupo kwenye mpango na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hizo kilomita tatu tutazitangaza, kuzijenga kwa hizo barabara nne, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nashon Bidyanguze, swali la nyongeza.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Spika, lini Serikali itamaliza upembuzi yakinifu wa Daraja la Malagarasi Chini pale Lagala? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, Daraja la Malagarasi Chini tuko mwishoni kabisa kukamilisha upembuzi na kinachotafutwa sasa ni fedha kwa ajili ya kujenga ile barabara yote sasa ya Simo mpaka pale Malagarasi, lakini kwa maana ya usanifu tuko mwishoni kabisa na Mheshimiwa Mbunge anajua ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecil Mwambe, swali la nyongeza.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, ni zaidi ya miezi sita mkataba umesainiwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara kati ya Nachingwea na Masasi ikiwemo pamoja na Daraja la Mto Lukuledi. Ninataka kufahamu Serikali na itoe *commitment* kwa sababu barabara hiyo kwa sasa haipitiki kabisa; ni lini watajenga Daraja la Mto Lukuledi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecil Mwambe, umeuliza maswali mawili katika swali moja. Swali la msingi linahusu daraja, uliza kuhusu daraja na ondoa swali lako kuhusu barabara.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, lini Daraja la Mto Lukuledi lililoko kwenye barabara inayoelekea Nachingwea… *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa sasa unataka kuleta ushindani ama? Uliza swali linalohusu daraja.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru ni lini Daraja la Mto Lukuledi litajengwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Daraja la Lukuledi lipo kwenye barabara ambayo tulishaisaini kuanzia Masasi, Nachingwea hadi Liwale na ni kweli lipo kwenye bonde hilo daraja, lakini kwa sasa tumekuwa tunafanya matengenezo ya muda na tunavyoongea sasa hivi lile daraja linapitika lakini litajengwa wakati tunajenga barabara yote, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa sasa na wewe utazifanya Taarifa Rasmi za Bunge zisikae sawa, kwa sababu swali linalohusu barabara ni 234 hili lingine linahusu daraja. Sasa kama unataka kumjibu Mbunge kuhusu barabara yote basi nimruhusu aulize barabara, kwa sababu wewe umetoa majibu ya swali ambalo hajauliza na

mimi nakuhurumia wewe kwa sababu hapa mbele mkiulizwa maswali yasiyohusiana na la msingi majibu yakitoka hayatoshelezi, Wabunge wanalalamika, ndiyo maana nilitaka ajielekeze kwenye swali la msingi, sasa wewe umpeleka kwenye swali ambalo mimi nimemkataza, basi nimpe nafasi ya kuuliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Cecil Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, ni zaidi ya miezi sita sasa Wizara ya Ujenzi wamesaini mkataba wa ujenzi wa Barabara ya Nachingwea-Masasi hadi Liwale yenye urefu wa kilometa 172; na nimesimama hapa kuuliza kwa sababu hakuna dalili zozote ya kinachoendelea pale.

Sasa nataka kufahamu ni lini mkataba huu utaanza kutekelezwa ili kuondoa adha ya wananchi wa Nachingwea na Masasi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Wiziri, majibu. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, taratibu zipo zinaendelea na tuko kwenye hatua za mwisho ni kati ya barabara zile ambazo tulisaini barabara saba ikiwepo hii barabara aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba taratibu zinaendelea na tunategemea kuanza kuzijenga hizi barabara mwaka huu wa fedha ikiwepo na hiyo barabara aliyoitaja, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, je, ni lini Madaraja ya Nguyami na Chakwale yatakamilika kujengwa kwa ukamilifu na kuanza kutumika? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, Madaraja ya Nguyami na Chakwale tumekamilisha usanifu na yako kwenye mpango wa kutangazwa yaanze kujengwa yote, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Aysharose Mattembe, swali la nyongeza.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Spika, je ni lini Daraja la Sanza Manyoni litaanza kujengwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, Daraja la Sanza ambalo linaunganisha Mkoa wa Dodoma na Singida linasubiri *signing*, tulishapata mkandarasi tunasubiri kulisaini, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, je, ni lini Serikali itaanza Ujenzi wa Daraja la Kikafu, Barabara ya Moshi-Arusha pamoja na kulipa fidia wananchi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Maadamu umejitolea kujibu maswali yote, haya.

Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, Daraja la Kikafu liko pamoja na mradi mkubwa wa kujenga barabara hiyo aliyoitaja na wenzetu wa *JICA* tuko tunakamilisha mazungumzo kwa sababu ndiyo watakaofadhili ujenzi wa hilo daraja pamoja na barabara husika. Kwa hiyo, ipo kwenye mpango tunaendelea, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, je, ujenzi wa Madaraja ya Bujonde na Ilondo yamefikia hatua gani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, madaraja aliyoyataja Mheshimiwa Ally yapo kwenye mpango wa kuyajenga kwa sababu tunajua changamoto ambayo wananchi wanaipata na Mheshimiwa Mbunge alishaahidiwa kwamba tuna mpango wa kuyajenga hayo madaraja, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Spika, Daraja la Mto Ng'wesi ni miezi michache iliyopita lilisogezwa na maji na tunaishukuru Serikali ikaja likaliweka sawa sawa na siku tatu zilizopita maji yalikuwa yamefunika kabisa daraja kiasi kwamba magari yalikuwa yameshindwa kupita kwa siku mbili mfululizo. Sasa mashaka yangu iko siku litasombwa kabisa na kukata mawasiliano moja kwa moja; je, nini tahadhari ya Serikali ili kuzuia athari itakayotokea kubwa ya kukatika kabisa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge ndiyo daraja kubwa kati ya Barabara ya Ruvuma kwenda Mtwara, lina zaidi urefu wa mita 100 ni kweli alichokisema, tulichofanya sasa hivi tumeshamwagiza Mtendaji Mkuu wa *TANROADS* waende wakafanye *study* kama kuna haja ya kuongeza mdomo ama kulipandisha juu hilo Daraja. Mdomo kwa maana ya sehemu ambayo maji yanapita, kwa sababu ni kweli daraja kubwa, lakini yanatoka na magogo yanakuja yanaziba na lilisogezwa mbele tukawa tunapita upande mmoja, tumeishalirudisha. Kwa hiyo, tahadhari hiyo tunaichukua kwa umakini sana, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Nusrat Shabaan Hanje, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza.

Na. 236

**Uwezo wa Wakaguzi wa Ndani nchini**

**MHE. AGNESTA L. KAIZA K.n.y. MHE. NUSRAT S. HANJE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani kuwajengea uwezo wa kimamlaka Wakaguzi Wakuu wa Ndani ili kuzuia ubadhirifu na wizi wa mali za umma?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Hamad Chande, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante na kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Fedha imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuimarisha utendaji kazi wa Wakaguzi wa Ndani ikiwemo kufanya mapitio ya Sheria ya Fedha za Umma Sura Na. 348, Muundo wa Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali pamoja na Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani katika Wizara, Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi zote za Umma kwa lengo la kuongeza uhuru wa ukaguzi wa ndani katika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Waraka Na. 02 wa mwaka 2024 wa Katibu Mkuu Kiongozi kuhusu Uwajibikaji katika Kusimamia Rasilimali za Umma na Kushughulikia Hoja za Ukaguzi, umewaelekeza Maafisa Masuuli wote kuhakikisha wanawawezesha Wakaguzi wa Ndani kwa kuwapatiwa rasilimali fedha na nyenzo muhimu kulingana na mipango kazi ya vitengo walivyopitisha na Kamati za Ukaguzi. Aidha, waraka huo pia

umewataka Maafisa Masuuli kutenga fedha za ukaguzi kwa kila mradi wa maendeleo ili kuwawezesha wakaguzi wa ndani kukagua kwa ufanisi na kudhibiti vihatarishi, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, swali la nyongeza.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, moja kati ya changamoto wanazokutananazo Wakaguzi wa Ndani ni hili ambalo wao wanawakagua wale ambao ni mabosi wao jambo ambalo linapelekea ufanisi katika utendaji wao wa kazi kuwa ni mdogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu je, ni lini Serikali, itawaondoa Wakaguzi hawa wa Ndani chini ya Wakurugenzi na Serikali za Mitaa na ikibidi kuwapeleka wawe chini ya *CAG* ili kuondoa sintofahamu ambazo zimekuwa zikijitokeza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, je, ni lini Serikali itawapatia vitendea kazi vya kutosha Wakaguzi hao wa Ndani ili mwisho wa siku kazi wanazozifanya ziweze kuonekana kwamba zina tija na hivyo kuondoa ile hali ya kufungamana pamoja na hao ambao nimesema ni mabosi wao? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Agnesta, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, nimwambie kwanza ahsante kwa ushauri, lakini nataka nimwambie kwamba Wakaguzi wa Ndani wa Serikali ni sehemu ya utekelezaji wa shughuli za Serikali za kila siku. Wakaguzi wa Ndani wanakagua kabla mradi haujaanza au kazi haijaanza, wakati kazi inaendelea ili kupunguza au kuondoa kabisa changamoto zinazoweza kujitokeza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba nimwambie kwamba *CAG* ni taasisi nyingine ambayo inakagua mradi wa Serikali

baada ya kukamilika ili kubaini mapungufu yaliyopo na kuweza kutushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu kuwajengea uwezo wa kuwapatia vitendea kazi. Serikali kila mwaka inawapatia vitendea kazi vya kutosha ikiwemo magari, kompyuta na kadhalika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana. Aaah, kuna Mbunge amesimama kule.

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Spika, naitwa Ally Makoa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Eeh, leo umevaa kiaina nimeshindwa hata kujua ni nani? Nikajua mtu amehama kwenye kiti chake. *(Makofi)*

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru…

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Makoa, Mbunge wa Kondoa.

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru, Wizara ya Fedha haioni haja sasa ya Idara hii/Kitengo hiki cha Wakaguzi wa Ndani kikaondolewa pale kwa Mkurugenzi japo kikapelekwa kwa *DC* ili wawe huru zaidi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nadhani kama swali hilo linafanana na swali la kwanza la nyongeza lakini tumechukua ushauri wake, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Charles Muguta Kajege, Mbunge wa Mwibara, sasa aulize swali lake.

Na. 237

**Ujenzi wa malambo ya kunyweshea mifugo - Mwibara**

**MHE. CHARLES M. KAJEGE** aliuliza:-

Je ni lini Serikali itajenga malambo ya kunyweshea mifugo katika Jimbo la Mwibara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Charles Muguta Kajege, Mbunge wa Mwibara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua changamoto ya upatikanaji wa maji kwa ajili ya mifugo katika maeneo mbalimbali hapa nchini ikiwemo Jimbo la Mwibara, Halmashauri ya Wilaya ya Bunda.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2024/2025 Wizara itashirikiana na Halmashauri ya Wilaya kufanya tathmini ya kuainisha chanzo cha maji na kufanya usanifu katika eneo litakalopendekezwa kujengwa lambo katika Jimbo la Mwibara ili kujumuishwa kwenye mpango na bajeti ya Wizara wa mwaka wa fedha 2025/2026 kadri ya ukomo wa bajeti utakavyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada zinazofanywa na Serikali za kujenga mabwawa na kuchimba visima virefu kwa ajili ya maji ya mifugo bado mahitaji ni makubwa. Hivyo, nitoe wito kwa Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya kuwahamasisha wafugaji na wadau mbalimbali wengine kuwekeza kwenye miundombinu ya maji kwa ajili ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Charles Kajege, swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kwa kuwa wananchi wa Vijiji vya Kamlevya, Kigaga na Lagata kwa kushirikiana na mimi Mbunge wao wanachangia kuweza kujenga malambo katika vijiji vyao je, ni lini Serikali itawashika mkono ili kukamilisha ujenzi huo?

Mheshimiwa Spika, lakini la pili ni ombi, nilikuwa naomba ikiwezekana Mheshimiwa Naibu Waziri baada ya Bunge hili basi tuongozane uweze ukaone jinsi sekta ya ufugaji ilivyo muhimu katika Jimbo langu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza ni kwamba anataka kujua Serikali inawasaidiaje wananchi hawa ambao wanajitoa? Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Mwibara kwa jinsi ambavyo amekuwa akifuatilia shida na shughuli za wananchi wake katika Jimbo lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nimhakikishie kwamba namna ambavyo wananchi wanavyojitoa kuchangia miradi ya maendeleo ndivyo ambavyo wanaishawishi zaidi Serikali kuchangia katika maendeleo hayo. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba Serikali itaweka mpango wa bajeti katika kuchimba malambo katika Jimbo lake kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na tunakwenda kuchimba lambo katika Jimbo lake na nimuondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba lambo hilo tutakwenda kulichimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini baada hapo hili la pili kwamba tuko tayari kama Wizara kwenda kulitembelea Jimbo la Mwibara kuona shughuli za wafugaji zinavyoendelea, lakini pia Mwibara ni sehemu ya pembezoni mwa Kanda ya Ziwa tuko tayari kwenda pia kuhamasisha ufugaji kwa njia ya vizimba. Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Mbunge tutakapokuja huko tutafanya vyote viwili kwa pamoja kuhakikisha kwamba watu wake wanapata manufaa katika uvuvi na ufugaji pia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuena Bushiri, swali la nyongeza.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa kuwa Kata ya Ruvu Wilayani Same ina mifugo mingi sana na asilimia 90 ni wafugaji katika eneo hilo na kuna josho moja tu la kuogeshea mifugo; je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza majosho? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, tutatuma wataalamu katika Jimbo hilo kwenda kuona umuhimu wa kuweka majosho na mara tutakapoona umuhimu huo unahitajika kuweka majosho tutakwenda kuweka majosho katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Justin Nyamoga, swali la nyongeza.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itatimiza maombi yetu ya kujenga na kukarabati lambo la kunyweshea mifugo la Kijiji cha Wahambingetwa ambalo tumeliwasilisha Wizarani? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge alishaleta maombi yake Wizarani hili nakiri wazi kabisa na tayari tunakwenda kuweka kwenye mpango wa fedha wa 2024/2025 kwa ajili ya utekelezaji wa malambo yake katika Jimbo lake.

**SPIKA:** Mheshimiwa Omari Kigua, swali la nyongeza.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Spika, katika Kijiji cha Kinkwembe katika Kata ya Mkindi, Wilayani Kilindi kuna bwawa la takribani shilingi milioni 500 lakini hivi navyozungumza muda huu Mkandarasi hajaonekana na mvua ambazo zimenyesha zimesababisha uharibifu mkubwa; je, Mheshimiwa Naibu Waziri uko tayari kufanya ziara kuona namna ambavyo bwawa lile limeharibika? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, taarifa za awali kuhusiana na bwawa hili tayari tumeshazipata kwamba bwawa limepasuka na sisi tuko tayari kwenda kutembelea na kuona namna uharibifu ulivyofanyika na tuko tayari kukarabati bwawa hilo, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali, nitaleta tangazo nililonalo hapa mbele halafu tutaendelea na ratiba yetu.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza ni tangazo la wageni walioko Jukwaa la Spika; tunaye mgeni wa Mheshimiwa Antony Peter Mavunde ambaye ni Waziri wa Madini na huyu ni Alhaji Mheshimiwa Ally Jabir M. Shekimweri, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma na huyu pia ni muasisi wa mdahalo ambao unaitwa *Inter School Debate Competition on Corruption* kwa miaka mitatu sasa, nakupongeza sana kwa juhudi hizo. *(Makofi)*

Pia, hapo yupo mgeni wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ambaye ni Mbunge Mstaafu, Mheshimiwa Selemani Bungala almaarufu kama Bwege, karibu sana, karibu sana, karibu sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni mbalimbali ambao wapo hapa Bungeni wageni wenu.

Tunao wageni 35 wa Mheshimiwa Antony Mavunde, Waziri wa Madini hawa ni washindi wa shindano la mdahalo wa shule kuhusu...

Waheshimiwa Wabunge mnaozungumza nimesimama.

Tunao wageni 35 wa Mheshimiwa Antony Mavunde ambaye ni Waziri wa Madini na hawa ni washindi wa midahalo ya

shule kuhusu rushwa; kwanza, tunao Bunge Sekondari ambao ni mshindi wa kwanza, hongereni sana. *(Makofi)*

Pia tunao Maria De Mathias ambao ni mshindi wa pili, karibuni sana. Hii nadhani nayo ni shule ya sekondari imeandikwa kama jina la mtu, kwa hiyo shule ya sekondari Maria De Mathias ndio washindi wa pili. *(Makofi)*

Haya wapo Dodoma Sekondari, mshindi wa tatu, karibuni sana. *(Makofi)*

Sasa hapo ni kama nimeona hizo shule za sekondari zote ni za wasichana, hebu simameni. Ndiyo, shule za sekondari zote za wasichana ndiyo zimefanya vizuri kwenye mashindano haya ambayo yameendeshwa na Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Dodoma. Tunakushukuru sana kwa kazi hiyo pia tunawapongeza sana washindi wa mdahalo huo. *(Makofi)*

Hawa naambiwa wameambatana na Waratibu wa Shindano hilo, hawa ni Maafisa Elimu Mkoa wa Dodoma, naona hawajapata nafasi ya kuingia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba ambaye ni Waziri wa Fedha, hawa ni ndugu zake kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 26 wa Mheshimiwa Godfrey Kasekenya Msongwe ambaye ni Naibu Waziri wa Ujenzi, hawa ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamisi ambaye ni Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kutoka Zanzibar. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Mheshimiwa Hamis Mwinjuma ambaye ni Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo ambaye ni baba mdogo na Katibu Kata wa Kata ya Mtindilo, Muheza, karibu sana. *(Makofi)*

Sasa hapa huyu maana yake vyeo viwili vyote ni vya kwake kwa maana ya baba yake mdogo, lakini pia ni Katibu Kata, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Priscus Tarimo ambaye ni mdogo wake kutoka Moshi, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Florence Kyombo ambaye ni Afisa Utumishi *DUWASA* kutoka Dodoma. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhani, ambaye ni Mwenyekiti wa Kijiji cha Ikanoda. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Joseph Kakunda ambao ni ndugu zake kutoka Sikonge. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda kutoka Kilwa, Mkoa wa Lindi. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Kavejuru Felix ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma. *(Makofi)*

Tunao wageni 12 wa Mheshimiwa Boniphace Butondo ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula ambao ni wifi zake kutoka Dar es Salaam. *(Makofi)*

Tunao wageni 30 wa Mheshimiwa Fatma Toufiq ambao ni Wanawake na Samia kutoka Jijini Dodoma, ahsanteni sana na karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo na hawa ni wanafunzi 15 kutoka Jumuiya ya Kikristo Tanzania *(CCTUSF)* kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, ahsante sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watano kutoka Kampuni ya *Natural Desire* ya Jijini Dodoma wakiongozwa na Ndugu Lisa Emmanuel, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge hao ndiyo wageni tulionao Bungeni, tunaendelea na ratiba yetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Katibu ili tuendelee na hoja zilizo mbele yetu, jana kuna jambo alilieleza Mheshimiwa George Mwenisongole kama jambo la dharura ambalo angetamani Bunge litoe maamuzi na jambo ambalo linahusu waajiriwa.

Sasa niliahidi kwamba ningeenda kupitia Taarifa Rasmi za Bunge acha nisimame ili watu wawe wamenyamaza na wanisikiliza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, alisimama jana Mheshimiwa George Mwenisongole kuhusu matangazo ya kazi yanayotolewa hasa na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama na wakati mwingine vyombo vingine vya Serikali ambavyo vinakuwa na takwa la kumtaka yule mwombaji awe amepitia mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa. Mheshimiwa Mbunge alijaribu kujenga hoja yake kwamba kigezo hiki kinawandoa wengine ambao hawajapata fursa ya kwenda kwenye hayo mafunzo ya JKT kwa sababu JKT haina uwezo wa kuwapokea watoto wote na kwa sababu hiyo, kuna watoto/vijana ambao wanakosa hizo fursa kwa sababu kigezo hiko wanakuwa hawana.

Sasa jana nikashindwa kuitoa hoja kwenu kwa sababu nilitaka kujiridhisha kama Bunge hatujawahi kufanya maamuzi juu ya jambo hilo ili tusijekuwa tunafanya maamuzi juu ya maamuzi mengine kwa maana jambo hilo nilisema limeshawahi kuzungumzwa huko nyuma.

Sasa kabla sijasema maamuzi baada ya kupitia hizo Taarifa Rasmi za Bunge, siku ya tarehe 9 Novemba, 2021 Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, alikuwa anachangia Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa na Mwongozo wa kuandaa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023, akachangia kuhusu jambo hilo na alitaja hapa mifano ya Taasisi kama TAKUKURU, Polisi, *TANAPA* na *TRA* kwamba walikuwa wakiweka kigezo hiki cha mwombaji kuwa awe amehitimu mafunzo ya JKT.

Kwa hiyo, akaeleza na akatoa ushauri wake hapo kuishauri Serikali na wakati huo aliyekuwa Spika, Mheshimiwa Job Yustino Ndugai alizungumzia suala hili na kwamba kitendo hiki ni cha ubaguzi ambacho hakitakiwi kufanywa na Serikali. Kwa hiyo, haikuwa imeelekezwa Serikali ifanyeje, lakini Mheshimiwa Ndugai alieleza Serikali kwamba kitendo hiki kinaleta hiyo hoja ya ubaguzi na ninazo *Hansard* hapa. *(Makofi)*

Halafu tarehe 2 Februari, 2023 Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo akiwasilisha Taarifa ya mwaka ya Shughuli za Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu Taasisi ya Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma alitoa taarifa kuwa Kamati imebaini changamoto ya baadhi ya vijana wanaoomba kazi Serikalini kukosa kwa kigezo cha kutokuwa na cheti cha kuhitimu mafunzo ya JKT wakati siyo vijana wote wanaomaliza masomo ya kidato cha sita wanaopata fursa ya kwenda kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa. *(Makofi)*

Sasa kwenye Taarifa ile ya Kamati walitoa kama ushauri kwamba wanaishauri Serikali ione umuhimu wa kuwawezesha vijana wote wanaomaliza masomo ya kidato cha sita kuhudhuria mafunzo ya JKT, ndipo iweke kigezo hiki kwa maana ya kwamba pamoja na kuwa hii ilikuwa ni Taarifa ya Kamati kama ingeletwa kama azimio yangekuwa ni Maamuzi ya Bunge. Kwa hiyo, walileta kama ushauri, kwa hiyo, Serikali labda bado inatafakari huo ushauri. Kwa hiyo, Bunge halikufanya maamuzi yoyote kuhusu jambo hili.

Tarehe 19 Aprili, 2023 Mheshimiwa Mhandisi Ezra John Chiwelesa akichangia bajeti wa Wizara ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora alizungumzia changamoto hii ya ajira kwa kigezo cha kuwa na cheti cha kuhitimu mafunzo ya JKT wakati kiuhalisia Serikali haijaweza kuwapeleka JKT watoto wote wanaomaliza masomo yao.

Kwa hivyo, yeye pia alitoa mfano wa ajira ambazo zinatolewa na aliendа kwenye ajira za Uhamiaji na Magereza na kuomba Serikali ilitazame upya suala hili ili watoto wa Tanzania wote waweze kupata nafasi hizo bila hicho kigezo.

Tarehe 9 Februari, 2024 Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, wakati akiwasilisha Taarifa ya mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama alizungumzia kuhusu athari za uchakavu wa miundombinu kwenye Kambi za JKT, ambao umechangia mafunzo ya JKT kwa mujibu wa sheria kutolewa kwa muda mfupi na kwa vijana wachache. Pamoja na mambo mengine aliishauri Serikali iandae mkakati madhubuti wa kuboresha mafunzo ya JKT kwa kujenga, kukarabati, kuendeleza na kuimarisha miundombinu iliyopo katika Kambi za JKT, ili watoto wote wanaomaliza masomo yao waweze kujiunga na JKT. Kwa hiyo, hata hapa Kamati yetu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama haikuweka kwenye azimio imeweka kwenye ushauri wa Kamati kwa Serikali na kwa mujibu ambao Bunge ilihojiwa tarahe 9 Februari Serikali ilichukua hayo maoni ama ushauri.

Sasa kwa sababu kwa kupitia taarifa hizi kunaashiria kumekuwa na ushauri wa Wabunge, lakini kumekuwa na ushauri wa Kamati mbili za Bunge na Wabunge ambao wamechangia kuhusu hoja hii nimeshawataja hapa, maana yake Bunge halijawahi kufanya maamuzi juu ya matumizi ya kigezo hiki. Hivyo, ni halali yake Mheshimiwa Mbunge kupewa nafasi kwa ajili ya kutoa hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa George Mwenisongole sasa kwa sababu nimetoa maelezo kwa kirefu na jana ulipata nafasi ya kutoa maelezo, leo eleza kwa kifupi, toa hoja kwa Bunge, kama utaungwa mkono haya tutaendelea.

Mheshimiwa George Mwenisongole.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kumalizia hoja yangu ya jana.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyotoa maelezo yangu ya jana kuna maelfu ya wanafunzi ambao wanamaliza kidato cha nne takribani 500,000; kuna wanafunzi 200,000 wa kidato cha sita wanaomaliza, na kuna wanafunzi 1,000,000 wa darasa la saba na wote hawa wangependa kupata nafasi ya kuajiriwa katika vyombo vyetu vya ulinzi na usalama; na kwa sasa Jeshi letu la Kujenga Taifa halina uwezo wa kumchukua kila mwanafunzi

anayetaka kwenda, halina uwezo wa kumpokea kila mtu. Wanaopata nafasi ni wachache na hao wachache wanaopata nafasi ndiyo wanaopata nafasi ya kuajiriwa katika vyombo vya ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Spika, hivyo mimi naomba kutoa hoja kwamba kigezo hiki kiondolewe, lakini vilevile kwa sababu mchakato wa ajira unaendelea; Idara ya Uhamiaji mchakato unaendelea, TAKUKURU wanaendelea na Magereza wanaendelea.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa heshima ya Bunge hili mchakato huo usiamishwe. Vijana ambao hawakupata nafasi ya kuomba kuajiriwa katika hivyo vyombo wapate nafasi ya kuomba ili wapate kuajiriwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. *(Makofi)*

Baada ya hoja kuungwa mkono kwa utaratibu wetu na kwa sababu leo ni siku ya mwisho watachangia Wabunge wachache sana kwa sababu hoja imeshaeleweka.

Sasa wale wa kuunga mkono wakae, halafu wabaki wale wanaotaka kuchangia. Kwanza, niwaondoe wale ambao wamezungumza leo, umeuliza swali la msingi, la nyongeza wakae. Kwanza, wakae hao halafu nione waliobaki. *(Kicheko)*

Bado mmebaki wengi, natafuta kigezo kingine. Mheshimiwa Hawa umezungumza leo, kaa, haya wale waliozungumza jana wakae. *(Kicheko)*

Nataka wabaki watu wachache, wakae waliouliza maswali jana na kuzungumza wakae. Mheshimiwa Jacqueline Msongozi ulizungumza jana uketi, ngoja, halafu Mheshimiwa Ighondo

Ramadhani ulizungumza jana keti, ngoja kwanza, lazima nijiridhishe, Mheshimiwa Sanga alizungumza jana, kaa. *(Kicheko)*

Ngoja, haya subirini basi Waheshimiwa tupunguze matumizi ya muda, natafuta kigezo kingine.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwigulu.

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Getere keti, umepigiwa kura za hapana kwamba wewe ulishazungumza, Mheshimiwa Minza jana ulikuwa na swali kaa, subirini kwanza.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda.

**SPIKA:** Keti Mheshimiwa.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, mimi Mjumbe wa Kamati naweza kutoa uzoefu wangu.

**SPIKA:** Kaa tuu Mheshimiwa, watatoa wengine. Hawa waliosiamama watatuwakilisha. *(Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Kilumbe huyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kilumbe ulichangia jana? Niliketi mimi hapa mbele, jana hajazungumza.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Bashungwa.

**SPIKA:** Nipeni muda kwanza, jamani mnakuwa wengi waliozungumza Mkutano huu? *(Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Chaya aliongea jana, kaa. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Waliozungumza Mkutano huu? Waliochangia Mkutano huu?

Kama umechangia kaa, nibaki nao ambao hawajachangia nione ni wangapi. Waliochangia Mkutano huu?

Haya basi, naanza upya, Mheshimiwa Felista, maana naona mmekuwa wengi, ninyi wawili Mheshimiwa Ngassa hujachangia? Kaa Mheshimiwa. Mheshimiwa Kamonga hujachangia?

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, alichangia.

**SPIKA:** Kaa. Mheshimiwa Dkt. Mnzava hujachangia? Haya.

Mheshimiwa Tabasam, Mheshimiwa Sekiboko, Mheshimiwa Shangazi amechangia?

**WABUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Keti Mheshimiwa, Hapana eh? Haya, Mheshimiwa Shangazi wanasema hajachangia. Mheshimiwa Mpina umechangia, hujachangia? Ngoja. *(Kicheko)*

Haya kwa upande wa Serikali, Mheshimiwa Bashungwa Mheshimiwa Mwigulu na Mheshimiwa Sagini.

Mheshimiwa Felista Njau atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mnzava, Mheshimiwa Tabasam ajiandae.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwanza, niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Mwenisongole kwamba vijana wengi wanaachwa na kunakuwa na mgawanyiko wa usawa.

Mheshimiwa Spika, kipengele hiki kimechukuliwa na Jeshi letu na majeshi yote kwa ujumla na watu wengine wanamesha-*adopt* tena. Kwa hiyo, tayari inapunguza wigo wa vijana wetu wenye weledi na fani zao kuajirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nipo upande wa Mheshimiwa Mwenisongole kwa sababu mpaka sasa majeshi yetu hayana uwezo wa ku-*accommodate* vijana wa JKT, lakini ichukuliwe kigezo vijana waende kwenye usaili, wale watakaopita Serikali au taasisi husika ichukue jukumu la kuwapeleka kama kigezo ni hicho, kwa sababu tukiwaacha tu waka-*hang* tatizo linakuwa kubwa kwa sababu huko mtaani kuna minong’ono, lakini pia

hatuwatendei haki kwa sababu wao hawana makosa, hakuna maeneo ya kutosha ya kuwa-*accommodate* vijana hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijadili kwa kina sana na ikaona hili *gap* na tayari tulileta mapendekezo, lakini haitoshi kwa sababu wimbi linazidi kuongezeka mtaani. Pia, wataalamu wenye weledi mpana tunashindwa kuwatumia kutokana na kigezo tu hawajaenda JKT. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaomba Serikali ilichukulie kwa umuhimu wake vijana hawa wachukuliwe wafanyiwe usaili, wakienda vizuri Serikali iwachukue iwapeleke JKT, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kelele zimekuwa nyingi sana, tupunguze sauti.

Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava atafuatiwa na Mheshimiwa Hamis Mwagao Tabasam, Mheshimiwa Husna Sekiboko, ajiandae.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kuchangia hoja iliyokuwa mezani kwako kutokana na kigezo ambacho kinawekwa na vyombo vyetu vya ulinzi inapofika suala la kuajiri vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, huu ni ubaguzi, kwa sababu nchi yetu ya Tanzania tumejenga shule nyingi sana za kata, vijana wengi wanasoma na wanahitimu *form four,* vijana wengi wanasoma wanahitimu kidato cha sita, vijana wengine wanakwenda moja kwa moja mpaka chuo kikuu, lakini linapofika suala la kuwaajiri katika vyombo vyetu vya ulinzi, kigezo cha kuhudhuria mafunzo ya JKT inakuwa ni kigezo kimojawapo. Hii inawanyima fursa na haki vijana ambao hawakupata fursa ya kwenda JKT. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba vijana wanaomaliza kidato cha sita ni wachache sana ambao wanapata fursa ya kuhudhuria hiyo JKT kwa kipindi cha miezi mitatu, lakini vijana wengi hawapati hiyo fursa. Linapokuja suala la ajira kigezo kimojawapo kinakuwa ni lazima wawe wamepitia JKT,

hiki ni kitendo ambacho kinawanyima fursa watoto wetu, kinawanyima fursa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sio hivyo tu, hata suala zima la…

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba sana kitambulisho cha *NIDA…*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mnzava, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa, aah, muda umeisha naona kengele imeshagonga hapa. Kwa hiyo, muda wako umekwisha na Taarifa inabidi isije, ahsante sana.

Mheshimiwa Hamis Mwagao Tabasam, atafuatiwa na Mheshimiwa Husna Sekiboko, Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa, ajiandae.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, ni kwamba upendeleo unaofanyika wa dhahiri kwa ajili ya watu wanaochaguliwa, wanafunzi/vijana wetu wanaochaguliwa kwenda JKT sisi tunaomba Serikali irudishe mfumo uliokuwepo zamani. Hakuna njia nyingine yoyote ambayo itaweza kulifanya hili jambo liwe sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo vijana wetu kule katika Wilaya na katika majimbo, Wabunge sisi tunakuwa wahanga. Simu zinakuwa nyingi kwa nini mtoto wangu hakuchaguliwa. Sasa hili jambo linatesa wazazi…

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, unajua kila Mbunge kapewa dakika mbili, kwa hiyo, ukitoa Taarifa. Haya Mheshimiwa Sanga.

**TAARIFA**

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ninaungana na Mheshimiwa Tabasam, mfumo wa zamani wa Serikali ulikuwa kama ajira ziko 1,000 ajira 200 zinaenda kwa wale wanaotoka JKT, ajira 400 zinatoka katika kundi maalum. Zilikuwa zinaenda zinagawanywa kwa mfumo huo ili kuweka *inclusive* kwenye upatikanaji wa ajira za Serikali.

Kwa hiyo, hicho anachokizungumza Mheshimiwa Tabasam, mfumo wa zamani wa Serikali ulikuwa unafanya kazi vizuri zaidi kuliko mfumo huu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tabasam, unaipokea Taarifa hiyo?

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, amenilia muda wangu, Taarifa siipokei.

Mheshimiwa Spika, umenipa dakika mbili, ni kwamba tunao wanafunzi ambao wamemaliza kidato cha sita, wanafunzi wamemaliza kidato cha nne, wamekaa pale wanasubiri kwenda makambini. Tunachoiomba Serikali itenge bajeti kubwa turudishe mfumo wa zamani kupeleka vijana wote waliomaliza kidato cha sita waende JKT.

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Husna Sekiboko, atafuatiwa na Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa, Mheshimiwa Shangazi ajiandae.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naona mambo mawili katika hoja hii, jambo la kwanza ni haki ya kila kijana wa Tanzania kuajiriwa, lakini jambo la pili ni namna na taratibu zinazotumika na vyombo vingine vya usalama, ukiacha jeshi katika kutekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika nchi ambayo bado hatujawa na uwezo wa kuwapeleka vijana wote kwenye Jeshi la Kujenga Taifa, tunatenda dhambi kuwabagua na kuwaajiri wengine kwa kutumia kigezo cha kupita kwenye Jeshi la Kujenga Taifa kwa sababu wapo vijana wengi wanatamani kuingia Jeshi la Kujenga

Taifa, lakini hawakuwahi kupata hiyo fursa ya kupita. Kwa hiyo, ukisema aajiriwe aliyepita JKT maana yake kwanza, alikosa nafasi ya kuingia JKT, lakini pili, unamnyima tena nafasi ya kuajiriwa. Hii ni dhambi, Bunge lako lisikubali kupita kwenye dhambi ya namna hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, vyombo vyetu vya ulinzi na usalama, ukiondoa Jeshi la Wananchi au majeshi, kwa mfano polisi; polisi ni *diplomatic unit,* wao wanapaswa kwenda kufanya masuala ya upelelezi, masuala ya kidiplomasia, masuala ya kupeleleza uhalifu wa nchi.

*Mheshimiwa Spika, unapopeleka wanajeshi waliofundishwa kupiga, kuuwa na kufanya vitu vya namna hiyo kwenye taasisi ambazo kazi yake parse sio hizo za mauaji na vitu vya namna hiyo, ndio sababu tunapata malalamiko mengi ya wananchi wanateswa wakati wa upelelezi, wananchi wanafanyiwa mambo mabaya huko kwenye vikosi vingine kama maeneo ya TANAPA, na kadhalika kwa sababu kuna sehemu tumekosea. Tumepeleka wanajeshi pure kwenye taasisi ambazo hazihitaji utaalamu wa kijeshi.* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Spika, nashukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Eeh, kidogo hapo mwisho naona nimepata changamoto na mchango wako. Umesema maeneo wanayochukua wanajeshi watu wana…

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, tunapeleka TAKUKURU vijana waliopita JKT, tunapeleka Polisi vijana waliopita JKT ili aajiriwe Polisi kigezo mojawapo ndio hicho apite JKT. Tunapeleka magereza na maeneo mengine mengi, lakini mafunzo ambayo kijana wa JKT anapewa ni ya kupigana na mtutu, ni ya kupigana na adui. Shughuli anazokwenda kuzifanya polisi sio *parse* za kupigana, matokeo yake tunakuta malalamishi…

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, yapo malalamiko maeneo mengi wakati wanahojiwa, wakati wanafanyiwa upelelezi, wananchi wamepigwa, wameteswa, wamefanyiwa *interrogation* kiasi ambacho hata wengine wamepoteza na maisha.

**SPIKA:** Sawa, sasa kwenye hii sehemu ya mwisho kwa muktadha wa mchango wetu hapa, lakini ili Taarifa zetu Rasmi za Bunge zikae sawa, itakuwa si sawa kwamba kwa kuwa hawa wamepitia haya mafunzo ndio maana kuna hizo changamoto. Changamoto zile nafikiri ni binafsi yule anayefanya anakuwa na changamoto zake na ndio maana na wao wanaendelea kufanya marekebisho mbalimbali inapotokea changamoto kama hiyo.

Kwa hiyo, isichukuliwe kwamba, hawa wanaochukuliwa ndio wenye changamoto kwa sababu kule jeshini, wamo Wabunge humu ambao wamepitia huko JKT, hatujaona wakileta changamoto.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, sehemu ya mchango ya hawa na zile changamoto tutaiondoa, ili Taarifa zetu Rasmi za Bunge zikae sawa, lakini pia nimetoa hayo maelezo ya ziada kwamba wale wanaofanya hizo changamoto kwenye hayo majeshi yetu ama kwenye vyombo vyetu vya ulinzi na usalama ni changamoto binafsi kuliko kuwa za kundi ambalo limepitia JKT.

Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Rashid Shangazi, Mheshimiwa Omar Omar, ajiandae.

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa JKT wanakwenda kujifunza ukakamavu, uzalendo, uraia na mengineyo, na kutokana na dhana ya vijana wengi kwamba wanabaguliwa kutokana na nafasi hizi kwa sababu hawajapitia JKT, mimi ushauri wangu kwa Serikali, sisi kama Bunge tuishauri Serikali kwanza wachaguliwe, isiwe kwa kigezo cha kwamba lazima awe ametoka JKT. Baada ya kuchaguliwa ndio wapelekwe JKT wote ili kusudi watimize vigezo vya kuchaguliwa katika ajira husika.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hata kipindi cha nyuma tunakumbuka walikuwa wakichaguliwa kwanza, wanapochaguliwa ndio wanapelekwa kwenye mafunzo ya JKT, ili kwenda kwenye ajira na hata kama wanakuwa wamekwenda JKT baada ya kuwa wametoka shuleni ni kwamba bado wanakuwa hawajajiweka kiakili kwamba wanakwenda kufanya kazi ya Jeshi la Polisi au majeshi mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ombi langu ni kwamba Serikali sasa ikubali kwamba waajiriwe kwanza vijana halafu wapelekwe kwenye mafunzo ya JKT ili na wao waweze kupata ajira, nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Shangazi, atafuatiwa na Mheshimiwa Omar Omar, Mheshimiwa Mpina ajiandae.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi na kwanza naanza kwa kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mwenisongole.

Mheshimiwa Spika, jambo hili ni baya sana kwa sababu kwanza linakiuka Katiba, Ibara ya 22(2), kiko wazi kwamba hapa kuna ubaguzi.

Mheshimiwa Spika, lakini Serikali ya Awamu ya Kwanza na ya Pili ya nchi yetu zilikuwa na mapato ambayo si makubwa sana, lakini bado katika awamu hizi waliweza kupeleka vijana wote waliomaliza kidato cha sita kwenda mafunzo ya JKT kwa mujibu wa sheria, na ilikuwa ni lazima vijana wote waende na tumeona wakienda kujifunza uzalendo, ukakamavu na kila kitu na ndio ambao waliobahatika kupata mafunzo hayo wametufikisha mahali pazuri katika Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nina ombi, kwa kuwa tatizo kubwa la JKT ni fedha kwamba hawapati fedha za kutosha, basi wangeangalia kuratibu haya mafunzo badala ya miezi mitatu ya sasa, wayapunguze hata kwa mwezi mmoja ili vijana wote waweze kwenda kama tatizo ni gharama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini la pili ni Wizara ya Fedha sasa kuona uwezekano wa kuweza kutoa fedha za kutosha kwa ajili ya JKT ili vijana wote wanaomaliza kidato cha sita waende wakapate mafunzo haya muhimu ambayo yanasaidia pia kutambua na kuelewa uzalendo wa Taifa lao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Omar Omar, atafuatiwa na Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mheshimiwa Patrobass Katambi ajiandae.

**MHE. OMAR ALI OMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na mimi kwanza naunga mkono hoja hii tuliyonayo hapa mezani, na sababu zangu kwa kweli, kwanza tunatengeneza ubaguzi na ubaguzi huu upo katika nchi yetu yote ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, tukiangalia JKU na JKT kwa sababu Zanzibar tuna JKU, wenzetu huku Tanzania Bara tuna JKT. Kwa hiyo, hili ni moja katika jambo ambalo vijana wetu wengi tunawakosesha fursa muhimu za kufanya kazi zao ambazo ni muhimu kwao.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, ni kwamba vijana wengi tunawapunguzia umri. Umri wao unapofika kuajiriwa, kama tunavyojua kwamba Jeshi la Polisi lina vigezo maalum, Jeshi la Magereza na majeshi yetu yote yana vigezo maalum vya umri, kwa hiyo, kipengele cha umri ni kipengele ambacho tunawanyima fursa. Kijana anakwenda ana umri wa miaka 25 sasa leo unampeleka siku zote anaomba nafasi hapati JKU hapati JKT, matokeo yake mpaka anafika miaka 35, kweli Jeshi la Polisi lina uwezo wa kumuajiri kijana mwenye miaka 35? Haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi naunga mkono hoja hii. Kwa kweli tuhakikishe kwamba, kipengele hiki tumekifuta kabisa na uzalendo utumike, ili vijana wetu waendelee kupata ajira katika nchi yetu, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, atafuatiwa na Mheshimiwa Patrobass Katambi, Mheshimiwa Jumanne Sagini ajiandae.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa natambua tatizo kubwa la ajira nchini, lakini hoja ya mtoa hoja ya kuondoa kigezo cha JKT kwa vijana wetu wanaochaguliwa kwenye haya majeshi yetu, moja, je, hapa tunataka kutibu nini?

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hivi vijana wenyewe wa JKT waliopo ambao wameshajitolea muda mrefu ni wengi, ukiniuliza mimi jimboni kwangu wako zaidi hata ya 200; kwa hiyo, hata ukisema na wengine waingie, tunataka kwamba hawa watapata hizo nafasi?

Mheshimiwa Spika, nafasi zinazotolewa sasa hivi hata wale wa JKT hata asilimia tano yenyewe haifiki. Kwa hiyo, ina maana kwamba sisi kama watunga sera hili suala tutafute namna nyingine ya kutafuta ajira ya vijana wetu, lakini hii bado haiwezi kutusaidia hata tukifanya haya maamuzi leo.

Mheshimiwa Spika, leo waniambie Waheshimiwa Wabunge zilipopatikana nafasi za Uhamiaji mlipata ngapi kwenye majimbo yenu? Zilipopatikana za Polisi walipata wangapi? Kwa hiyo, hata ukisema vijana wengine waongezeke bado hii haiwezi ikatibu tatizo tulilonalo, lakini je, hii inatuwezesha kuwa na jeshi imara?

Mheshimiwa Spika, kama vyombo vya dola viko *comfortable* kwamba vinapomchukua kijana ambaye walau ana mafunzo ya awali ya kijeshi, vinatengeneza askari wazuri, tatizo letu sisi ni nini? Je, haya maamuzi haya yatatusaidia kutengeneza jeshi?

Mheshimiwa Spika, lakini lingine ni kwamba *message* tunayoipeleka sasa vijana wengine wameshajitolea miaka mitatu kwenye kambi za jeshi, halafu tukachukue mwingine wa kawaida inatusaidia?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele imeshagonga Mheshimiwa, ahsante sana.

Mheshimiwa Patrobass Katambi, atafuatiwa na Mheshimiwa Jumanne Sagini, Mheshimiwa Innocent Bashungwa ajiandae.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa fursa hii.

Mheshimiwa Spika, mimi ninataka tu kuchangia kwenye eneo moja kwa sababu aligusia Ibara ya 21(2) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mimi niongeze Ibara ya 12 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inatoa usawa kwa wananchi wote au kwa binadamu.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huu wa usawa katika taratibu kuna *equity* na *equality.* Sasa kwenye misingi ya utoaji wa ajira huwa kuna masharti, sifa na vigezo na katika masharti sifa na vigezo ambavyo vimeainishwa kwa mujibu wa sheria mbalimbali Katiba hii imeruhusu pia sheria nyingine zilizotungwa kwa mujibu wa Katiba kutengeneza utaratibu wa kutoa fursa na nafasi kwa Watanzania kulingana na sifa, hali, lakini pia mahitaji na vigezo.

Mheshimiwa Spika, moja ya eneo ni kwenye vyombo vya ulinzi na usalama katika Ibara 117, na hapa inatoa ruksa kwamba katika vyombo vilivyoundwa na kwa mahitaji yao wanayo haki ya kuweza kutengeneza taratibu, bila kuvunja sheria, kuweka sifa, masharti na vigezo ili katika kurahisisha utekelezaji wa majukumu.

Mheshimiwa Spika, sasa katika sifa hizi ambazo zimeelezwa, kwanza vimetolewa vigezo au sifa za waombaji, lakini katika sharti hilo kuna masharti ya lazima na yasiyo ya lazima; na sifa iliyotolewa hapo ni moja ya sifa kama ya ziada kwa maana ya *added advantage* kwa mtu ambaye atakuwa amepitia kwenye vyombo vya ulinzi na usalama katika ngazi hiyo. Kwa hiyo, halikuwekwa kama sharti la lazima.

Mheshimiwa Spika, lakini pili, katika …

**SPIKA:** Ngoja, ngoja. Mheshimiwa George Mwenisongole mpelekee matangazo Mheshimiwa, yale ya kazi halafu nitakupa nafasi baadae kidogo ya kuchangia. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Jumanne Sagini.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, nimalizie.

**SPIKA:** Ngoja akuletee yale matangazo, nitakupa nafasi ya kuchangia ukishamaliza kuyapitia. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Jumanne Sagini. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika na Bunge lalo Tukufu, tunapokea hizi *concern* za msingi kabisa za Waheshimiwa Wabunge kuhusu nafasi za ajira kutaja kigezo cha kupita JKT kama moja ya masharti ya kujiunga na vyombo hivi, lakini kama nilivyoeleza jana kwa ufupi, msingi wa msimamo huu yalikuwa ni masuala mawili muhimu kabisa kuliko yote ni imani ya uzalendo, lakini la pili ilikuwa ni kwamba tunapelekwa kwenye vyombo vya ulinzi na usalama, lazima tujiridhishe na mwenendo wao.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine ni kwamba, hata hizi nafasi zinazotolewa si nyingi kiasi hicho kwamba ukifungulia ndio tutapata ufanisi mkubwa wa ajira. Kwa mfano, mwaka huu hizi nafasi zilizotangazwa za upande wa *Immigration* ni watu 400 tu. Upande wa *Fire* ni nafasi 200, upande wa Magereza nafasi 500 na polisi ni nafasi 1,500. Sasa hata kama ungesema wawe Watanzania wote, bila shaka si wote wangeweza kupata hizi ajira, lakini tunaheshimu mawazo yenu.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nikueleze tu kwamba katika Taarifa ya Haki Jinai ambayo tunaendelea kuifanyia kazi, eneo hilo pia tumeelekezwa tulitazame kwa madhumuni ya kuboresha mfumo wa ajira wa vyombo hivi kama ilivyoelezwa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge. Kwa vile, taarifa hii ina maeneo mengi ya kufanyiwa kazi tulikuwa tunaomba maelekezo yako yaende sambamba na kutekeleza ushauri uliotolewa na Tume ya Haki

Jinai ili kwa pamoja tuwe tumekamilisha jambo hili kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya nikushukuru kwa nafasi hii uliyonipa, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Mheshimiwa Katambi uko tayari au niendelee kwa mwingine?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** *(Hapa hakutumia kipaza sauti).*

**SPIKA:** Niendelee kwa mwingine?

Haya Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba, tutamalizia na Mheshimiwa Katambi, mtoa hoja ajiandae.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Upande wa Serikali, maelekezo yatakayotolewa na Bunge tuko tayari kuyafanyia kazi, lakini nilipenda niseme mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza, sisi upande wa Serikali tukisaidiwa na Bunge lako tusiji-*confine* kwenye tatizo la ajira la vijana wetu nchini na kuitizama JKT kama muarobaini wa kumaliza changamoto hii.

Mheshimiwa Spika, Bunge linayo nafasi ya kusaidia upande wa Serikali wa kuangalia ni namna gani tutaongeza wigo wa kuzalisha ajira kwa vijana nchini ili tuweze kutengeneza fursa nyingi kwa vijana wetu, kwa sababu kwa upande wa kwa mfano Jeshi la Wananchi Tanzania pamoja na vyombo vya ulinzi na usalama wanavyo vigezo maalum vya kutafuta vijana ambao wanahitajika kwenda kufanya kazi kwenye vyombo vyetu vya ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Spika, nikijitolea mfano mimi mwenyewe, nikijiweka kwenye vigezo yaani kwa kuzaliwa mimi sikuwahi ku-*qualify* kujiunga na Jeshi la Wananchi Tanzania, kwa sababu watu wenye *flat feet* mimi nina miguu inaitwa *flat feet,* si-*qualify* kwenda jeshini kwa sababu ukisimama kwenye gwaride muda mrefu watu wenye *flat feet* kama mimi huwezi ukahimili kusimama muda mrefu, lakini pia ukitembea umbali mrefu watu wenye *flat feet* kama mimi unaweza ukapata changamoto usifike.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele imeshagongwa Mheshimiwa.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kigezo kama hicho pamoja na vingine, vyombo vya ulinzi na usalama wana vigezo maalumu ambavyo siyo kila Mtanzania anaweza ku-*qualify* kwenda kule.

Kwa hiyo, mimi nataka nikuombe pamoja na Waheshimiwa Wabunge, tupokee changamoto ya upungufu ya ajira nchini kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, Bunge pamoja na Serikali tutafakari namna ya kuongeza *scope* ya kupata ajira nyingi kwa vijana wetu, lakini tusiji-*confine* kwa JKT peke yake *silver bullet* ya kumaliza changamoto hii, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na nampongeza mtoa hoja kwa kuleta hoja hii ambayo inaongelea maoni na masuala yanayowagusa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, moja, hatubishani na hoja kwa sababu jambo linalosemwa lina ukweli ndani yake kwamba kuna watoto wanakosa fursa hiyo kwa sababu walikosa fursa ya kwenda JKT.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hoja hii tayari ipo inafanyiwa kazi kupitia maoni yaliyotolewa na Tume ile iliyoundwa na

Mheshimiwa Rais na itafanyia kazi na baadae litakwenda kwenye vyombo, vishirikishwe vyombo kwenye Kamati Kuu ile ya masuala ya usalama na baadae mwongozo utatoka wa namna nzuri ya kuweza kutekeleza mambo haya, naliomba Bunge lako Tukufu likubali Serikali tupokee jambo hili, liunganishwe kwenye maoni yaliyotolewa na Tume ya Haki Jinai, yafanyiwe kazi kwa pamoja ili jibu litakapotoka litoke likiwa linajumuisha maoni yote ya wadau, yakihusisha na haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *spirit* ile ile ya taasisi muhimu za nchi hii kuheshimiana, Bunge linaheshimiana na Mahakama, Bunge linaheshimiana na Serikali, lakini vyombo vya ulinzi na usalama ni moja ya taasisi nyingine katika nchi ambayo tunaiheshimu. Namuomba Mheshimiwa Mbunge aridhie kwamba Serikali tumepokea jambo hili, litapelekwa kwenye vyombo, litapelekwa kwenye Kamati, litajadiliwa na litatolewa uamuzi ili kuweza kuleta utaratibu ambao utakuwa na manufaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, si tu kwa ajili ya kuajiri lakini katika manufaa ya kujenga vyombo ambavyo vina nguvu ya kuweza kufanya kazi kwa maslahi mapana ya Taifa. Masuala ya *security* ni masuala *sensitive*, hata tu kuyajadili kwamba mwongozo wetu wa kuajiri utakuwa huu, si kitu sawasawa. Kwa hiyo, tulichukue lakini nadhani litafanyiwa kazi ili kuweza kuhakikisha kwamba vyombo vyetu vya ulinzi vinazingatia mambo yote kwa masilahi mapana ya Taifa, kuliko kutoa maelekezo kwamba mchakato usimame, yataanza kuingia na masuala ya kihabari habari ama masuala ya namna yoyote yenye chumvi ambayo yanaweza yakaleta makwazo kwenye vyombo vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naliomba Bunge na mtoa hoja kwamba hoja ni ya msingi, imepokelewa, iunganishwe na hoja iliyotolewa na Kamati ya Haki Jinai, halafu ifanyiwe kwa pamoja. La sasa hivi ambalo lilishaendelea, liendelee likamilike lakini hili si la mwisho, litatolewa mwongozo ambao utasaidia katika muda mwingine uliosalia. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Mheshimiwa Patrobass Katambi, mtoa hoja ajiandae.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, nimepitia barua zote za mamlaka ambazo zimetoa, ikiwepo barua ya Uhamiaji, lakini pia barua ya Jeshi la Magereza na andiko la TAKUKURU. Zote hizi zimeainisha sifa mbalimbali, mojawapo ikiwa hiyo ya kupita kwenye vyombo vya ulinzi na usalama. Kuna moja ndiyo inaonesha kama ni sharti lakini hizi nyingine zimeonesha kuwa kama ni kama sifa ya ziada au ya nyongeza kwa mwombaji ambaye atakuwa ameomba.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa msingi huo …

**SPIKA:** Hebu hao waliosema ya nyongeza, maana tusijekuwa tunajadili hoja hapa kumbe haipo. Waliosema ni sifa ya nyongeza ni nani na nani kwenye hayo matangazo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, haijatoa maelezo, lakini *from the* … *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia katika maelezo ukiangalia kuna moja imesema sifa za mwombaji na nyingine tofauti imesema masharti ya jumla ya mwombaji. Sasa hizi ni lugha tofauti hasa katika *context* ya kutafsiri; pia kwenye barua nyingine amesema sifa ya mwombaji.

Sasa kwa lugha hizi zilizotumika tunarudi kwenye msingi ule ule kwamba kwa sababu ni mamlaka zimetoa barua hizi na ni za Serikali na jambo hili ni moja ya jambo ambalo liko kwenye mjadala wa Tume ya Haki Jinai na tatu ni kwa sababu vyombo hivi vina mamlaka yake ya Kikatiba kwa mujibu wa Ibara ya 117 na kwamba sheria nyingine zimetungwa kwa ajili ya kurahisisha mchakato, nirudi pale pale kama walivyosema Waheshimiwa Mawaziri wenzangu kwamba tulirudishe kwa upande wa Serikali, tulichukue kwa ajili ya kulifanyia kazi na baada ya hapo tuweze kuendelea na utaratibu huo, lakini tukiwa tumezingatia zaidi mwongozo wa Bunge lako Tukufu kwamba ni jambo la kulichukulia *serious concern,* ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mtoa hoja, hitimisha hoja yako.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuhitimisha hoja yangu.

Kwanza nianze kwa kuwashukuru Wabunge wenzangu ambao wameunga mkono hii hoja, kwa kweli nawashukuru sana kwa kuliona hili tatizo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imesema tuipe muda kuhusu mapendekezo yaliyotolewa na Tume Jinai, lakini mimi hapa nina taarifa ya Tume Jinai na naomba niinukuu; "Tume imependekeza, suala la kupitia mafunzo ya JKT na JKU kwa kujitolea lisiwe kigezo cha msingi cha kujiunga na Jeshi la Polisi na la Magereza." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hata Tume yenyewe iliyoundwa na Rais imesema hiki kitu kisiwe kigezo cha msingi cha kuajiriwa. Sasa sielewi hoja ya Serikali inaposema tuungane na hii Tume wakati Tume yenyewe inakataa hiki kigezo, hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, hata Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ...

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja ikiwa inahitimishwa huwa haina taarifa na ndiyo maana Waziri akisimama hapa mbele huwa hatumpi taarifa.

Hata hivyo, kwa sababu tunaelekea kufanya maamuzi, labda Mheshimiwa anayo taarifa itakayolisaidia Bunge kufanya maamuzi, Mheshimiwa Patrobass. *(Makofi)*

Kaa Mheshimiwa Mwenisongole, labda anayo taarifa itakayotusaidia kama Bunge.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, hili ni jambo muhimu na ni *sensitive*, tunakubaliana kabisa na hoja na hizi zinazoelezwa ni *valid* kwa sababu lengo ni kutanua nafasi na fursa kwa ajili ya vijana wa Kitanzania kuweza kupata bila kuwa na masharti yanayowabana. Kama alivyoeleza vizuri, Tume ya Haki Jinai imetoa mapendekezo, bado yako kwenye hatua za mchakato maana yake mapendekezo yanaenda sasa kwenye hatua za kwenda kufanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndicho hiki ambacho tumekisema kwenye Bunge lako Tukufu kwamba tulichukue upande wa Serikali ili michakato katika upande wa Serikali itimie kwa maana ya ile taarifa ya mwisho kufanyiwa kuwa *digested* ya Tume ya Haki Jinai, lakini pili maangalizo haya yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge ili mwisho wa siku Serikali ikija inakuja na *position* moja, kuliko kufanya maamuzi wakati Tume imepeleka mapendekezo, lakini pia Bunge liwe limeshafanya maamuzi. Kwa hiyo, ilikuwa ndiyo ...

**SPIKA:** Taarifa ya ziada unayompa ni ipi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, taarifa niliyoitoa ni kwamba alichokisema yeye mwenyewe amesema ana nakala ya Taarifa ya Tume ya Haki Jinai, ikiwa ni mapendekezo. Sasa mapendekezo maana yake hayajafikia mwisho kwenye kufanyiwa maamuzi ambayo yanaenda sasa kwa Mheshimiwa Rais kwa ajili ya hatua ambazo zita...

Mheshimiwa Spika, sasa maamuzi ya mwisho yatakuwa ni upande wa Serikali, ikiwa mojawapo ni *concern* hii ambayo imeletwa kwenye Bunge lako Tukufu.

**SPIKA:** Mheshimiwa George Mwenisongole, malizia hoja yako. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kumalizia hoja yangu.

Mheshimiwa Spika, licha ya Tume ya Haki Jinai kupendekeza hiki kigezo kisiwe cha msingi katika kuajiriwa, hata Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 22(2) inasema wazi kabisa kwamba, kitendo chochote cha kubagua hakiendi hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nihitimishe kwa kusema haya; kwa sababu mchakato wa ajira katika Idara ya Uhamiaji, Jeshi letu la Magereza na TAKUKURU, bado haujafika mbali, ...

**SPIKA:** Mwanasheria Mkuu wa Serikali naona umesimama hoja ikiwa inahitimishwa, anaenda kinyume na sheria ama? *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba asome kwa ukamilifu hilo pendekezo la Tume ya Haki Jinai ili isaidie uamuzi. Asome kwa ukamilifu kipengele anachokisoma.

**SPIKA:** Wewe uko nayo hapo Mheshimiwa?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Tusomee wewe kwa ukamilifu, maana yeye amesoma nusu. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, haya, naomba nisome, inapatikana kwenye ukurasa wa 27; “Taasisi za Haki Jinai ziajiri wataalamu…” *No, no, no, sorry*. *(Makofi)*

“Suala la kupitia mafunzo ya JKT na JKU kwa kujitolea lisiwe kigezo cha msingi cha kujiunga na Jeshi la Polisi na Jeshi la Magereza, hasa katika ajira za utaalamu kama vile udaktari na uhandisi, isipokuwa kigezo hicho kinaweza kuwa kigezo cha ziada.” *(Makofi)*

**SPIKA:** Kinaweza kuwa kigezo cha ziada.

Mheshimiwa Mwenisongole malizia hoja yako. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa ruhusa yako naomba nimkumbushe tu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwenye taarifa hiyo hiyo ya Haki Jinai, kifungu namba 14 inasema; "Utaratibu wa kuajiri askari wa Jeshi la Magereza na Jeshi la Polisi kwa kigezo cha kupitia Jeshi la Kujenga Taifa na Jeshi la Kujenga Uchumi kwa kujitolea, umelalamikiwa na wadau kuwa umechangia baadhi ya vijana wenye sifa za kujiunga na Jeshi la Polisi na Jeshi la Magereza kukosa nafasi." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo, Tume imependekeza kwamba hicho kigezo kisiwe cha msingi, ukweli unabaki kuwa ukweli Mwanasheria Mkuu, hili suala ni suala la kibaguzi, ifike hatua sasa Bunge letu lifanye maamuzi kwa manufaa ya vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba kwa sababu mchakato wa ajira uliotangazwa na Uhamiaji, Jeshi la Magereza na TAKUKURU bado haujafika mbali, naomba mchakato huo utangazwe upya ili vijana waliomaliza kidato cha nne na cha sita ambao hawajapata nafasi ambao hawajapata nafasi ya kuajiriwa kutokana na hicho kigezo, waruhusiwe kuomba kuajiriwa tena, wapate nafasi ya kuomba kuajiriwa na hilo jeshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ngoja ngoja.

Waheshimiwa Wabunge, unajua hizi kanuni pamoja na kwamba tunakaribia mwisho wa maisha ya Bunge hili, bado tunajifunza.

Waheshimiwa Wabunge, utaratibu aliousema hapo Mheshimiwa Mbunge wetu anapaswa kuleta azimio. Sasa hapo mwisho ndiyo amelisema, anataka Bunge liazimie nini.

Mheshimiwa Mbunge, kama ambavyo niliongoza jana ndiyo hivyo hivyo, lazima tuongozane kwa mujibu wa kanuni zetu. Bunge kufanya maamuzi kuhusu hoja hii, likielekeza kuhusu hizi ajira ambazo tayari ziko kwenye mchakato, itakuwa ni kama kutunga sheria ambayo inaenda nyuma. Kwa hiyo, tukifanya maamuzi leo ni kwa ajili ya yale yanayokuja, siyo kwa ajili ya haya ambayo tayari yametangazwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ili hoja yetu iende vizuri na Bunge liweze kuwa limefanya maamuzi, sasa nataka nimpe picha vizuri ili azimio letu liwe na sura ambayo tunafuata taratibu tulizojiwekea wenyewe. Bunge lilishawahi kutoa ushauri huko nyuma, kwanza, kwa Wabunge kadhaa ambao waliwahi kuchangia na michango ya Wabunge inapotolewa, Serikali ikisimama inasema imechukua hayo mawazo yaliyotolewa na Bunge.

Kwa hiyo, kuanzia mwaka 2021 jambo hili limekuwa likizungumziwa; Novemba 2021 limezungumza na Mbunge, Februari, 2022 limezungumzwa na Kamati kama ushauri kwa Serikali, Aprili, 2023 limezungumzwa na Mbunge kama ushauri kwa Serikali, tarehe 9 Februari, 2024 hili limezungumzwa siyo kuhusu ajira, lakini kuhusu vijana kwamba wote waende JKT, yaani mazingira yawekwe vizuri kule kwa maana ya majengo yaongezeke na vitu kama hivyo ili vijana wote waende.

Sasa ili maamuzi yetu yawe yamekaa vizuri kwa kuzingatia ushauri ambao tumeshautoa huko nyuma na hatukufanya maamuzi, ndiyo maana ni ngumu kuifuatilia Serikali kwamba mmefikia wapi. Sasa pamoja na kwamba Tume ya Haki Jinai inaendelea na kazi yake, kazi ya Haki Jinai siyo shughuli ya Mahakama, ni shughuli ya Kiserikali na ndiyo maana Mheshimiwa Rais ndiye aliyeunda ile Tume. Kufanya kazi kwa ile Tume hakulizuii Bunge kufanya kazi yake. *(Makofi)*

Sasa Mheshimiwa Mbunge nakuongoza kwa maana ya kwamba ulete sasa azimio la kufanya maamuzi hapa, hatuwezi kufanya maamuzi kama Bunge juu ya ajira ambazo tayari zimeshatangazwa, itakuwa ni kufanya maamuzi ambayo yanarudi nyuma. Tunaweza kufanya maamuzi yanayorudi nyuma katika mazingira fulani, lakini kwa muda wetu wa leo siwezi sasa

kutoa mhadhara mrefu kwamba tunaweza kutengeneza sheria za namna hiyo, lakini kwenye hili inaweza kutupa ugumu kidogo kurejea nyuma, kwamba waache huu mchakato, isipokuwa kwa michakato inayokuja tunaweza sasa kufanya maamuzi kama Bunge halafu hayo maamuzi yataenda huko sasa yakaambatane wakati Serikali inajaribu kulifanyia kazi hilo azimio, watakuwa sasa wanatazama Tume imesema nini na wao wanajipanga vipi, muktadha ni huo. Kwa sababu Bunge haliwezi kufanya maamuzi leo kwamba Serikali ipeleke watu wote JKT; kwa nini, kwa sababu inategemea uwezo wa kifedha na uwezeshaji wa jeshi ambalo linaendesha mafunzo hayo, hayo maamuzi pia hatuwezi kuyafanya.

Waheshimiwa Wabunge, tunayoweza kufanya ni yale ambayo hayatamuathiri mwananchi ambaye hajapata kwenda kule, kwa sababu jeshi halina uwezo wa kupokea watu wote. Sasa azimio lako linatakiwa kuwa la jumla kwa sura hiyo kwamba huko mbele Serikali ikiondoe kigezo hiki ama iweke kama cha ziada kwa pale ambapo wanaona kuna umuhimu.

Waheshimiwa Wabunge, kwa nini, pamoja na umuhimu wa michango iliyotolewa na Serikali, kipindi fulani kulikuwa hakuna mafunzo ya JKT, taasisi hizi zilikuwa bado zinaajiri na zilikuwa zikishaajiri ndiyo zinapeleka watu JKT. Kwa hiyo, Bunge likifanya maamuzi kwenye hilo, hakuna mahali ambapo Serikali mtasema kuna kugongana mahali, hakuna kugongana. Kama Serikali iliweza kufanya hizo ajira kipindi ambacho hatukuwa tunaenda jeshini, sasa hivi inayo uweza wa kuajiri na wale ukishawaajiri ndiyo uwapeleke kule jeshini wakapate hayo mafunzo unayoyahitaji. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa kwa haya maelezo sasa tuletee azimio lako, kama kuna mahali litakuwa limepelea mimi nitakujazia, halafu tutafanya maamuzi kama Bunge. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi, naomba Bunge lako Tukufu liazimie kwamba kigezo hiki cha kuwataka vijana wanaotaka nafasi kwenye vyombo vyetu vya ulinzi na usalama wawe na kigezo cha kupitia JKT kiondolewe. *(Makofi)*

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani mmeielewa hoja?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**SPIKA:** Mmeelewa hoja? Msije mkaanza mbona tena, hapana. Kwa maelezo haya nikishawahoji kwa upande wa Serikali, hatutatarajia matangazo ya ajira kwenye ajira hizi na zingine, ziwe na hicho kigezo. Kwa nini, kwa sababu hatuna uwezo wa kupeleka watu wote.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kwa mwongozo huo ulioutoa, namwomba Mheshimiwa Mbunge arekebishe, isiwe kiondolewe bali kisiwe cha lazima, yaani isiwe kigezo cha lazima.

Mheshimiwa Spika, kwa ninavyoelewa hiki Kiswahili kwamba kikiondolewa maana yake kwenye vigezo vyote kisiwe kinaonekana, haitakuwa sawa. Badala yake aweke neno kigezo cha vijana kupitia JKT kisiwe kigezo cha lazima. Inaweza ikawa sifa ya nyongeza ama inaweza isiwepo, lakini tusiweke kwenye sharti kwamba hiki kisiwepo.

**SPIKA:** Tukisema kisiwe cha lazima halafu kikawekwa kwamba ni cha ziada, maana yake wataangalia hawa wote halafu watamtafuta mwenye nacho. *(Makofi)*

Hapana, kwenye hili tunataka tu twende vizuri, hata tukisema kisiwe cha lazima, wao wanajua. Nadhani yale maelezo yaliyotumiwa na Tume ya Haki Jinai, yale ya kusema kwenye hizi kazi fulani, kwenye kazi fulani. Sasa sisi kwa sababu tunaweka

azimio kwa muktadha wa ajira hizi ambazo zimetangazwa, hizo zingine za kutaka mtu lazima anaenda kupigana sijui yuko *frontline*, wewe unamjua nani ukamuweke.

Sisi kipindi chetu, ngoja nieleze vizuri sana, sisi kipindi tumemaliza chuo wapo watu wameenda kuajiriwa Uhamiaji, walipita JKT lini na mimi nimesoma nao? Hawajapita huko maana yake uwezo wa kuajiriwa wanao, wale unaotaka lazima wapite wewe wachukue wapeleke, kuna shida gani hapo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, mimi nakuelewa vizuri kabisa na naliomba Bunge lako Tukufu kwa heshima zote itakuwa ni makosa sana Bunge hili kuweka sheria inayokataza mtu aliyepita JKT kuajiriwa, yaani kwamba kwenye, aah, tusikilizane ndiyo maana kuna hoja mezani. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, tusikilizane ndiyo maana tunahoja ipo mezani, naombeni tusikilizane ndiyo maana na mimi nawasikiliza.

Mheshimiwa Spika, ipo hivi utaratibu mzuri ni kuweka kisiwe kigezo cha lazima, tutakuwa tumeshakidhi kwamba wakitaka ambaye ameenda JKT wapate, wakitaka ambaye hajaenda JKT wapate. Sheria inapaswa kuwa wazi namna hiyo, lakini tukiweka ki-*clause* tutakuwa tunaenda kwenye *extreme* nyingine... *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ni kwa muktadha upi wanakuwa wamekataliwa ambaye amepita JKT?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ninaosemea ni pale tutakaposema kwenye matangazo yoyote kigezo cha JKT kisiwepo, kiondolewe.

**SPIKA:** Wewe ungependa kiwepo kwenye yapi ili tutenganishe kwenye azimio letu?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, mimi ningependa vile walivyoweka Tume ya Haki Jinai kwamba kwenye maeneo ambayo yanahitaji utaalam siyo lazima mtu awe vile kigezo si lazima kuwepo, lakini kwenye maeneo ambayo yanahitaji mtu

ambaye ameenda JKT tusiwabane vyombo kutumia hivyo na ameiongea vizuri Mheshimiwa Mpina pale, tusiwabane…*(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, humu ndani kuna mwanajeshi?

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, wapo.

**SPIKA:** Ngoja yupo yupo, kaa Mheshimiwa Mwigulu. Mwanajeshi unapoanza mafunzo kule jeshini, si unaanza kama yale ya JKT taratibu?

**WABUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Haya tusaidie mwanajeshi ndiyo tuelewane vizuri ama ukiwa tu…

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, hiki kigezo ambacho vyombo vya ulinzi vinaweka kina sababu zake nyingi sana huko ndani; moja, naomba muwe watulivu sasa mimi ndiyo mwanajeshi mwenyewe niliyoombwa kutoa ufafanuzi. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Haya jamani.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, mimi ndiyo mwanajeshi ambaye nimeombwa na Bunge…

**SPIKA:** Haya haya twende twende.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naomba niwaeleze suala…

**SPIKA:** Twende tu taratibu tutafika mahali pazuri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, twende taratibu mtaelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kigezo kile kuwekwa kwenye vyombo, maana yake kuna eneo ambalo litakuwa limepunguza ule urasimu wa ukaguzi wa wale vijana kwenda kujiunga na vile vyombo, kwa sababu tayari walishapita kwenye chombo ambacho kimeaminiwa na vyombo vile kama sehemu ya familia ile. Kwa mfano alitoa mzungumzaji ambaye ni Waziri wa Ulinzi mstaafu pale kwamba ukiwa na mguu *flat* kwa kule jeshini…*(Makofi)*

**SPIKA:** Sasa hayo jamani, hayo tutakuwa tunarefusha mjadala, miguu *flat, no flat* huyo ni mwanajeshi…

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Miguu *flat* ana shida gani kwenye Uhamiaji, mbona *flat* wapo kibao huko na tunawaona kila siku? *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naomba tulekebishe vizuri lugha yetu, vyombo ambavyo Bunge lako Tukufu…

**SPIKA:** Usiende kwenye *flat* kwa sababu kule sidhani kama anayeenda JKT sawa, yaani mnataka kuweka mazingira fulani hivi yaani kwamba hivi vyombo vimetengwa kwa ajili ya waenda JKT, je, huyo ambaye hakwenda? Hivyo vyombo havina wanasheria huko Mheshimiwa? *(Makofi)*

Ngoja, havina wanasheria, hebu tusaidiane vizuri havina?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kidogo tu nisikilize, Bunge lako…

**SPIKA:** Ngoja kwanza, ili twende na wewe vizuri na mimi nilitaka kwenda Jeshi niliishia njiani.

Mheshimiwa tusaidie wewe ulienda Jeshi ukiwa na miaka mingapi? Samahani, ulikuwa na miaka mingapi ulipoenda Jeshi? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, mwaka 1985 ndiyo nimejiunga na Jeshi la Kujenga Taifa.

**SPIKA:** Ulisoma ukiwa Jeshini, yaani umesomeshwa ukiwa umeshaenda Jeshini. Wapo waliosoma ambao wameenda jeshini baada ya kusoma.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ni sahihi kabisa.

**SPIKA:** Unawajua? Wale walienda JKT saa ngapi?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ninachotaka kwanza ni tafsiri vizuri na Waheshimiwa Wabunge muelewe...

**SPIKA:** Tafsiri kwa muktadha wa ajira, usitafsiri kwa muktadha kwamba kila mtu atakuwa mwanajeshi. Mwanajeshi inajulikana kabisa ndiyo maana nimekusimamisha, lakini siyo kila aliyeenda JKT atakuwa mwanajeshi, ajira hizi zingine hazihitaji hicho. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, nataka nifafanue kidogo...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, subiri kidogo, Waheshimiwa nataka nitafsiri kidogo...

**SPIKA:** Haya tumsikilize mwanajeshi baada ya huo ufafanuzi niliyotoa, tusikilizane endelea Mheshimiwa nakusikiliza.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, hebu nisikilizeni kidogo.

Mheshimiwa Spika, tangu nimefika hapa Bunge lako Tukufu limebadili sheria mbalimbali kuchukua vyombo kadhaa kuvibadili

kuwa kwenye sura ya Jeshi, mojawapo ni Uhamiaji, mojawapo ni Jeshi ambalo linasimamia Maliasili, mojawapo ni Magereza kuliongezea nguvu kuwa Jeshi kamili. *I mean* Bunge hili hili ndiyo limepitisha hiyo sheria, kwa hiyo, wale siyo raia, wale ni wanajeshi kutokana na majukumu wanayokwenda kuyafanya ya kimkakati yanayolenga usalama wa nchi. Kwa hiyo, ninaomba msije mkapoteza sifa ya majeshi haya kwa maana ya ile sheria ambayo imetungwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninachoweza kusema ni kwamba ibaki kama sifa ya ziada ili vyombo viweze kutumia nafasi hiyo kwenye kupata watu waliyo sahihi, sifa ya ziada.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, taarifa, taarifa na uzoefu.

**SPIKA:** Wanasheria tusikilizane na Wabunge tusikilizane. Mheshimiwa Kilumbe.

**TAARIFA**

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, hoja hapa iliyokuwa inaweza ikatusaidia kutoka hapo ni kwamba mtu akiwa ametoka JKT anataka kuajiriwa Jeshini ni kipi ambacho Jeshi kitasema madhali huyu alikwishatoka JKT basi anakwenda moja kwa moja, hakuna. Zoezi la kumuingiza mtu katika Jeshi hata kama alipita JKT linaanza hatua moja mpaka nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naunga mkono hoja ya kwamba kigezo hiki kiondolewe. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwigulu, umeshaongea mara nyingi sana sina hakika unataka kutupeleka…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Sasa sijajua taarifa anapewa nani? Mheshimiwa Mwigulu, mara yako ya mwisho kuzungumza tunafanya maamuzi sasa. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, najua sisi ni wawakilishi wa wananchi na mara zote tunapoona vijana wamekosa nafasi inaleta hisia, inaleta muamko, lakini mimi ningeomba hili jambo tunaloongelea ni la vyombo vya ulinzi na usalama, tusifanye kabisa kwa hisia. Mimi naendelea tu kusisitiza hivyo… *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa nisaidie jambo moja kuna shida gani aliyeajiriwa na TAKUKURU kupelekwa JKT, kuna changamoto yoyote hapo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, mimi nakubaliana raia kabisa aliyeajiriwa na TAKUKURU kupelekwa JKT, ninachopinga ni kuondoa kabisa kabisa kigezo kile…

**SPIKA:** Hayo maneno ya kuondoa kabisa kabisa ni nani ameyaweka Mheshimiwa?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, azimio linasema kigezo hicho kiondolewe.

**SPIKA:** Bunge limeshahojiwa au mimi nimeanza kuongea kwa sababu zipi Mheshimiwa?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kama utatuongoza kigezo hicho kiendelee kuwepo kama sharti la ziada tunakubaliana nacho.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza niseme wazi nadhani watu mnaweza kuwa hamjapata picha ya changamoto ya hii hoja.

Waheshimiwa Wabunge, mjadala umeshakuwa mrefu lazima tufanye maamuzi, haya matabu niko nayo hapa mbele ni

ya taarifa za humu ndani zinazohusu hoja hii. Serikali ilishasikia hoja hii tangu mwaka 2021, 2022, 2023, 2024 ni muda ambao Serikali kama ingetaka, kwa sababu Kamati ya Bunge ya wakati huo ilikuwa imeungana na Utawala na TAMISEMI ilishasema, ilitoa ushauri kwa Serikali. Kamati nyingine imekuja imeuweka ule ushauri kwa sura nyingine haijaenda kwenye ajira imesema Serikali itazame namna ya kuweka wigo mpana ili kila anayetaka kwenda JKT aende ama siyo kila anayetaka, lakini alazimike kwenda ili baadae kigezo hiki kinapomkuta Serikali iwe tayari ilishampa fursa. *(Makofi)*

Sasa uwezo wa Serikali kuwapa fursa vijana wote wanaomaliza kidato cha nne na cha sita kwenda JKT haupo. Kwa kuwa uwezo huo haupo sasa, wanaokwenda huko ni *a selected few,* hawa wanaobaki ambao na wao wangetamani kwenda JKT wanakosa nafasi kwanza ya kwenda JKT, ya pili wanakosa nafasi ya ajira kwa kuwa walikosa nafasi ya kwenda JKT. *(Makofi)*

Sasa wewe unawekaje mazingira ya huyu mtu kupata kitu kinaitwa *double jeopardy*, wakati siyo yeye amesababisha? Yeye angependa kwenda kwa sababu hiyo ushauri Bunge lilishatoa kwa hiyo miaka mitatu mfululizo na mwaka huu imetoa tena nadhani ni ushauri ambao hata sisi tunaelewa Serikali haina uwezo wa kujenga miundombinu yote sasa hivi ya kuwapata vijana wote. Mpaka hilo litakapokamilika ndipo ambapo tutaweza kuweka utekelezaji huu wa haya ambayo ni ya muhimu sana mlivyoyazungumza Serikali, ni ya muhimu kwa kweli, lakini ukimnyima huyu kijana fursa mara mbili umemuonea. *(Makofi)*

Sasa nimetumia neno umemuonea na sijatumia neno ubaguzi, kwa nini? Ni kwa sababu nafahamu neno ubaguzi ni zito linaenda na mambo mengi, ndio yale ambayo upande wa Serikali mengine mlikuwa mnaeleza kwamba hivi ni vigezo ambavyo ni vya kawaida kwa upande wa vyombo vya ulinzi na usalama. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hoja ya ubaguzi haipo lakini hoja ya uonevu ipo, hoja ya ubaguzi haipo lakini ipo hoja ya uonevu. Kipindi hiki ambacho Serikali inajipanga kwanza kwa ajili ya kuanza kupeleka vijana wote JKT; cha pili inajipanga na mipango mizuri kabisa na

Bunge linaendelea kushauri namna ya kupanua hizi fursa za ajira kipindi hiki Serikali haiwezi kutumia kigezo hicho. *(Makofi)*

Sasa hata ukitaka kutumia maneno ya kwamba hiki kitakuwa cha ziada tuviache vile vyombo kwa sababu huo uziada ndiyo maana huwa mtu unapoomba kazi unapeleka vyeti vyote ulivyonavyo, vingine wataangalia ufaulu wako darasani, vingine hawataangalia ufaulu wataangalia tabia. Hivyo ndiyo hivyo vya ziada vyote huwa haviandikwi, sasa sisi tukiweka mazingira kwamba kitaandikwa lakini kitakuwa ni cha ziada maana yake tayari umemnyima huyu ambaye hakwenda huko. *(Makofi)*

Kwa hiyo, yale mengine tuachane nayo yaende na hizo *flat shoes*, yaende na nini na *flat* sijui nini, *flat feet* sijui *foot* ama urefu, ufupi hayo yote yalishazungumzwa humu ndani. Hayo mkaendelee nayo kwa utaratibu wenu, lakini kwa zile ajira ambazo zimeletwa kama hoja hapa ndani kumnyima huyu mtoto fursa kwa sababu hajapita JKT anakuwa ameonewa. *(Makofi)*

Sasa kwa sababu imeletwa kama hoja na Serikali ilishashauriwa na Serikali imetueleza hapa kwamba inaendelea na utaratibu wa kufanyia kazi maoni ya Tume ya Haki Jinai, sasa basi kwa sababu Mheshimiwa Mbunge maneno aliyotumia imeonekana kama Serikali inaona dah, sasa hapa tunaazimia jambo gani? Maazimio yakishaazimiwa na Bunge, Serikali mnapoenda kuyafanyia kazi si huwa tunaletewa taarifa hapa ndani.

Kwa hiyo, inawapa ninyi nafasi ya kwenda kusema Bunge limeamua hivi, Haki Jinai imesema hivi, tuyachakate haya tunafikia mwisho upi? Kwa hiyo, hakuna hoja ya kuwa na wasiwasi kwenye jambo hili. Kwanza zile ajira zilizotangazwa zinaondoka kwenye hii hoja, kwa hiyo zile zinaendelea na utaratibu, lakini ajira zinazofuata zisimuonee Mtanzania yeyote. *(Makofi)*

Kwa hiyo kipindi hiki ambacho Serikali inajipanga, Azimio la Bunge ambalo nitaenda kuwahoji muda si mrefu; kipindi ambacho Serikali inajipanga kwa ajili ya kuhakikisha wale vijana wote waostahili kwenda JKT wanakwenda, kigezo hiki cha kijana

kupita JKT kama kigezo cha yeye kuajiriwa huko, huyu kijana aajiriwe, halafu apelekwe huko JKT inatoa uwanja mpana na inatoa haki kwa kila kijana kushiriki katika mchakato wa ajira kwa sababu hata ajira hawatapa wote, hao watakaopata wenye vigezo wapewe nafasi. Kwa hiyo, muktadha huo nadhani umeeleweka vizuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo nadhani tumeelewana ili tusije kuwa, sasa kwa sababu na mimi mwenyewe sijaandika hapa mbele…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, isomeke na JKU; JKT na JKU.

**SPIKA:** Aaah! Isomeke JKT na JKU?

Ni kweli, lakini sasa JKU kwa sababu hapo itabidi nianze kupitia vifungu vya Katiba hapa ili tusije tukawa tumefanya jambo ambalo kidogo ndivyo sivyo, Bunge lisije likawa limefanya maamuzi ambayo yanapaswa kuamuliwa na Baraza la Wawakilishi, sitaki kuweka hayo mazingira. Naona nataka kusaidiwa lugha na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huu uliyoeleza na kwa kuzingatia matangazo yaliyotolewa na vyombo vyetu vya usalama na kwa sababu vyombo hivi hasa vinavyohusu Mambo ya Ndani ukiondoa Magereza vinagusa pande mbili za Muungano huwa mara nyingi tukisema tunasema JKT au JKU. Kwa hiyo, aliyosema nadhani yupo sahihi kwa maana ya ajira kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sasa kwa sababu hili azimio litakuwa la jumla na Magereza umesema, Polisi ndio?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi ni la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenda mpaka upande wa pili wa Muungano.

**SPIKA:** Uhamiaji?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, *Immigration* kadhalika inakwenda mpaka upande wa pili wa Muungano.

**SPIKA:** Magereza?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, Magereza kule ni Chuo cha Mafunzo huku ni Jeshi la Magereza, *Fire* ni ya upande mmoja kila mmoja ana utaratibu wake. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Sawa, mimi nafikiri kwa sababu tunataka kuliweka la jumla kwa kweli na wengine watajikuta humo ama pengine tusitaje neno JKT, tutaje neno gani? Tuseme mafunzo, kwa hiyo JKU iingie?

**WABUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Haya maana sitaki kulipeleka Bunge kufanya maamuzi ambayo tusije tukawa tunapoka madaraka ya mahali kwingine.

Waheshimiwa Wabunge, sawa, kwa hiyo maneno yawekwe vizuri. Hapa nakumbushwa jamani, ajira siyo suala la Muungano, lakini ajira kwenye vyombo, nadhani kuna... Mheshimiwa Waziri, ajira kwenye vyombo si ni suala la Muungano? Ajira kama ajira siyo suala la Muungano, lakini ajira kwenye vyombo si ni suala la Muungano? Si huwa ajira kule wanaajiriwa wote wa pande mbili? Hebu tusaidiane Mheshimiwa.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ajira kwenye vyombo vinavyogusa Muungano ni vile viwili kama nilivyovitaja, vyombo vipo, *sorry* vitatu kwa maana ya Jeshi la Wananchi, Jeshi la Polisi, Uhamiaji; Magereza na *Fire* siyo sehemu ya ajira za Muungano, nashukuru.

**SPIKA:** Haya, waheshimiwa wabunge kigezo cha kupitia mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa na Jeshi la Kujenga Uchumi

kisiwe kigezo, aah, kisiwe kigezo nini Kiswahili? Kisiwe kigezo cha lazima, cha msingi?

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, kisiwe kigezo.

**SPIKA:** Kisiwe kigezo?

Waheshimiwa Wabunge, jamani haya nadhani muktadha umeeleweka kwa sababu nilikuwa sijaandika hapa kwa hiyo ningewasomea, lakini maneno yale ambayo yalikuwa yanaleta ukakasi hayatakuwepo na nafikiri ili jambo liwe limeenda vizuri wasaidizi watanisaidia kuiweka vizuri halafu nitawasomea namna inavyosomeka, lakini kwa maana ya hoja wacha niwahoji ili tuifunge halafu baadae nitawasomea kitasomeka namna gani.

Waheshimiwa Wabunge, sasa ntawahoji hoja ya Mheshimiwa George Mwenisongole, baada ya haya marekebisho na hilo azimio.

Nani huyo ameweka *microphone?* Haya hairuhusiwi kusema kwenye *microphone*.

Mmoja, haya. Walioafiki wameshinda, aliyesema siyo ni mmoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Ahsante Sana. Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaendelea.

Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* - KATIBU MEZANI.**

## HOJA YA KAMATI

### Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninamwita sasa Mwenyekiti wa Kamati Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, aje awasilishe hoja ya Kamati. *(Makofi)*

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha Taarifa ya mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2023 hadi Januari, 2024, lengo ikiwa nikukidhi masharti ya Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya taarifa; utaratibu wa Bunge kuitumia Kamati hii katika udhibiti wa utekelezaji wa madaraka ya kutunga sheria ndogo unahitaji desturi ya Kamati kuripoti kwa Bunge lenyewe. Hivyo taarifa hii inazingatia desturi hiyo na madhumuni yake ni kulijulisha Bunge hali halisi.

Mheshimiwa Spika, muundo wa taarifa; Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti kuhusu muundo wa taarifa inayowasilishwa Bungeni. Kwa madhumuni ya kuonesha uzingatiaji wa masharti hayo, naomba kubainisha muundo wa taarifa hii ambayo imegawanyika katika sehemu kuu tatu: -

(i) Sehemu ya Kwanza, ni utangulizi ambao unajumuisha maelezo ya jumla ili kujenga misingi ya taarifa;

(ii) Sehemu ya Pili, inahusu ufafanuzi wa shughuli kwa kipindi cha Februari, 2023 hadi Januari, 2024; na

(iii) Sehemu ya Tatu, inafanya majumuisho ya maoni ambayo chimbuko lake ni shughuli zilizotekelezwa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba taarifa yote na viambatanisho vyake viingie kwenye *Hansard* kama ilivyowekwa mezani mapema leo asubuhi.

Mheshimiwa Spika, msingi wa shughuli za Kamati; shughuli za Kamati hii zinatokana na masharti yaliyofafanuliwa katika misingi mitatu; kwanza, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo imeweka mgawanyo wa madaraka ya msingi wa uendeshaji wa Bunge; pili, Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 inayodhatiti kanuni za msingi kuhusu maana, ufafanuzi, uandishi, matumizi na mambo mengine kuhusu misingi ya sheria za nchi zikiwemo sheria ndogo; na tatu, Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 ambazo zinaweka utaratibu wa uendeshaji wa Bunge na Kamati zake ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Spika, shughuli zilizotekelezwa; shughuli za Kamati kwa kipindi cha mwaka Februari, 2023 hadi Januari, 2024 zinagusa uelewa na uzoefu wa Wajumbe pamoja na utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Ufafanuzi wa shughuli hizo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mafunzo kwa Wajumbe; mara baada ya Wabunge kupangwa upya kwenye Kamati za Kudumu za Bunge, shughuli ya kwanza ilikuwa ni kupata mafunzo kutokana na asili ya majukumu ya Kamati. Kanuni za Bunge zimeitaja Kamati hii katika kundi la Kamati za Sekta Mtambuka na zimeipa jukumu lenye upekee. Kwa mantiki hiyo, mafunzo hayo muhimu yalilenga kuwazoeza Wajumbe mazingira mapya ya kazi yao ya kipekee. Aidha, mafunzo yaliwatambulisha Wajumbe kwenye majukumu, mchakato, vigezo vya kazi, misingi na desturi za shughuli za Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, ninafurahi kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba mambo hayo yalisaidia ushiriki mzuri wa Wajumbe katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo, katika misingi wa utekelezaji bora wa madaraka Bunge upo wajibu wa kufuatilia

utekelezaji wa maazimio hayo kwa niaba ya wananchi. Kwa desturi za Kibunge, Kamati za Bunge ni nyenzo muhimu ya kuliwezesha Bunge kupata picha halisi ya utekelezaji uliofanyika. Ninaomba kutoa taarifa kuhusu utekelezaji wa maazimio ya Bunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni utekelezaji wa maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo ambazo matokeo yake yaliripotiwa Bungeni; kwa kuwa Bunge ndilo lenye dhamana ya kuweka sheria za nchi zinazowezesha ustawi wananchi, Kamati ilifuatilia utekelezaji wa maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo yaliyolenga kuweka sawa masharti ya sheria nchini. Kamati ilipokea taarifa za utekelezaji wa maazimio ya Bunge yaliyolenga kuondoa dosari katika jumla ya sheria ndogo 31. Sheria ndogo hizo ni zile zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa. Matokeo ya uchambuzi yaliripotiwa Bungeni wakati wa Mkutano wa Kumi na Mbili.

Mheshimiwa Spika, pili, utekelezaji wa maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Kumi na Moja; uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa maazimio uliangalia hatua mbalimbali zilizofikiwa katika utekelezaji wa maazimio hayo. Ninaomba kufafanua hatua zilizofikiwa pamoja na kubainisha Wizara zilizohusika katika utekelezaji wa maazimio ya Bunge. Lengo la ufafanuzi huu ni kuliwezesha Bunge kubaini hatua za utekelezaji wa maazimio yake na kufanya maamuzi sahihi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kubainisha Wizara nne zilizohusika na utekelezaji wa maazimio ya Bunge kama ifuatavyo:-

Kwanza, Wizara ya Katiba na Sheria iliyokuwa na sheria ndogo mbili zilizobainika kuwa na dosari kumi na moja; pili, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari iliyokuwa na sheria ndogo moja iliyobainika kuwa na dosari tatu; tatu, Wizara Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi iliyokuwa na sheria ndogo moja iliyobainika kuwa na dosari sita; na nne, Wizara ya Maliasili na Utalii iliyokuwa na sheria ndogo moja yenye dosari sita.

Mheshimiwa Spika, hatua zilizofikiwa na Wizara zilizotajwa katika utekelezaji wa maazimio ya Bunge zimeoneshwa katika kiambatanisho namba. Pamoja na jedwali hilo, ninaomba kufafanua hatua hizo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hatua ya rasimu ya marekebisho katika ngazi ya Wizara; uchambuzi ulibainisha kwamba Wizara moja ipo katika hatua za ndani za kukamilisha mchakato wa kufanya marekebisho ya sheria ndogo moja. Hatua hii inahusu rasimu ya marekebisho kuandaliwa na kuwekwa katika ngazi ya Wizara. Kwa msingi huo Wizara hii iliyofikia hatua hii haijatatua dosari kama ilivyoelekezwa na Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua ya rasimu ya marekebisho kuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa uhakiki; hatua ya rasimu ya marekebisho iliyowasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakiki ni hatua muhimu ya kushughulikia maazimio ya Bunge kwa lengo la kuondoa dosari iliyobainika. Uchambuzi wa taarifa za utekelezaji ulibainisha kuwepo kwa utekelezaji wa maazimio ya Bunge kuhusu dosari 20 katika sheria ndogo tano. Utekelezaji huo ulifika hatua ya rasimu ya marekebisho kuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa sheria ndogo; Kifungu cha 38(1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kimeweka sharti kuwa sheria ndogo zote zinatangawa kwenye Gazeti la Serikali ziwasilishwe Bungeni. Uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Kumi na Mbili na Mkutano wa Kumi na Tatu umefanyika kwa lengo la kufanikishwa wajibu wa Bunge kudhibiti mamlaka yake na kutunga sheria nchini. Kwa desturi za uendeshaji wa Bunge letu, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo imekuwa karakana ya Bunge ambapo wajibu wa udhibiti wa sheria ndogo huanza kutekelezwa. Dhima kuu ya Kamati wakati wa uchambuzi ni kubainisha dosari na baadae kulishauri Bunge kuhusu hatua stahiki za kuchukua.

Naomba kubainisha dosari zilizobainika kwa uchambuzi wa jumla wa sheria ndogo 22 kama ifuatavyo:-

(a) Dosari ya kuwa na masharti yanayokinzana na masharti ya Katiba; Katiba ya nchi ndiyo sheria kuu na inapaswa kuzingatiwa na sheria zote za nchi. Sheria ndogo inayofafanua Sheria ya Bunge haitarajiwi kukinzana na masharti ya Katiba. Uchambuzi umeonesha kuwa zipo sheria ndogo ambazo zimebainika kuwa na masharti yanayokizana na Katiba.

Mheshimiwa Spika, mfano wa sheria ndogo hizo ni Kanuni za Utoaji wa Leseni za Biashara za mwaka 2023 zilizo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara *(BRELA).* Kanuni ya 16 ya Kanuni hizo inaweka katazo la uwakilishi wa Wakili pale ambapo mamlaka imeruhusu mrufani kufika mbele yake kwa ajili ya kusikiliza shauri la rufaa.

Mheshimiwa Spika, masharti yanayowekwa na kanuni hii ni kinyume na masharti ya Ibara ya 13(6)(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Ibara hiyo inaelekeza kuwa wakati haki na wajibu wa mtu yeyote vinahitaji kufanyiwa uamuzi wa Mahakama au chombo kingine chochote kinachohusika, basi mtu huyo pamoja na haki nyingine atakuwa na haki ya kupewa fursa kusikilizwa kwa ukamilifu. Miongoni mwa misingi ya haki ya kusikilizwa kikamilifu ni fursa ya kuwakilishwa Kisheria. Hivyo, katazo linalowekwa na Kanuni ya 16 ya kanuni hizo linakiuka msingi muhimu wa haki ya kusikilizwa kikamilifu, jambo linalokinzana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(b) Dosari ya kuwa na masharti yanayokinzana na sheria mama na sheria nyingine za nchi; Sheria ya Tafsiri ya Sheria ilitungwa na Bunge kwa lengo la kuweka misingi ya uandishi, tafsiri, matumizi na mambo mbalimbali mengine muhimu kuhusu sheria za nchi. Kifungu cha 36(1) cha sheria hiyo, kimeweka masharti yanayozitaka sheria ndogo kutokuwa kinyume na masharti ya sheria mama na sheria nyingine za nchi. Ili kujiridhisha na masharti hayo Kamati ilitaka kujua mambo manne yafuatayo:-

(i) Iwapo sheria ndogo zinaendana na malengo ya sheria inayotekelezwa;

(ii) Iwapo ukubwa wa adhabu hauzidi kiwango cha ukomo wa adhabu ulioruhusiwa na sheria mama;

(iii) Iwapo taratibu zinazowekwa na sheria ndogo hazikiuki taratibu zinazotakiwa na sheria inayotekelezwa; na

(iv) Iwapo lugha iliyotumika katika sheria ndogo haipotoshi madhumuni ya sheria mama.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi umeonesha kuwa baadhi ya sheria ndogo zina dosari ya kuwa masharti yanayokinzana na sheria mama, mfano wa dosari hiyo umejitokeza katika, Kanuni za Ukusanyaji na Uchakataji wa Taarifa Binafsi, 2023. Kanuni hizo ambazo zimetungwa chini ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (Na. 11 ya 2022) zina masharti yanayokinzana na sheria mama. Dosari hiyo, inajitokeza katika kanuni ya 11 ambayo inaipa Tume nguvu ya kumruhusu mtu yeyote kupekua na kupakua taarifa yoyote ilioingizwa katika rejista.

Mheshimiwa Spika, ruhusa inayotolewa na Tume kwa mtu yoyote kupekua na kupakua taarifa binafsi inakinzana na azma ya ulinzi wa taarifa binafsi. Mkinzano huo umetokana na kumruhusu mtu yeyote kuzifikia taarifa binafsi ilhali nia ya sheria mama ni ulinzi wa taarifa binafsi. Masharti hayo ya kanuni ya 11, hayaendani na lengo kuu la sheria mama la kuimarisha ulinzi wa taarifa binafsi.

Mheshimiwa Spika, dosari ya kuweka masharti yasiyo na uhalisia; pamoja na masuala mengine lengo la uandishi wa sheria ni kuweka masharti mbalimbali ambayo matokeo ya utekelezaji ni kushughulikia, kufanikisha na kutatua jambo fulani. Uchambuzi umebainisha kuwa masharti yaliyowekwa na sheria ndogo ambayo utekelezaji wake hauna uhalisia, dosari hiyo imebainika Kanuni za *The Tanzania Shipping Agencies (Cargo Security and Safety of Terminal Operations) Regulations, 2023.*

Mheshimiwa Spika, kanuni inaelekeza kuwepo kwa vali zuizi *(block valve)* katika maeneo ya kushushia na kuhifadhia shehena.

Vali hizo zitafunguliwa pale ambapo janga la dharura limetokea. Hata hivyo, kanuni ya 23(4) inaelekeza kuwa vali hizo zinapaswa kuwa wazi muda wote. Sharti hilo halina uhalisi katika utekelezaji, kwa kuwa vali hizo haziwezi kuwa wazi muda wote isipokuwa tu, pale ambapo zitahitajika kutumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, dosari ya kutoendana na misingi ya uandishi wa sheria, madhumuni ya misingi ya uandishi wa sheria ni kuwezesha sheria za nchi kufanikisha lengo lililokusudiwa na sheria inayohusika. Aidha, uzingatiaji wa misingi hiyo ni kuwezesha sheria kueleweka kwa urahisi miongoni mwa watu au wananchi wanaoguswa na wanaosimamia au wenye jukumu la kuzitafsiri. Ili kujiridhisha Kamati ilitaka na mambo yafuatayo: -

(i) Iwapo sheria inayotoa mamlaka ya kuwa na sheria ndogo inayohusika imerejewa inavyostahili; na

(ii) Iwapo mamlaka iliyoweka sheria ndogo inayohusika imebainishwa.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi umeonesha kuwepo kwa dosari ya sheria ndogo kutozingatia masharti ya uandishi, mfano wa sheria ndogo zenye dosari hiyo ni Kanuni za Shughuli za Uzalishaji, Upelekaji na Usambazaji Umeme, 2023, chini ya Sheria ya Umeme, Sura 131.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi umebainisha dosari ya makosa ya uandishi katika kanuni ya 35 inayohusu notisi ya kuingilia huduma. Kanuni hii imeweka muda wa vipindi viwili tofauti vya utoaji wa notisi, ambapo muda wa kwanza, uliotajwa na kanuni ni muda wa saa 24 na muda wa pili, ni wa siku saba. Uandishi huu ambao unaonesha muda tofauti kuhusu utekelezaji wa jambo moja unasababisha mkanganyiko mkubwa.

Mheshimiwa Spika, dosari za uandishi wa majedwali; kwa mujibu wa Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Jedwali ni sehemu ya sheria hivyo inastahili kuwa na misingi inayofanikisha lengo la sheria. Kwa kuzingatia hilo Kamati ilitaka kujiridhisha na mambo yafuatayo: -

(i) Iwapo kuna kifungu wezeshi cha Jedwali inalohusika;

(ii) Iwapo kifungu wezeshi cha Jedwali hilo kimerejewa na kuoneshwa kwenye Jedwali hilo; na

(iii) Iwapo Jedwali linatoa ufafanuzi uliokamilika.

Mheshimiwa Spika, kwa kawaida majedwali *(schedules)* katika sheria yoyote ni sehemu ya sheria na lengo lake ni kutoa ufafanuzi wa ziada. Madhumini yake ni kuwezesha utekelezaji kutimiza malengo ya vifungu vya sheria vinavyohusika. Kwa msingi, huo ikiwa kuna dosari yoyote ya jedwali upo uwezekano wa kutokukamilika kwa malengo ya vifungu vinavyohusiana na jedwali, hivyo kukwamisha azma iliyokusudiwa na sheria inayayohusika.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi umeonesha kuwa zipo sheria ndogo zenye dosari katika uandishi wa majedwali. Mfano wa Sheria Ndogo hizo ni *The Plant Health Regulations, 2023*. Uchambuzi umeonesha makosa katika kanuni ya 95(1) na kanuni ya 97(2). Kanuni hizo zinarejea jedwali la 51 pamoja na jedwali la 57, majedwali ambayo yanarejewa hayapo katika kanuni hizo. Hali hiyo inasababisha masharti ya kanuni zinazohusika kukosa kukamilika na hivyo kukwamisha azma ya sheria ndogo hiyo.

Mheshimiwa Spika, mfano mwingine wa dosari ya uandishi wa majedwali inadhihirika katika sheria ndogo ya *The Tanzania Shipping Agencies (Shippers Registration) Regulations*, 2023, ambapo majedwali yote saba yaliyo katika sheria ndogo hii yana kasoro katika vifungu vinavyoyaanzisha. Hali hiyo inakwamisha azma ya masharti ya sheria ndogo inayaohusika.

Mheshimiwa Spika, maoni na mapendekezo; maelezo ya jumla; kwa kuwa ni jukumu la Kamati hii kujiridhisha iwapo sheria ndogo zimekidhi masharti ya Katiba, sheria mama na sheria nyingine za nchi; uchambuzi ulizingatia vigezo hivyo. Matokeo ya uchambuzi huo yanafanikisha dhima ya Bunge kusimamia madaraka yake iliyoyakasimu kwa mamlaka nyingine ili kutunga sheria ndogo.

Mheshimiwa Spika, maoni ya jumla; kwa kuwa utekelezaji wa sheria ndogo unagusa moja kwa moja maisha ya wananchi, dosari zilizobainika zinawezakuwa na madhara katika utekelezaji wa sheria na zinaathiri maisha ya watu. Kwa msingi hiyo, Bunge ambalo ndilo lenye madaraka ya asili ya kutunga sheria linapaswa kuzitaka mamlaka zinazohusika na sheria ndogo zenye dosari kurekebisha haraka.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo; kutokana na matokeo ya uchambuzi, Kamati inapendekeza kama ifuatavyo:-

Moja, sheria ndogo kuwa na masharti yanayokinzana na masharti ya Katiba:-

Kwa kuwa, baadhi ya sheria ndogo zimebainika kuwa na masharti yanayokinzana na masharti ya Katiba na hivyo kuwa kinyume na misingi ya sheria inayotambua ukuu wa Katiba;

Na kwa kuwa, ukiukwaji wa msingi wa masharti ya Katiba kwa sheria ndogo yoyote au sheria ya Bunge ni kinyume na Ibara ya 64(5) ya Katiba ambayo inabatilisha sheria inayokinzana na Katiba;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba mamlaka zilizoweka sheria ndogo zote ambazo zimebainika kuwa na dosari ya kukinzana na masharti ya Katiba ya nchi zifanye marekebisho.

Mheshimiwa Spika, mbili, dosari ya kuwa na masharti yanayokinzana na masharti ya sheria mama na sheria nyingine za nchi:-

Kwa kuwa, zipo sheria ndogo ambazo zimebainika kuwa na vifungu vinavyokinzana na masharti ya sheria mama na sheria nyingine za nchi, jambo ambalo–

(i) Linatofautiana na dhamira ya Bunge kukabidhi kwa mamlaka Serikalini madaraka ya kufafanua sheria ndogo;

(ii) Ni ukiukwaji wa katazo lililowekwa na kifungu cha 36 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1; na

(iii) Halisaidii utekelezaji wa sheria mama inayohusika au Sheria nyingine ya nchi ilivyostahili.

Na kwa kuwa, kuwepo kwa sheria ndogo zinazokinzana na sheria mama au sheria nyingine za nchi;

(i) Ni jambo linalobatilisha sheria ndogo hizo kwa kiasi inachokiuka na kukinzana na masharti ya sheria mama au sheria nyingine za nchi.

(ii) Ni kuvuka mipaka iliyowekwa na Bunge ambalo halitarajii na haliwezi kutarajia sheria inayotokana na Bunge kukasimu madaraka yake, likiuke sheria za Bunge.

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba mamlaka zilizotunga sheria ndogo ambazo zimebainika kukinzana na masharti ya sheria mama na sheria nyingine za nchi, zifanye marekebisho ili kuondoa dosari hizo.

Mheshimiwa Spika, tatu ni masharti yasiyo na uhalisia:-

Kwa kuwa, dosari ya kuwa na masharti yasiyozingatia uhalisia imebainika kuwa katika baadhi ya sheria ndogo, jambo linaloweza kuchangia ugumu wa utekelezaji;

Na kwa kuwa, athari ya ugumu katika utekelezaji wa sheria ndogo ni jambo linalovuruga upatikanaji wa tija ya sheria ndogo hizo na kuondoa maana ya madhumuni ya kukasimu madaraka ya Bunge kutunga sheria;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba mamlaka zinazotunga sheria ndogo zilizobainika kuwa na masharti yasiyozingatia uhalisia, zifanye marekebisho ili kuondoa dosari za masharti yasiyo na uhalisia.

Mheshimiwa Spika**,** nne, dosari ya kutoendana na uhalisia wa sheria:-

Kwa kuwa, baadhi ya sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni wakati wa Mkutano wa Kumi na Mbili na Mkutano wa Kumi na Tatu zimebainika kuwa na dosari ya kutokuendana na misingi ya uandishi wa sheria;

Na kwa kuwa, uandishi wa sheria ndogo usioendana na misingi ya uandishi wa sheria;

(i) Unaweza kuathiri maana iliyokusudiwa katika sheria ndogo inayohusika; na

(ii) Unaweza kuwa sehemu ya chanzo cha sheria ndogo hiyo kushindwa kufanikisha madhumuni ya sheria.

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba mamlaka zilizokabidhiwa madaraka ya kutunga sheria ndogo zilizochambuliwa na kuripotiwa katika taarifa hii, zirekebishe dosari za kutoendana na misingi ya uandishi wa sheria.

Mheshimiwa Spika, tano, ni dosari za uandishi wa majedwali:-

Kwa kuwa, majedwali ni sehemu ya sheria kwa mujibu wa kifungu cha 25(2) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria na kwamba yanastahili kusomwa kwa pamoja na vifungu vinavyohusika, lakini baadhi ya sheria ndogo zinazochambuliwa zimebainika kuwa na dosari katika majedwali;

Na kwa kuwa, dosari za uandishi wa majedwali ya baadhi ya sheria ndogo zilizochambuliwa na kuripotiwa katika taarifa hii,

(i) Ni jambo linaloweza kukanganya ufafanuzi unaotolewa; na

(ii) Linatatiza utekelezaji wa sheria ndogo inayohusika kutokana na kukosa ukamilifu.

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba mamlaka zilizotunga sheria ndogo ambazo zimebainika kuwa na dosari katika uandishi wa majedwali, zifanye marekebisho ya kuondoa dosari hizo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kurekebisha dosari zilizobainika kwenye sheria ndogo na madhara yake:-

Kwa kuwa, dosari zilizobainika kwenye sheria ndogo kama ilivyofafanuliwa katika jedwali la uchambuzi ambalo ni Kiambatisho Na. 1 ni jambo ambalo:-

(i) Linaendeleza madhara yasiyokubalika na Bunge lenye madaraka halisi ya kutunga sheria za nchi; na

(ii) Linalohitaji hatua stahiki za Bunge linalokasimu madaraka yake kwa mamlaka zilizoweka sheria ndogo ambazo zimebainka kuwa na dosari na kutakiwa kurekebishwa.

Na kwa kuwa, kuendelea kwa madhara ya dosari zilizobainika kwenye sheria ndogo hata baada ya kuazimiwa na Bunge zirekebishwe, ni suala ambalo: -

(i) Linaweza kuliweka Bunge lawamani kwa wananchi ambao hawalitarajii au wanalitarajia kuhakikisha kwamba sheria za nchi zinakidhi mahitaji badala ya kuwa na dosari;

(ii) Linaweza kuwa linatokana na Bunge kutopatiwa Taarifa za utekelezaji wa mamlaka yake.

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zote zinazohusika na sheria ndogo zenye dosari kama zilivyotajwa katika Kiambatisho Na. 01:-

(i) Zitekeleze maazimio haya kwa kasi inayotakiwa ili kuepusha madhara ya dosari zilizobainishwa; na

(ii) Ziwasilishe taarifa ya utekelezaji wa maazimio yote kuhusu dosari za sheria ndogo kwa Katibu wa Bunge ifikapo Jumatatu ya kwanza ya mwezi Mei, 2024.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kutokukamilika kwa utekelezaji wa maazimio ya Bunge yaliyolenga kurekebishwa kwa sheria ndogo:-

Kwa kuwa, athari za dosari za sheria ndogo zinafikia hatua ya juu ya kushughulikiwa kwa marekebisho ya sheria ndogo kutangazwa katika Gazeti la Serikali, lakini zipo mamlaka zilizobainika kutofikia hatua za kutangaza marekebisho ya sheria ndogo, licha ya maazimio ya Bunge kutaka marekebisho hayo; na pili, wananchi wanaowakilishwa na Bunge wanaendelea kuathiriwa na madhara ya dosari za sheria ndogo licha ya Bunge kuwa na maazimio yaliyolenga kuondoa athari hizo;

Na kwa kuwa, kuendelea kwa dosari za sheria ndogo na athari zinazotokana na dosari hizo ni jambo ambalo: -

(i) Linalotatiza dhamira ya Bunge kukasimu madaraka yake kwa mamlaka zilizoruhusiwa kuweka sheria ndogo hizo; na

(ii) Linastahili kupatiwa maelezo ya mamlaka zinazohusika ili kutatua tatizo la msingi linaloweza kuwa linakwamisha dhamira ya Bunge.

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba mamlaka zilizobainika kutokuwa zimefikia hatua ya kutangaza marekebisho ya sheria ndogo zenye dosari kama zilivyobaishwa katika Kiambatisho Na. 02 ziwasilishe taarifa za utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu taarifa za utekelezaji kwa Katibu wa Bunge, mwezi Machi, 2024 wakati wa vikao vya Kamati kuekelea Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, shukrani; napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi kwa uongozi wako mahiri wa Bunge, ambao umeweka utaratibu wa Taarifa ya

Kamati ya Sheria Ndogo kuwasilishwa katika Vikao vya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Sheria Ndogo kwa kazi kubwa na nzuri ya kuchambua sheria ndogo pamoja na Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge. Umahiri wao katika kazi hii umewezesha kukamilika taarifa hii inayosomwa mbele ya Bunge lako leo hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa dhati nimshukuru Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu kwa uratibu unaowezesha mawasiliano mazuri kati ya Wizara na Kamati hivyo kuongeza tija katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa ufanisi. Aidha, niwashukuru Mawaziri waliohusika na sheria ndogo katika kipindi hicho kwa kutoa ushirikiano mkubwa ambao pia uliwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ya uchambuzi wa sheria ndogo na taarifa za utekelezaji wa maazimio ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, nichukue fursa hii kuishukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushiriki wao usio kifani katika vikao vya uchambuzi wa sheria ndogo na vikao vya kupokea taarifa za utekelezaji wa maazimio ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, napenda kuishukuru kwa dhati Ofisi ya Bunge chini ya uongozi mahiri wa Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* kwa ushirikiano anaoipatia Kamati hatimaye kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja; sasa naomba kutoa hoja kwamba, Bunge liipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2023 hadi Januari, 2024 pamoja na maoni na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

## TAARIFA YA MWAKA YA SHUGHULI ZA KAMATI KWA KIPINDI CHA FEBRUARI 2023 HADI JANUARI 2024 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

[Imetolewa chini ya Kifungu cha 136(15) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge,Toleo la Februari, 2023]

## SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI
### 1.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, Naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kwa kipindi cha kuanzia Februari 2023 hadi Januari 2024 ili kukidhi masharti ya Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Kanuni hiyo imeweka sharti la lazima kwa kila Kamati kuwasilisha Bungeni Taarifa ya Mwaka ya shughuli zake, kwa madhumuni ya kujadiliwa katika Mkutano wa Mwisho wa Bunge kabla ya Mkutano wa Bajeti. Nilikumbushe Bunge lako Tukufu kuwa, Mkutano huu ndio Mkutano wa mwisho kabla ya Mkutano wa Bajeti.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa inayowasilishwa leo Bungeni, inaelezea kwa kina shughuli zote zilizotekelezwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kwa kuzingatia masharti ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Kanuni hizo, zimeeleza bayana majukumu ya Kamati ya Sheria Ndogo na msingi wa shughuli zake.

#### 1.1.1 Madhumuni ya Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, Utaratibu wa Bunge kuitumia Kamati hii katika udhibiti wa utekelezaji wa madaraka ya kutunga Sheria yaliyokasimiwa kwa mamlaka mbalimbali serikalini, unahitaji desturi ya Kamati kuripoti kwa Bunge lenyewe. Taarifa hii ni sehemu ya desturi hiyo na madhumuni yake ni kulijulisha Bunge hali halisi ya utekelezaji wa madaraka ya kutunga sheria yaliyokasimiwa kwa mamlaka mbalimbali za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na maelezo hayo, Taarifa hii inalenga kuripoti mambo makuu mawili ambayo ni:

(i) Hali ya jumla kuhusu sheria ndogo zinazotumika nchini baada ya Bunge kukasimu madaraka kwa mamlaka mbalimbali kwa kipindi cha mwaka 2023; na

(ii) Mapendekezo yanayohitaji kufanyiwa kazi kutokana na maoni ya Kamati kuhusu hali hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Madhumuni hayo yanatimizwa kwa kufafanua kwa ujumla hali ya utekelezaji wa madaraka ya Bunge ya Kutunga Sheria yaliyokasimiwa Serikalini na Matokeo ya uchambuzi mahsusi wa Sheria Ndogo zilizowekwa mezani wakati wa Mkutano wa Kumi, Mkutano wa Kumi na Moja, Mkutano wa Kumi na Mbili na Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge. Aidha, Taarifa hii inaripoti matokeo ya uchambuzi mahsusi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo. Maazimio hayo yanahusu Sheria ndogo zilizowekwa Mezani wakati wa Mkutano wa Nane, Mkutano wa Tisa, Mkutano wa Kumi na Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge.

**1.1.2 Mawanda (*Scope*) ya Taarifa**

**Mheshimiwa Spika**, Mawanda ya Taarifa hii kulingana na madhumuni niliyoyabainisha, yanagusa masuala yafuatayo: -

(i) Shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha mwezi Februari 2023 hadi Januari, 2024;

(ii) Matokeo yaliyobainika wakati wa utekelezaji wa shughuli za Kamati; na

(iii) Mapendekezo kwa Bunge kuhusu mambo yanayostahili kufanyika au kutokufanyika kutokana na yaliyobainika kwa kipindi kinachoripotiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Shughuli zinazoripotiwa katika taarifa hii zinaliwezesha Bunge, ambalo msingi wa madaraka na mamlaka yake ni wananchi, kufuatilia namna madaraka ya kuweka sheria ndogo yanavyotumika. Ufuatiliaji huo ni jukumu la msingi la Bunge na unachangia katika kulisimamia lengo la Serikali ambalo ni ustawi wa wananchi kwa mujibu wa Ibara ya 8 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

## 1.2 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, imeweka masharti kuhusu muundo wa Taarifa inayowasilishwa Bungeni. Kwa madhumuni ya kuonesha uzingatiaji wa masharti hayo, naomba kubainisha Muundo wa Taarifa hii ambayo imegawanyika katika sehemu kuu tatu:

(i) Sehemu ya Kwanza ni utangulizi ambao unajumuisha maelezo ya jumla. Maelezo hayo yanakusudia kujenga msingi wa maudhui ya Taarifa hii, pia kuwezesha majadiliano ya Bunge;

(ii) Sehemu ya Pili inahusu ufafanuzi wa shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha Februari 2023 hadi Januari 2024. Sehemu hii inatoa maelezo ya kina kuhusu shughuli hizo, msingi wake pamoja na mambo yaliyobainika wakati wa utekelezaji wa shughuli za Kamati; na

(iii) Sehemu ya Tatu na ya mwisho inafanya majumuisho ya maoni ambayo chimbuko lake ni shughuli zilizotekelezwa. Nia ni kuweka msingi wa mapendekezo katika hoja ya Kamati inayojadiliwa Bungeni leo. Aidha, sehemu hii inatoa Mapendekezo kwa mfumo wa Hoja kama ilivyoelekezwa katika Kanuni ya 61 (3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge kuhusu mfumo wa maneno ya Hoja. Lengo ni kuliwezesha Bunge kufanya uamuzi ambao ni bayana.

**Mheshimwa Spika,** Taarifa hii inaishia kutoa hoja ili kutoa fursa ya kuungwa mkono na kujadiliwa inavyostahili. Kwa hatua hiyo, Bunge linaweza kukamilisha mjadala na kufanya uamuzi kuhusu eneo la udhibiti wa madaraka ya Sheria ndogo yanayokasimiwa kwa mamlaka mbalimbali serikalini.

**Mheshimiwa Spika,** Muundo huo wa Taarifa unaendana na wasilisho halisi la taarifa yenyewe na viambatisho ambavyo navyo vinastahili kuingia kwenye Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*). Kwa sababu hiyo, niliombe Bunge liipokee na kuijadili taarifa hii ikiwa na viambatisho vyote ambavyo ni: -

**Kiambatisho Na. 1** ambacho ni Jedwali la Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Kumi na mbili na Mkutano wa Kumi na Tatu; na

**Kiambatisho Na. 2** ambacho ni Jedwali la Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Kumi na Mkutano wa Kumi na Moja.

**Mheshimiwa Spika,** Viambatisho hivyo ni muhimu kwa kuwa vinafafanua kwa kina mambo yote yanayotokana na uchambuzi. Lengo lake ni kutoa picha halisi ya mambo yaliyobainishwa ili kuliwezesha Bunge kusimamia madaraka yake ya kutunga sheria iliyoyakabidhi kwa mamlaka nyingine serikalini.

### 1.3 Msingi wa Shughuli za Kamati

**Mheshimiwa Spika,** Shughuli za Kamati hii zinatokana na masharti yaliyofafanuliwa katika misingi mitatu ambayo ni: -

### 1.3.1 Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 4 (1) ya Katiba inaweka mgawanyo katika utekelezaji wa mamlaka ya nchi. Mgawanyo huo unalitambua Bunge kuwa ndio chombo chenye mamlaka ya kutekeleza shughuli za kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma. Aidha, Ibara ya 97 (5) ya Katiba inalipa Bunge uwezo wa kukabidhi kwa mtu yeyote au idara yoyote ya Serikali madaraka ya kuweka Kanuni zenye nguvu ya kisheria au kuzipa nguvu ya kisheria kanuni zilizowekwa na mtu yeyote au idara yoyote ya serikali.

### 1.3.2 Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 (*The Interpretation of Laws Act, Cap.*1)

**Mheshimiwa Spika,** Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 ni sheria inayozatiti kanuni za msingi kuhusu maana, ufafanuzi, uandishi, matumizi na mambo mengine kuhusu misingi ya sheria za nchi. Lengo lake ni kuimarisha sheria za nchi kwa kuleta utangamano na uwazi wa sheria zote ili hatimaye mfumo mzima wa sheria uwe na mambo yafuatayo:

(i) Uhakika wa uamuzi wowote unaofanyika kwa misingi ya sheria;

(ii) Urahisi katika ujazaji wa mapengo kwenye masharti ya sheria za nchi;

(iii) Matarajio ya kuondolewa kwa utata unaoweza kusababishwa na sheria yeyote; na

(iv) Uwezekano wa kurekebisha uandishi usiokamilika wa sheria za nchi pale unapotokea.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa msingi huu, mfumo wowote wa kuwa na sheria ndogo nchini pamoja na mchakato wa kuanzisha matumizi yake unapaswa kuzingatia masharti yaliyowekwa na sheria hii. Hivyo, uchambuzi wa Sheria Ndogo unaongozwa na Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 na Bunge linapojadili Taarifa hii pia linatarajiwa kupima kwa vigezo vilivyobainishwa katika masharti ya sheria hii.

**1.3.3 Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023**

**Mheshimiwa Spika,** Chimbuko la Kanuni za Kudumu za Bunge ni Ibara ya 89 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kanuni hizi zinaweka utaratibu wa kutekeleza Shughuli za Bunge. Utaratibu unaowekwa na Kanuni za Bunge ni kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa Shughuli za Bunge, sekretarieti ya Bunge na Kamati za Bunge ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo inayoripoti shughuli zake leo. Utaratibu huo unapaswa kufuatwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni za Bunge zinafafanua muundo na utaratibu wa utekelezaji wa majukumu na mamlaka ya Bunge na Kamati zake zinazojumuisha Kamati hii. Aidha, Kanuni hizo zinabainisha masharti mbalimbali kuhusu uendeshaji wa shughuli za Bunge na Kamati zake. Naomba kulihakikishia Bunge kwamba, shughuli zote zinazoripotiwa katika taarifa hii zinatokana na Kanuni za Bunge na zimefanyika kwa kuzingatia masharti yanayohusika.

**1.4 Njia Zilizotumika**

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni ya 142 (a) ya Kanuni za Bunge inaweka sharti la kila taarifa ya Kamati ya Bunge inayowasilishwa Bungeni kubainisha njia zilizotumika katika kutimiza majukumu

yake. Kwa kuzingatia sharti hilo, Taarifa hii inaeleza njia ambazo Kamati ilitumia kutekeleza majukumu yake. Njia hizo ni: -

(i) Mapitio ya matoleo ya Magazeti ya Serikali ya mwaka 2023 yaliyowasilishwa Mezani. Mbinu hiyo ilisaidia Kamati kuandaa orodha na jumla ya Sheria Ndogo zote zilizotangazwa katika magazeti hayo. Aidha, mbinu hiyo iliiwezesha Kamati kubaini mwelekeo na wigo wa kazi ya uchambuzi pamoja na kutambua sekta zinazohusika na sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni;

(ii) Uchambuzi wa awali wa sheria ndogo ili kubaini masharti yanayowekwa na Sheria hizo. Mbinu hiyo, ilisaidia kutathmini namna sheria ndogo zilivyozingatia masharti ya Katiba, Sheria Mama na Sheria zingine za nchi;

(iii) Uhakiki wa mtiririko wa maudhui ukilinganishwa na masharti yanayowekwa katika sheria ndogo. Mbinu hii ilifanikisha dhamira ya Kamati kubaini iwapo kuna ukamilifu uliokusudiwa na Bunge wakati wa kukasimu madaraka ya ufafanuzi uliotakiwa kufanywa na sheria ndogo inayohusika;

(iv) Uoanishaji wa masharti ya Sheria Ndogo inayohusika na misingi iliyowekwa katika Katiba na Sheria Nyingine za nchi. Nia ni kujiridhisha na ukubalifu wa Sheria Ndogo kwa misingi ya Sheria za nchi inayopaswa kuzingatiwa;

(v) Urejeleaji wa madhumuni ya Sheria mama iliyoruhusu kutungwa kwa sheria ndogo na kupima iwapo maudhui ya sheria ndogo yanaweza kufanikisha madhumuni ya Sheria Kuu. Mbinu hii imewezesha kufanikisha wajibu wa Bunge kujiridhisha iwapo sheria ndogo inafanikisha nia yake ya kutunga Sheria Kuu na kukasimu madaraka ya ufafanuzi; na

(vi) Mahojiano na mamlaka zilizotunga sheria ndogo kwa idhini ya Bunge. Mbinu hii ililenga kuiwezesha Kamati kupima uthabiti wa hoja dhidi ya ufafanuzi wa mamlaka zinazohusika, jambo linalosaidia kuiwezesha Kamati kuwa na mapendekezo ya maazimio ya Bunge yenye kufaa na yanayotekelezeka.

**Mheshimiwa Spika**, Naomba kulihakikishia Bunge lako tukufu kuwa, njia zilizotumika zimechangia kubainika kwa mambo yanayojenga maoni ya Kamati ambayo ni msingi wa Maazimio ya Bunge yanayopendekezwa katika taarifa hii.

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA

### 2.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** Shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha mwaka 2023, zinahusu kujijengea uwezo wa utekelezaji wa majukumu na madaraka ya Kamati na utekelezaji wa majukumu ya msingi kwa mujibu wa Kanuni za Bunge. Shughuli hizo kwa ujumla zinaainishwa kwa kujumuishwa katika maeneo matatu ambayo ni:

(i) Mafunzo kwa Wajumbe wa Kamati yaliyolenga kuwajengea uwezo na kuwapa muktadha wa kazi;

(ii) Uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni kwenye Mkutano wa Kumi, Mkutano wa Kumi na Moja, Mkutano wa Kumi na Mbili na Mkutano wa Kumi na Tatu; na

(iii) Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni kwenye Mkutano wa Nane, Mkutano wa Tisa, Mkutano wa Kumi na Mkutano wa Kumi na Moja.

**Mheshimiwa Spika,** Matokeo ya Uchambuzi wa Sheria Ndogo za Mkutano wa Kumi na Mkutano wa Kumi na Moja yaliwasilishwa Bungeni katika Taarifa ya Kamati mnamo tarehe 5 Septemba, 2023 wakati wa Mkutano wa Kumi na Mbili wa Bunge. Katika Taarifa hii matokeo ya Uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni wakati wa Mkutano wa Kumi na Mbili na Mkutano wa Kumi na Tatu, yanaripotiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo za Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa wa Bunge yaliwasilishwa Bungeni wakati wa Mkutano wa Kumi na Mbili tarehe 5 Septemba, 2023. Taarifa hii inaripoti Matokeo ya Utekelezaji wa

Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Mkutano wa Kumi na Moja, yanabainishwa katika Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** Shughuli za Kamati zinazoripotiwa zimetokana na masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano na zinaongozwa na Sheria ya Tafsiri ya Sheria Sura ya 1. Utaratibu uliotumika umefuata masharti ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Kwa msingi huo, shughuli hizo zinahusu masharti katika mambo makuu mawili. Jambo la kwanza ni mamlaka ya kutunga sheria. Bunge ndicho chombo chenye mamlaka kamili ya kutunga sheria na kufuta sheria za nchi.

**Mheshimiwa Spika,** Jambo la pili ni kuhusu masharti ya kukabidhi kwa mtu au idara ya serikali madaraka ya kufafanua Sheria zinazotungwa na Bunge. Nilikumbushe Bunge lako tukufu kuwa, lengo la hatua hiyo ya Bunge ni kusaidia ufafanuzi wa Sheria za Bunge katika utekelezaji ikiwemo, uzingatiaji wa mambo maalumu ya kitaalamu na mazingira halisi ya utekelezaji. Kwa kufanya hivyo, Bunge halijiondoi kwenye dhima ya kuweka sheria za nchi zinazosimamia maslahi ya wananchi na ustawi wao kwa ujumla. Hivyo, shughuli zinazoripotiwa zinalisaidia Bunge kuwajibika katika utekelezaji wa shughuli zake kwa lengo la kuhakikisha kwamba, sheria za nchi zinalindwa na kutekelezwa kama inavyoelekeza katika Ibara ya 9 (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

### 2.1.1 Mafunzo kwa Wajumbe

**Mheshimiwa Spika**, Mafunzo kwa Wajumbe ni shughuli iliyotokana na matokeo ya kutekelezwa kwa masharti ya Kanuni ya 135 (7) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Kanuni hiyo iliweka masharti yaliyotaka ujumbe wa Kamati za Kudumu za Bunge ukome baada ya nusu ya kwanza ya maisha ya Bunge, yaani miaka miwili na nusu. Kwa msingi huo, uteuzi wa Wajumbe ulifanyika na Kamati ikapata Wajumbe wapya ambao kwa muktadha wa kazi za Kamati ililazimu kuwa na mafunzo ya awali wakati wa Vikao vya Kamati mwezi Machi 2023.

**Mheshimwa Spika,** Kamati hii kwa asili (*by nature*), ni Kamati ya Sekta Mtambuka yenye jukumu ambalo lina upekee na

linalobeba dhima ya asili ya Bunge. Kwa mantiki hiyo, mafunzo hayo muhimu yalilenga kuwazoeza Wajumbe mazingira mapya ya kazi yao ya kipekee. Aidha, mafunzo yaliwatambulisha wajumbe kwenye majukumu, mchakato, vigezo vya kazi, misingi na desturi za shughuli za Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo. Mambo hayo yalisaidia ushiriki mzuri wa wajumbe katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati na uzingatiaji wa misingi ya kazi.

**Mheshimiwa Spika**, Kutokana na mazingatio yaliyopatikana kutoka kwenye mafunzo, uchambuzi wa Sheria ndogo umefanyika kwa namna yenye tija inayodhihirishwa na matokeo ya uchambuzi kama inavyoripotiwa.

### 2.1.2 Uchambuzi wa Sheria Ndogo Zilizowasilishwa na Matokeo Kuripotiwa Bungeni

**Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha Januari 2023 hadi Agosti 2023, Serikali iliweka Mezani Bungeni Magazeti yaliyotangaza Sheria Ndogo. Jumla ya Sheria ndogo mia nne ishirini na nne (424) zilichambuliwa na matokeo yake yaliwasilishwa Bungeni wakati wa Mkutano wa Kumi na Mbili na maazimio yaliyolenga kurekebisha dosari yalitolewa na kupitishwa na Bunge. Naomba kuthibitisha kuwa mjadala wa Bunge ulikuwa na tija kwa wananchi na wapo waliopongeza kupitia vyombo vya Habari, warsha na makongamano mbalimbali.

### 2.1.3 Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo ambao Matokeo Yake Yaliripotiwa Bungeni

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa Bunge ndilo lenye dhamana ya kuweka sheria za nchi zinazowezesha ustawi wa wananchi, Kamati ilifuatilia utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyolenga kuweka sawa masharti ya kisheria nchini. Kwa kipindi cha Januari 2023 hadi Agosti 2023, Kamati ilipokea Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyolenga kuondoa dosari katika jumla ya Sheria ndogo thelathini na moja (31) zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa. Maazimio yote kuhusu Sheria Ndogo hizo yametekelezwa. Sheria Ndogo hizo zilikuwa chini ya: -

(i) Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI);
(ii) Ofisi ya Makamu Wa Rais , Muungano na Mazingira;
(iii) Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi;
(iv) Wizara ya Fedha; na
(v) Wizara ya Madini.

**Mheshimiwa Spika**, Utaratibu huo uliliweka Bunge katika nafasi yake ya kusimamia utekelezaji wa madaraka ya kuweka sheria ndogo yaliyokabidhiwa kwa mamlaka mbalimbali serikalini. Kamati itaendelea kuutumia utaratibu huo ili kulisaidia Bunge katika utekelezaji wa madaraka yake kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano.

**2.1.4 Uchambuzi wa Sheria Ndogo Zilizowasilishwa Bungeni wakati wa Mkutano wa Kumi na Mbili na Mkutano wa Kumi na Tatu**

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 38 (1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kimeweka sharti kwa Sheria Ndogo zote zinazotangazwa kwenye Gazeti la Serikali kuwasilishwa Bungeni ndani ya siku sita za vikao vinavyofuata baada ya tarehe ya kuchapisha toleo la Gazeti lililotangaza Sheria Ndogo hizo. Kwa msingi huo, Sheria Ndogo zilizochapishwa baada ya Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge ziliwasilishwa Bungeni wakati wa Mkutano wa Kumi na Mbili na zile zilizochapishwa baada ya Mkutano wa Kumi na Mbili ziliwasilishwa wakati wa Mkutano wa Kumi na Tatu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilichambua Sheria Ndogo hizo kwa mujibu wa Kifungu cha 10 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Matokeo ya uchambuzi huo yanaripotiwa katika Taarifa hii ili kuliwezesha Bunge kufanya uamuzi bayana unaohusu dosari zilzobainika wakati wa uchambuzi. Ufafanuzi wa matokeo hayo unapatikana katika **kipengele cha 2.2.**

**2.1.5 Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Mazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo ambao Matokeo yake Hayajaripotiwa Bungeni**

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo, ambao matokeo yake hayajaripotiwa, unahusu sheria ndogo sita (6). Maazimio hayo yalitolewa baada ya Taarifa ya Kamati iliyowasilishwa tarehe 5 Septemba, 2023 wakati wa Mkutano wa Kumi na Mbili.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia kuwa Kamati ya Sheria Ndogo ni nyenzo ya Bunge ya kufuatilia utekelezaji wa madaraka ya kuweka sheria ndogo yanayokabidhiwa kwa mamlaka mbalimbali serikalini, Kamati ilichambua Taarifa za Utekelezaji wa maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo. Matokeo ya Uchambuzi huo yanafafanuliwa katika **kipengele cha 2.3** cha Taarifa hii.

## 2.2 Matokeo ya Uchambuzi wa Sheria Ndogo Zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Kumi na Mbili na Mkutano wa Kumi na Tatu

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Kumi na Mbili na Mkutano wa Kumi na Tatu umefanyika kwa lengo la kufanikisha wajibu wa Bunge kudhibiti mamlaka yake ya kutunga sheria nchini. Kwa desturi za uendeshaji wa Bunge letu, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo imekuwa karakana ya Bunge lako ambapo wajibu wa udhibiti wa sheria ndogo huanza kutekelezwa. Dhima kuu ya Kamati wakati wa uchambuzi ni kubainisha dosari na baadaye kulishauri Bunge kuhusu hatua stahiki za kuchukua.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mantiki hiyo**,** matokeo ya uchambuzi wa sheria ndogo ni muhimu kuwasilishwa Bungeni ili iwe rahisi kwa Bunge kudhibiti madaraka yake ya kutunga sheria yaliyokasimiwa kwa mamlaka nyingine serikalini. Ninaomba kulihakikishia Bunge lako kuwa, matokeo ya uchambuzi wa sheria ndogo yanayowasilishwa kupitia taarifa hii, yameoneshwa kwa namna rahisi itakayoliwezsha Bunge kuona hatua stahiki dhidi ya dosari zinazobainishwa. Kwa urahisi wa kufuatilia, Jedwali la Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Kumi na Mbili na Mkutano wa Kumi na Tatu linaambatishwa na kuwa **Kiambatisho Na. 01**. Jedwali hilo linachanganua sheria ndogo zenye dosari mbalimbali kama ifuatavyo: -

(i) Dosari kumi na tatu (13) za masharti yanayokinzana na Katiba;

(ii) Dosari ishirini na saba (27) za masharti yanayokinzana na Sheria Mama na sheria nyingine za nchi;

(iii) Dosari sita (6) za masharti yasiyo na uhalisi katika utekelezaji;

(iv) Dosari sabini (70) za kutoendana na misingi ya uandishi; na

(v) Dosari saba (7) za uandishi wa Majedwali.

**Mheshimiwa Spika**, Lengo la Sheria Ndogo ni kufafanua na kutekeleza masharti yaliyowekwa na sheria ya Bunge. Hivyo, dosari au hitilafu zilizobainika kutokana na uchambuzi wa Kamati, zinaweza kukwamisha lengo la Bunge kuhusu utekelezaji wa sheria ya Bunge. Kwa mantiki hiyo, haitarajiwi kwamba Bunge litaendelea na utungaji wa sheria zake pasipo kusahihisha dosari zilizopo katika sheria ndogo.

**Mheshimiwa Spika**, ili Bunge liwe katika nafasi nzuri ya kutoa uamuzi wake, sehemu hii ya taarifa inaonesha kwa kina mifano ya dosari zilizobainika kama ifuatavyo: -

### 2.2.1 Dosari ya Kuwa na Masharti Yanayokinzana na Masharti ya Katiba

**Mheshimiwa Spika,** Katiba ya Nchi ndiyo Sheria Kuu na inapaswa kuzingatiwa na sheria zote za nchi. Sheria zote zinazotungwa na Bunge hazipaswi kukinzana na masharti ya Katiba. Hali kadhalika, sheria ndogo inayofafanua sheria ya Bunge haitarajiwi kukinzana na masharti ya Katiba.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa madhumuni ya kujiridhisha na msingi huo, Kamati ilichambua sheria ndogo kwa kulinganisha na masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Matokeo ya uchambuzi yameonesha kuwa, zipo sheria ndogo ambazo zimebainika kuwa na masharti yanayokinzana na Katiba.

**Mheshimiwa Spika,** Mfano wa sheria ndogo hizo ni **Kanuni za Utoaji wa Leseni za Biashara za Mwaka 2023 (TS Na. 626 la 1 Septemba,2023).** Kanuni ya 16 inaweka katazo la uwakilishi wa wakili pale ambapo mamlaka imeruhusu mrufani kufika mbele yake kwa ajili ya kusikiliza shauri la rufaa. Masharti yanayowekwa na kanuni hii ni kinyume na masharti ya Ibara ya 13 (6) (a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,1977.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara hiyo inaelekeza kuwa, wakati haki na wajibu wa mtu yeyote vinahitaji kufanyiwa uamuzi wa mahakama au chombo kinginecho kinachohusika, basi mtu huyo pamoja na haki nyingine, atakuwa na haki ya kupewa fursa ya kusikiliswa kikamilifu

**Mheshimiwa Spika**, miongoni mwa misingi ya haki ya kusikilizwa kikamilifu ni fursa ya kuwakilishwa kisheria. Hivyo, katazo linalowekwa Kanuni ya 16 ya Kanuni hizo, linakiuka msingi muhimu wa haki ya kusikilizwa kikamilifu, jambo linalilokinzana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

### 2.2.2 Dosari ya Kuwa na Masharti Yanayokinzana na Sheria Mama na Sheria Nyingine za Nchi

**Mheshimiwa Spika,** Sheria ya Tafsiri ya Sheria ilitungwa na Bunge kwa lengo la kuweka misingi ya uandishi, tafsri, matumizi na mambo mengine muhimu kuhusu sheria za nchi kwa ujumla. Kifungu cha 36 (1) cha sheria hiyo, kimeweka masharti yanayozitaka sheria ndogo kutokwenda kinyume na masharti ya sheria mama na sheria nyingine za nchi. Ili kufuatilia uzingatiaji wa masharti hayo, Kamati ilitaka kujiridhisha na mambo makuu manne yafuatayo: -

(i) Iwapo sheria ndogo zinaendana na malengo ya sheria inayotekelezwa;

(ii) Iwapo ukubwa wa adhabu hauzidi kiwango cha ukomo wa adhabu ulioruhusiwa na sheria inayotekelezwa;

(iii) Iwapo taratibu zinazowekwa na sheria ndogo hazikiuki taratibu zinazotakiwa na sheria inayotekelezwa; na

(iv) Iwapo lugha iliyotumika katika sheria ndogo haipotoshi madhumuni ya sheria mama.

**Mheshimiwa Spika,** Matokeo ya uchambuzi yanaonesha kuwa, baadhi ya sheria ndogo kuwa zina masharti yanayokinzana na sheria mama na sheria nyingine za nchi. Mfano wa dosari ya kuwa na masharti yanayokinzana na sheria mama, yapo katika **Kanuni za Ukusanyaji na Uchakataji wa Taarifa Binafsi, 2023 (TS. Na 349 la tarehe 12 Mei, 2023).** Kanuni hizo ambazo zimetungwa chini ya

**Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (Na. 11 ya 2022)** zina masharti yanayokinzana na sheria mama. Dosari hiyo, inajitokeza katika **Kanuni ya 11** ambayo inaipa Tume nguvu ya kumruhusu mtu yeyote kupekua na kupakua Taarifa yoyote ilioingizwa katika rejesta.

**Mheshimiwa Spika,** Ruhusa inayotolewa na Tume kwa mtu yoyote kupekua na kupakua taarifa binafsi inakinzana na azma ya ulinzi wa taarifa binafsi. Mkinzano huo umetokana na kumruhusu mtu yeyote kuzifikia taarifa binafsi ilhali nia ya sheria mama ni ulinzi wa taarifa hizo.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa namna yalivyo masharti ya **Kanuni ya 11,** ni wazi kuwa hayaendani na lengo kuu la sheria mama la kuimarisha ulinzi wa taarifa binafsi zinazochakatwa na vyombo vya Serikali na vyombo binafsi. Kutoendana na lengo la sheria mama ni kukinzana na azma ya Bunge lililotunga sheria ya kuweka masharti kuhusu ulinzi wa taarifa binafsi.

**Mheshimiwa Spika,** Mfano mwingine ni sheria ndogo ziitwazo ***The Tanzania Shipping Agencies (Cargo Security and Safety of Terminal Operations) Regulations*, 2023** (**TS Na. 381 la 2023 la tarehe** 2 Juni 2023). Sheria ndogo hiyo, imeweka adhabu inayozidi kiwango cha ukomo wa adhabu kilichoruhusiwa na Sheria inayotekelezwa. Dosari ya kuweka adhabu inayozidi ukomo, inajitokeza katika **Kanuni ya 57 ya Kanuni hizo** inaweka adhabu ya jumla pale ambapo hakuna adhabu iliyotamkwa kwa kuvunja masharti yaliyopo katika Kanuni, kuwa ni adhabu ya faini isiyopungua shilingi milioni mbili na isiyozidi shilingi milioni ishirini ama kifungo kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka mitano ama adhabu zote kwa pamoja. Adhabu ya jumla inayotamkwa na kanuni hii inazidi kiwango cha ukomo wa adhabu kilichoruhusiwa na Sheria inayotekelezwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kama inavyofahamika, Bunge linapokabidhi kwa mamlaka za serikali madaraka ya kutunga kanuni, halikusudii kuruhusu sheria ndogo inayokinzana na masharti yanayowekwa na Bunge kupitia sheria linazozitunga. Hivyo, sheria ndogo zote zenye masharti yanayokinzana na masharti yaliyowekwa na Bunge hazistahili kuwa sehemu ya sheria za nchi na hazipaswi

kutumika kama inavyoelekezwa na masharti ya **Kifungu cha 36 (1)** cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria.

**2.2.3 Dosari ya Kuweka Masharti Yasiyo na Uhalisia**

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na masuala mengine, uandishi wa sheria hulenga kuweka masharti mbalimbali ambayo zao la utekelezaji wake ni kushughulikia, kufanikisha au kutatua jambo fulani miongoni mwa wanaolengwa na masharti yanayohusika.

**Mheshimiwa Spika,** Matokeo ya uchambuzi wa Kamati yanabainisha masharti yaliyowekwa na sheria ndogo ambayo utekelezaji wake hauna uhalisia ikilinganishwa na lengo la sheria ndogo. Dosari hiyo imebainika Kanuni za ***The Tanzania Shipping Agencies (Cargo Security and Safety of Terminal Operations) Regulations, 2023*** **(TS Na. 381 la 2023).** Kanuni hizi zinahusu usalama wa shehena na shughuli za kituoni kwa Meli za Mizigo *(terminal)*.

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni inaelekeza kuwepo kwa vali zuizi (*block valve*) katika maeneo ya kushushia na kuhifadhia shehena. Vali hizo zitafunguliwa pale ambapo janga la dharura limetokea. Hata hivyo **Kanuni ya 23(4)** inaelekeza kuwa, vali hizo zinapaswa kuwa wazi muda wote. Sharti hilo halina uhalisi katika utekelezaji, kwakuwa vali hizo haziwezi kuwa wazi muda wote isipokuwa tu, pale ambapo zitahitajika kutumika.

**2.2.4 Dosari ya Kutoendana na Misingi ya Uandishi wa Sheria**

**Mheshimiwa Spika**, Madhumuni ya misingi ya uandishi wa sheria ni kuwezesha sheria za nchi kufanikisha lengo lililokusudiwa na sheria inayohusika. Aidha, uzingatiaji wa misingi hiyo ni kuwezesha sheria kueleweka kwa urahisi miongoni mwa watu au wananchi wanaoguswa pamoja na wanaosimamia au wenye jukumu la kuzitafsiri sheria hizo. Ili kujiridhisha na uzingatiaji wa misingi ya uandishi wa sheria inayowekwa na Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Kamati ilitaka kujiridhisha na mambo yafuatayo: -

(i) Iwapo sheria inayotoa mamlaka ya kuwa na sheria ndogo inayohusika imerejewa inavyostahili; na

(ii) Iwapo Mamlaka iliyoweka sheria ndogo inayohusika imebainishwa.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati unaoripitiwa katika taarifa hii unabainisha dosari ya sheria ndogo kutozingatia masharti ya uandishi. Mfano wa sheria ndogo zenye dosari hiyo ni **Kanuni za Shughuli za Uzalishaji, Upelekaji na Usambazaji Umeme, 2023 (TS. Na 452 la tarehe 7 Julai, 2023)**, **ambazo zimetungwa chini ya** Sheria ya Umeme, Sura 131.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi unabainisha dosari katika **Kanuni ya 35** inayohusu notisi ya kuingilia huduma. Kanuni hii imeweka muda wa vipindi viwili tofauti ya utoaji wa notisi ambapo muda wa kwanza, kanuni inaonesha kuwa notisi itakuwa ni ya saa ishirini na nne na notisi ya pili inaonesha kuwa itakuwa ya muda wa siku saba.

**Mheshimiwa Spika**, Uandishi uliosababisha kuwa na notisi inayoonesha muda tofauti kuhusu utekelezaji wa jambo moja unasababisha kutokueleweka kwa muda mahsusi uliokusudiwa, hivyo kuleta mkanganyiko miongoni mwa watekelezaji na wanaolengwa na masharti ya sheria ndogo hizi hali inayoweza kuathiri utekelezaji wake. Kwa minajili hiyo, Bunge haliwezi kufumbia macho makosa hayo ya kiuandishi yanayoweza kuathiri dhima ya sheria ndogo ambayo msingi wake ni sheria iliyotungwa na Bunge lenyewe.

### 2.2.5 Dosari za Uandishi wa Majedwali

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Sheria ya Tafsri ya Sheria, Jedwali ni sehemu ya sheria hivyo inastahili kuwa na misingi inayofanikisha lengo la sheria. Bunge linapofuatilia sheria ndogo haliwezi kuacha kujiridhisha na jambo linaloweza kuathiri tija ya sheria. Kwa kuzingatia hilo, Kamati ilifanya uchambuzi kwa kujiridhisha na mambo yafuatayo: -

(i) Iwapo kuna kifungu wezeshi cha Jedwali inalohusika

(ii) Iwapo Kifungu wezeshi cha Jedwali hilo kimerejewa na kuoneshwa kwenye Jedwali hilo; na

(iii) Iwapo Jedwali linatoa ufafanuzi uliokamilika.

**Mheshimiwa Spika**, Matokeo ya uchambuzi yanaonesha kuwepo kwa sheria ndogo zenye dosari katika uandishi wa majedwali yaliyo katika sheria ndogo zinazohusika. Ikumbukwe kwamba, Majedwali katika Sheria yoyote huwa ni sehemu ya sheria kwa ajili ya kutoa ufafanunuzi wa ziada wenye lengo la kuwezesha utekelezaji na kutimiza malengo ya vifungu vya sheria vinavyohusika. Kwa msingi huo ikiwa kuna dosari yoyote ya Jedwali, upo uwezekano wa kutokamilika kwa malengo ya vifungu vinavyohusiana na Jedwali hivyo kukwamisha azma iliyokusudiwa na sheria inayohusika. Matokeo ya uchambuzi yanayoripotiwa katika taarifa hii yanaonesha kwamba, dosari ya uandishi wa majedwali katika baadhi ya sheria ndogo.

**Mheshimiwa Spika,** Mfano wa sheria ndogo hizo ni ***The Plant Health Regulations, 2023***, uchambuzi unabainisha makosa katika **Kanuni ya 95(1) na Kanuni ya 97(2)** ambazo zinarejea Jedwali la hamsini na moja pamoja na Jedwali la hamsini na saba. Uchambuzi wa Kamati ulibaini Majedwali yanayorejewa hayapo katika Kanuni hizo. Mfano mwingine wa dosari ya uandishi wa majedwali inadhihirika katika sheria ndogo ya ***The Tanzania Shipping Agencies (Shippers Registration) Regulations*, 2023** ambapo majedwali yote saba yaliyo katika sheria ndogo hii yana kasoro katika vifungu vinavyoyaanzisha.

**Mheshimiwa Spika,** Kasoro za uandishi wa majedwali ni vema zikaondoshwa kwa kuwa, zinaweza kutokutoa ufafanuzi unaokusudiwa na Kifungu kinachohusika hivyo kutofanikisha malengo ya Kanuni inayohusika. Kwa mantiki hiyo, Bunge lako ambalo ndio lenye mamlaka ya kutunga sheria za nchi, halipaswi kufumbia macho dosari zilizo katika sheria ndogo ambazo chimbuko lake ni mamlaka yaliyokasimiwa na Bunge.

### 2.3 Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo Zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Kumi na Mkutano wa Kumi na Moja

**Mheshimiwa Spika,** Katika msingi ya utekelezaji bora wa madaraka ya Bunge, upo wajibu wa kufuatilia utekelezaji wa maazimio hayo kwa niaba ya wananchi. Kwa desturi ya kibunge,

Kamati za Bunge ni nyenzo muhimu ya kuliwezesha Bunge kutoa picha halisi ya utekelezaji uliofanyika. Naomba kutoa taarifa kua, Kamati imefuatilia utekelezaji wa maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Mkutano wa Kumi na Moja. Ufuatiliaji huo ulifanyika kwa kuchambua taarifa za utekelezaji zilizowasilishwa na Serikali wakati wa vikao vya mwezi Oktoba, 2023 na Januari, 2024.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio uliangalia hatua mbalimbali zilizofikiwa katika utekelezaji wa Maazimio hayo. Uangaliaji na ufuatiliaji wa hatua zilizofikiwa katika utekelezaji ulidadisi mambo manne kama yafuatayo: -

(i) Iwapo hakuna kabisa utekelezaji wa maazimio;

(ii) Iwapo utekelezaji wa Maazimio umefikia hatua ya Rasimu ya marekebisho katika ngazi ya Wizara;

(iii) Iwapo utekelezaji wa Maazimio umefikia hatua ya Rasimu ya marekebisho kupelekwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa uhakiki; na

(iv) Iwapo utekelezaji wa Maazimio umefikia hatua ya marekebisho kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Naomba kufafanua hatua zilizofikiwa pamoja na kubainisha Wizara zinazohusika katika utekelezaji wa Maazimio ya Bunge. Lengo la ufafanuzi huu ni kuliwezesha Bunge kubaini hatua ya utekelezaji wa maazimio yake na kufanya uamuzi stahiki. Naomba kubainisha Wizara nne zinazohusika na utekelezaji wa maazimio ya Bunge kama ifuatavyo:-

(i) Wizara ya Katiba na Sheria ilikuwa na sheria ndogo mbili (02) zilizobainika kuwa na dosari Kumi na Moja (11);

(ii) Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari iliyokuwa na sheria ndogo moja (01) iliyobainika kuwa na dosari tatu (03);

(iii) Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi iliyokuwa na sheria ndogo moja (01) iliyobainika kuwa na dosari sita (06); na

(iv) Wizara ya Maliasili na Utalii iliyokuwa na sheria ndogo moja (01) yenye dosari sita (06).

**Mheshimiwa Spika,** Hatua zilizofikiwa na Wizara zilizotajwa katika utekelezaji wa Maazimio ya Bunge zinaoneshwa katika **Kiambatisho Na. 2** (Jedwali la Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Kumi na Mkutano wa Kumi na Moja). Pamoja na Jedwali hilo, kwa ajili ya kuwezesha majadiliano ya Bunge juu ya hoja hii, naomba kufafanua hatua zilizofikiwa kama ifuatavyo: -

**2.3.1 Hatua ya Rasimu ya Marekebisho katika Ngazi ya Wizara**

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge unabainisha matokeo yanayoonesha kwamba, Wizara moja ipo katika hatua za ndani za kukamilisha mchakato wa kufanya marekebisho ya sheria ndogo. Hatua hii inahusu Rasimu ya Marekebisho kuandaliwa na kuwepo katika ngazi ya Wizara. Kwa msingi huo, Wizara iliyo katika hatua hii haijatatua dosari kama ilivyoelekezwa na Bunge. Kufanya hivyo ni kuendeleza dosari zilizobainishwa, ambazo madhara yake yanaendelea kuwepo pasipo kuwa yamefanyiwa kazi.

**Mheshimiwa Spika**, Matokeo yanaonesha kuwa maazimio ya Bunge kuhusu dosari nane (08) za sheria ndogo ya ***The Law School of Tanzania (Admission, Fees and Conduct of Practical Training) Rules, 2022*** iliyo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria, ipo katika hatua ya michakato ya ndani ya Wizara. Hatua hiyo inahusu kukamilisha Rasimu ya Marekebisho ndani ya Wizara ili baadaye iwasilishwe Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa hatua ya uhakiki na kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, hatua ya Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo katika ngazi ya Wizara baada ya Maazimio ya Bunge, inaweza kuwa ni kuchelewesha azma ya Bunge ambalo ndilo mamlaka kuu ya utungaji wa sheria za nchi. Maazimio ya Bunge

yanalenga kusimamia madaraka yake yaliyokabidhiwa kwa mamlaka nyingine, hivyo utekelezaji wa maazimio unaochelewa, unazorotesha dhamira ya Bunge kuondoa dosari zilizobainika.
**Mheshimiwa Spika,** mfano wa changamoto inayoendelea kwa sababu ya kutokamilika kwa Marekebisho ya sheria ndogo inabainishwa katika **Kanuni ya 13**. Kanuni hii inaweka ulazima kwa wanafunzi kutii miongozo, utaratibu na maelekezo yaliyowekwa na Mkuu wa Chuo. Kanuni ndogo ya (2) inaelezea hatua ambazo Mkuu wa Chuo atachukua endapo hatoridhishwa na mahudhurio, bidii na ujuzi wa Mwanafunzi ikiwemo kuitaarifu Kamati ambayo Itashauri Bodi kuchukua hatua stahiki dhidi ya Mwanafunzi anayehusika.

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni haioneshi vigezo ambavyo Mkuu wa Chuo atatumia kujiridhisha na bidii na ujuzi wa mwanafunzi, aidha Kanuni haijaweka bayana hatua stahiki zinazoweza kuchukuliwa na Bodi endapo haijaridhishwa na bidii na ujuzi wa mwanafunzi. Vilevile, Kanuni hiyo haioneshi utaratibu wa kutoa taarifa kwa Mwanafunzi juu ya mchakato unaoendelezwa na Mkuu wa Chuo dhidi yake.

**Mheshimiwa Spika,** Dosari hizo zinaendeleza mkanganyiko na kutokufahamika kwa vigezo vya ujuzi na bidii vinavyokusudiwa na pia inaendeleza uwezekano wa wanafunzi kutopata taarifa kutokana juu ya mchakato unaoendelezwa na Mkuu wa Chuo dhidi yake.

### 2.3.2 Hatua ya Rasimu ya Marekebisho Kuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa Uhakiki

**Mheshimiwa Spika,** Hatua ya Rasimu ya Marekebisho iliyowasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uhakiki ni hatua muhimu ya kushughulikia maazimio ya Bunge kwa lengo la kuondoa dosari iliyobainika.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji ulibainisha kuwepo kwa utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu dosari ishirini (20) katika sheria ndogo tano (05) uliofikia hatua ya Rasimu ya Marekebisho kuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa uhakiki. Mchanganuo wa dosari zilizotolewa maazimio na kufikia hatua hiyo ni kama ifuatavyo: -

(i) dosari tatu (03) zinahusu sheria ndogo moja (01) inayosimamiwa na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari;

(ii) dosari tatu (03) moja inayosimamiwa na Wizara ya Katiba na Sheria;

(iii) dosari tano 05) zinahusu sheria ndogo moja (01) inayosimamiwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi;

(iv) dosari tatu (03) zinahusu sheria ndogo moja (01) inayosimamiwa na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo; na

(v) dosari sita (06) zinahusu sheria ndogo moja (01) inayosimamiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii.

**Mheshimiwa Spika**, Sheria ndogo zilizofikia hatua ya marekebisho kufanyiwa kwa hatua hii ni:

(i) Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta Kuhusu Usajili wa Laini za Simu, 2023;

(ii) *The Whistleblower and Witness Protection Regulations, 2023;*

(iii) Kanuni za Uteuzi, Malipo na Nidhamu kwa Madalali wa Baraza na Wasambaza Nyaraka za Mwaka, 2023;

(iv) *The Copyright and Neighbouring Rights (Royalty Collection and Distribution) (Collective Management Organisations) Regulations, 2023*; na

(v) Kanuni za Usafirishaji wa Mazao ya Misitu Kuingia Ndani ya Nchi na Kutoka Nje ya Nchi za Mwaka 2023

**Mheshimiwa Spika**, Mfano wa sheria ndogo zilizofikia hatua hiyo ni **Kanuni za Usafirishaji wa Mazao ya Misitu Kuingia Ndani ya Nchi na Kutoka Nje ya Nchi za Mwaka 2023.** Dosari iliyobainishwa

inahusu **Kanuni ya 16** inayorekebishwa kutobainisha muda wa Waziri kushughulikia rufaa.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa rejea ya Bunge lako tukufu, Kanuni ya 16 inazungumzia kuhusu Rufaa dhidi ya uamuzi wowote uliofikiwa chini ya Kanuni hizi kuwa, itapelekwa kwa Waziri ndani ya siku 30 tangu kutolewa kwa uamuzi unaohusika.

**Mheshimiwa Spika**, Dosari iliyobainishwa ni Kanuni kutotaja utaratibu wa namna ya kushughulikia rufaa ikiwemo *format* ya rufaa na muda ambao Waziri atapewa kufanyia kazi Rufaa inayohusika. Kukosekana kwa muda mahsusi kunaweza kusababisha Waziri ashughulikie shauri la rufaa kwa muda atakaoona unafaa, hali inayoweza kusababisha ucheleweshaji wa haki ya mrufani.

**Mheshmiwa Spika**, Azimio la Bunge katika Sheria Ndogo hii liliitaka mamlaka inayohusika kufanya marekebisho ya Kanuni ya 16 lengo likiwa kuweka muda maalum ambao utatumiwa na Waziri kushughulikia Rufaa hizo.

**Mheshimiwa Spika**, Hatua iliyofikiwa katika kutekeleza azimio la Bunge ikikamilika, itasaidia kuondoa ucheleweshaji wa mashauri ya rufaa yaliyowasilishwa kwa Waziri.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

### 3.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa Kamati hii imepewa majukumu ya kuchambua Sheria Ndogo ili kujiridhisha iwapo zimekidhi matakwa na masharti ya Katiba, Sheria inayotekelezwa na sheria ndogo inayohusika pamoja na sheria nyingine za nchi Kamati imechambua kwa kuzingatia vigezo hivyo. Kupitia uchambuzi unaofanywa na Kamati, Bunge huutumia katika kusimamia matumizi ya madaraka ya Bunge ya kutunga sheria iliyoyakasimu kwa mamlaka nyingine ili kutunga sheria ndogo.

### 3.2 Maoni ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, Kwakuwa utekelezaji wa sheria ndogo unagusa moja kwa moja maisha ya wananchi, ninaliomba Bunge

lako lipokee mapendekezo yote yaliyomo katika Taarifa hii na hatimaye liyafanyie kazi. Kwa madhumuni hayo, naomba kudhihirisha mtazamo wa Kamati unaotokana na uchambuzi kama ifuatavyo: -

**3.2.1 Dosari ya Sheria Ndogo kuwa na Masharti Yanayokinzana na Masharti ya Katiba**

**Mheshimiwa Spika,** Dosari ya sheria ndogo kuwa na maudhui yanayokinzana na Katiba ya Nchi ni jambo lisilopaswa kufumbiwa macho. Sababu yake ni kuwa, dosari hiyo inaiweka Sheria nje ya misingi ya utungaji wa sheria za nchi. Ni maoni ya Kamati kwamba, Bunge halitarajiwi kuruhusu madaraka yake ambayo limeyakabidhi kwa mamlaka nyingine, yatumike kinyume na misingi hiyo. Sababu ni kuwa, Bunge ambalo lina madaraka ya asili, linapotunga sheria za nchi linazingatia misingi hiyo.

**3.2.2 Dosari ya Sheria Ndogo kuwa na Masharti Yanayokinzana na Sheria Mama na Sheria Nyingine za Nchi**

**Mheshimiwa Spika,** Kama inavyofahamika, Sheria inayotungwa na Bunge hulenga kuweka masharti ya kushughulikia jambo fulani. Hivyo, sheria ndogo inayotokana na sheria iliyotungwa na Bunge, inastahili kuelekezwa kwenye dhamira ya Bunge kushughulikia jambo hilo na kutokinzana na Sheria nyingine yoyote iliyotungwa na Bunge au iliyowekwa kwa kuruhusiwa na Bunge. Kamati ina maoni kwamba, sheria ndogo zote zilizobainika kukinzana na masharti yaliyowekwa na sheria mama au sheria nyingine za nchi zinastahili kurekebishwa.

**3.2.3 Sheria Ndogo Kuwa na Masharti Yasiyozingatia Uhalisia**

**Mheshimiwa Spika,** Sheria ndogo zenye Masharti yasiyozingatia uhalisia zinaweza kukwamisha malengo ya Bunge kutunga Sheria Mama inayohusika. Ni maoni ya Kamati kuwa, zaidi ya kukwamisha malengo ya sheria mama, sheria ndogo zenye dosari hiyo zinaweza kusababisha kero kwa Wananchi. Bunge ambalo ni chombo cha uwakilishi wa wananchi linahitaji kuona madaraka yake yanayokabidhiwa kwa mamlaka nyingine hayatumiki kusababisha kero kwa wananchi.

### 3.2.4 Dosari ya Sheria Ndogo Kutoendana na Misingi ya Uandishi wa Sheria

**Mheshimiwa Spika,** Ufasaha katika uandishi wa sheria hufanikisha kueleweka kwake inavyostahili. Aidha, ufasaha huo, huweka maudhui yenye tafsiri inayokusudiwa na sheria inayohusika. Ni mtazamo wa Kamati kuwa, sheria ndogo zilizo na makosa ya uandishi zinaweza kuondoa maana iliyokusudiwa na kuzuia kufanikiwa kwa malengo ya sheria mama au sheria ndogo inayohusika.

### 3.2.5 Dosari za Uandishi wa Majedwali

**Mheshimiwa Spika**, Majedwali ni sehemu ya sheria ambayo kwa pamoja husomwa na vifungu vinavyohusika kwa ajili ya kufafanua zaidi. Kamati ina maoni kuwa, kutokuzingatiwa ipasavyo kwa misingi ya uandishi wa majedwali, ni jambo linaloweza kukanganya ufafanuzi unaotolewa. Mkanganyiko huo unaweza kuathiri utekelezaji wa sheria ndogo inayofafanua Sheria ya Bunge.

### 3.2.6 Utekelezaji wa Maazimio Yanayohusu Kurekebisha Sheria Ndogo

**Mheshimiwa Spika**, Uamuzi wowote unaofikiwa unalenga kutatua changamoto kwa kutoa suluhisho. Maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo yanalenga kusahihisha madhara ya dosari zilizobainika. Ni maoni ya Kamati kwamba, kutofikia hatua ya kutangaza marekebisho katika Gazeti la Serikali tofauti na ilivyokusudiwa kwenye maazimio ya Bunge ni jambo linaloendeleza madhara yanayotokana na dosari za sheria ndogo.

### 3.3 Mapendekezo

**Mheshimiwa Spika,** Msingi wa Mapendekezo ya Kamati ni maoni yake yaliyotokana na shughuli zinazoripotiwa katika Taarifa hii. Shughuli hizo zimebainisha uchambuzi na yatokanayo na uchambuzi. Kutokana na matokeo ya Uchambuzi Kamati inazingatia masharti ya Kanuni ya 61 ya Kanuni za Kudumu za Bunge kuhusu mfumo wa maneno kwenye mapendekezo yake na kuliomba Bunge lijadili na Taarifa hii na kupitisha maazimio kama ifuatavyo: -

### 3.3.1 Sheria Ndogo Kuwa na Masharti Yanayokinzana na Masharti ya Katiba

**KWA KUWA**, Baadhi ya sheria ndogo zimebainika kuwa na masharti yanayokinzana na masharti ya katiba, na hivyo kuwa kinyume na misingi ya sheria inayotambua Ukuu wa Katiba,

**NA KWA KUWA**, Ukiukwaji wa msingi wa masharti ya Katiba kwa sheria ndogo yoyote au sheria ya Bunge ni kinyume na Ibara ya 64 (5) ya Katiba ambayo inabatilisha sheria inayokinzana na Katiba,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Mamlaka zilizoweka sheria ndogo zote ambazo zimebainika kuwa na dosari ya kukinzana na masharti ya Katiba ya nchi zifanye marekebisho.

### 3.3.2 Dosari ya Kuwa na Masharti Yanayokinzana na Masharti ya Sheria Mama na Sheria Nyingine za Nchi

**KWA KUWA**, Zipo sheria ndogo ambazo zimebainika kuwa na vifungu vinavyokinzana na masharti ya Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi, jambo ambalo –

(i) linatofautiana na dhamira ya Bunge kukabidhi kwa mamlaka serikalini madaraka ya kufafanua sheria yake;
(ii) ni ukiukwaji wa katazo lililowekwa na Kifungu cha 36 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1; na
(iii) halisaidii utekelezaji wa Sheria mama inayohusika au Sheria nyingine ya nchi ilivyostahili,

**NA KWA KUWA,** Kuwepo kwa sheria ndogo zinazokinzana na sheria mama au sheria nyingine za nchi -

(i) ni jambo linalobatilisha sheria ndogo hizo kwa kiasi inachokiuka au kukinzana na masharti ya sheria mama au sheria nyingine za nchi,
(ii) ni kuvuka mipaka iliyowekwa na Bunge ambalo halitarajii na haliwezi kutarajia sheria inayotokana na Bunge kukasimu madaraka yake, likiuke Sheria za Bunge,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zilizotunga sheria ndogo ambazo zimebainika kukinzana na masharti ya sheria mama na sheria nyingine za nchi, zifanye marekebisho ili kuondoa dosari hizo.

### 3.3.3 Masharti Yasiyo na Uhalisia

**KWA KUWA**, dosari ya kuwa na masharti yasiyozingatia uhalisia imebainika katika baadhi ya sheria ndogo, jambo linaloweza kuchangia ugumu wa utekelezaji,

**NA KWA KUWA**, Athari ya ugumu katika utekelezaji wa sheria ndogo ni jambo linalovuruga upatikanaji wa tija ya sheria ndogo hizo na kuondoa maana ya madhumuni ya kukasimu madaraka ya Bunge kutunga Sheria,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Mamlaka zinazotunga sheria ndogo zilizobainika kuwa na masharti yasiyozingatia uhalisia, zifanye marekebisho ili kuondoa dosari za masharti yasiyo na uhalisia.

### 3.3.4 Dosari ya Kutoendana na Misingi ya Uandishi wa Sheria

**KWA KUWA,** Baadhi ya sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni wakati wa Mkutano wa Kumi na Mbili na Mkutano wa Kumi na Tatu, zimebainika kuwa na dosari ya kutokuendana na misingi ya uandishi wa sheria,

**NA KWA KUWA,** Uandishi wa sheria ndogo usioendana na misingi ya uandishi wa sheria –

(i) Unaweza kuathiri maana iliyokusudiwa katika sheria ndogo inayohusika; na

(ii) Unaweza kuwa sehemu ya chanzo cha sheria ndogo hiyo kushindwa kufanikisha madhumuni ya Sheria,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zilizokabidhiwa madaraka ya kutunga sheria ndogo zilizochambuliwa na kuripotiwa katika taarifa hii, zirekebishe dosari za kutoendana na misingi ya uandishi wa sheria.

### 3.3.5 Dosari za Uandishi wa Majedwali

**KWA KUWA**, Majedwali ni sehemu ya sheria kwa mujibu wa Kifungu cha 25 (2) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria na kwamba, yanastahili kusomwa kwa pamoja na vifungu vinavyohusika, lakini baadhi ya sheria ndogo zilizochambuliwa zimebainika kuwa na dosari katika uandishi wa majedwali;

**NA KWA KUWA**, Dosari za uandishi wa Majedwali ya baadhi ya sheria ndogo zilizochambuliwa na kuripotiwa katika Taarifa hii:

(i) ni jambo linaloweza kukanganya ufafanuzi unaotolewa,

(ii) Ni chanzo cha kutatiza utekelezaji wa Sheria ndogo inayohusika kutokana na kukosa ukamilifu,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zilizotunga sheria ndogo zilizobainika kuwa na dosari katika uandishi wa majedwali, zifanye marekebisho ili kuondoa dosari hizo.

### 3.3.6 Kurekebisha Dosari Zilizobainika kwenye Sheria Ndogo na Madhara Yake

**KWA KUWA**, Dosari zilizobainika kwenye sheria ndogo kama ilivyofafanuliwa katika Jedwali la Uchambuzi ambalo ni Kiambatisho Na. 1 cha Taarifa hii, ni jambo –

(i) linaloendeleza madhara yasiyokubaliwa na Bunge lenye madaraka halisi ya kutunga sheria za nchi,

(ii) linalohitaji hatua stahiki za Bunge linalokasimu madaraka yake kwa mamlaka zilizoweka sheria ndogo ambazo zimebainka kuwa na dosari na kutakiwa kurekebishwa,

**NA KWA KUWA**, Kuendelea kwa madhara ya dosari zilizobainika kwenye sheria ndogo baada ya kuazimiwa na Bunge zirekebishwe, ni suala ambalo:

(i) linaweza kuliweka Bunge lawamani kwa wananchi ambao wanalitarajia kuhakikisha kwamba, Sheria za Nchi zinakidhi mahitaaji badala ya kuwa na dosari,

(ii) linaweza kuwa linatokana na Bunge kutopatiwa Taarifa za utekelezaji wa Maazimio yake,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zote zinazohusika na sheria ndogo zenye dosari kama zilivyotajwa katika Kiambatisho Na. 01 cha Taarifa hii:

(i) zitekeleze maazimio haya kwa kasi inayotakiwa ili kuepusha madhara ya dosari zilizobainishwa; na

(ii) ziwasilishe Taarifa ya utekelezaji wa maazimio yote kuhusu dosari za sheria ndogo kwa Katibu wa Bunge ifikapo Jumatatu ya kwanza ya Mwezi Mei, 2024.

### 3.3.7 Kutokukamilika kwa Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge Yaliyolenga Kurekebishwa kwa Sheria Ndogo

**KWA KUWA**, Athari za dosari za sheria ndogo zinafikia hatua ya juu ya kushughulikiwa kwa Marekebisho ya Sheria Ndogo kutangazwa katika Gazeti la Serikali, lakini –

(i) Zipo mamlaka zilizobainika kutofikia hatua za kutangaza marekebisho ya sheria ndogo, licha ya Maazimio ya Bunge kutaka marekebisho hayo,

(ii) Wananchi wanaowakilishwa na Bunge wanaendelea kuathiriwa na madhara ya dosari katika sheria ndogo licha ya Bunge kuwa na maazimio yaliyolenga kuonda athari za dosari,

**NA KWA KUWA**, Kuendelea kwa dosari za sheria ndogo na athari zinazotokana na dosari hizo ni jambo –

(i) linalotatiza dhamira ya Bunge kukasimu madaraka yake kwa mamlaka zilizoruhusiwa kuweka sheria ndogo hizo; na

(ii) linalostahili kupatiwa maelezo ya Mamlaka zinazohusika ili kutatua tatizo la msingi linaloweza kuwa linakwamisha dhamira ya Bunge,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zilizobainika kutokuwa zimefikia hatua ya kutangaza marekebisho ya sheria ndogo zenye dosari kama zilivyobaishwa katika Kiambatisho Na. 2– Ziwasilishe taarifa za utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu taarifa za utekelezaji kwa Katibu wa Bunge, Mwezi Machi, 2024, wakati wa vikao vya Kamati kuekelea Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge.

### 3.4 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi kwa uongozi wako mahiri wa Bunge, ambao umeweka utaratibu wa Taarifa ya Kamati ya sheria ndogo kuwasilishwa katika vikao vya Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee kabisa niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Sheria Ndogo kwa kazi kubwa na nzuri ya kuchambua Sheria Ndogo pamoja na Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge. Umahiri wao katika kazi umewezesha kukamilika taarifa hii inayosomwa mbele ya Bunge lako leo hii. Kwa heshima kubwa naomba kuwatambua majina yao kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Dkt. Jasson Samson Rweikiza, (Mb) – Mwenyekiti;
2. Mhe. Ramadhan Suleiman Ramadhan,(Mb) - M/ Mwenyekiti;
3. Mhe. Ally Yahya Mhata, Mb - Mjumbe;
4. Mhe. Amour Khamis Mbarouk, (Mb) - Mjumbe;
5. Mhe. Jacob Tarimo Priscus, (Mb) - Mjumbe;
6. Mhe. Khamis Ali Vuai, (Mb) - Mjumbe;
7. Mhe. Eng. Dkt. Leonard M. Chamuriho, (Mb) -Mjumbe;
8. Mhe. Simai Hassan Sadiki, (Mb) - Mjumbe;
9. Mhe. Balozi. Liberata Rutageruka Mulamula, (Mb) -Mjumbe;
10. Mhe. Godwin Emmanuel Kunambi, (Mb) - Mjumbe;
11. Mhe. Abdallah Dadi Chikota, (Mb) - Mjumbe;
12. Mhe. Aloyce Andrew Kwezi, (Mb) - Mjumbe;
13. Mhe. Hamida Mohammed Abdallah, (Mb) - Mjumbe;
14. Mhe. Ally Mohamed Kassinge, (Mb) - Mjumbe;
15. Mhe. Dkt. Paulina Daniel Nahato, (Mb) - Mjumbe;
16. Mhe. Maryam Omar Said, (Mb) - Mjumbe;
17. Mhe. Zulfa Mmaka Omar, (Mb) - Mjumbe;
18. Mhe. Lugaha Joelson Mpina, (Mb) - Mjumbe;
19. Mhe. Amina Bakar Yusuf, (Mb) - Mjumbe;
20. Mhe. Latifa Khamis Juakali, (Mb) - Mjumbe; na
21. Mhe. Benaya Liuka Kapinga, (Mb) - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** Kwa dhati nimshukuru Mhe. Jenista Muhagama, (Mb) – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) kwa uratibu unaowezesha mawasiliano mazuri kati ya Wizara na Kamati hivyo, kuongeza tija katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa ufanisi. Aidha, niwashukuru Mawaziri waliohusika na sheria ndogo katika kipindi hicho, kwa kutoa

ushirikiano mkubwa ambao pia uliiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ya uchambuzi wa sheria ndogo na Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, Aidha, nichukue fursa hii kuishukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushiriki wao usio kifani katika Vikao vya Uchambuzi wa sheria ndogo na Vikao vya kupokea Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile, napenda kuishukuru kwa dhati Ofisi ya Bunge chini ya uongozi mahiri wa Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* kwa ushirikiano anaoipatia Kamati hatimaye kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

### 3.5 Hoja

**Mheshimiwa Spika,** Sasa naomba kutoa hoja kwamba, Bunge liipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2023 hadi Januari, 2024 pamoja na maoni na mapendekezo yaliyotolewa.

**Mheshimiwa Spika**, Naomba kutoa hoja.

Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mb
**MWENYEKITI Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo**
16 Februari, 2024

**KIAMBATISHO NA. 1**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**BUNGE LA TANZANIA**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO**

**JEDWALI LA UCHAMBUZI WA SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA BUNGENI KATIKA MKUTANO WA KUMI NA MBILI NA MKUTANO WA KUMI NA TATU**

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA BUNGENI KATIKA MKUTANO WA KUMI NA MBILI** | | | | | | |
| 1. | **(TS Na. 284)**<br><br>21 Aprili, 2023 | *The Plant Health Regulations, 2023* (Zimetungwa chini ya Kifungu cha 64) | *The Plant Health Act, (Cap133)* | Wizara ya Kilimo | 1. **Kanuni 3** inaweka tafsiri ya maneno mbalimbali yaliyotumika katika Kanuni hizi.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni haijaweka tafsiri ya maneno mbalimbali kama vile *Registrar, Authority, Service, United Republic, Labaratory, partner state,* ambayo yametumika katika kama vile Kanuni ya 5(1), 7(1), 10(6), 70(2), 115(2).<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kutokuwekwa kwa tafsiri ya maneno | 1. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kuweka tafsiri ya maneno na kufanya rejea ya tafsiri ya maneno inayotolewa katika sheria mama. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | hayo kunasababisha: -<br>a) Mkanganyiko katika usomaji wa Kanuni<br><br>b) Kutokueleweka kwa kile kilichokusudiwa na Kanuni hizi hali inayoweza kuathiri malengo yalikusudiwa. | |
| | | | | | 2. **Kanuni ya 4 (1) (g)** inaweka sharti la kuwasilisha risiti malipo yatakayoelekezwa.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni hazioneshi viwango vya malipo hayo. | 2. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuonesha malipo yanayokusudiwa yanahusu maombi ya usajili wa kiutilifu ili kuendana na maudhui ya Jedwali la Pili. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 3. **Kanuni ya 4(8) na 4(9)** zinaweka masharti kwa mamlaka kumtaarifu mhusika kwa maandishi kuomba kibali kwa ajili ya kusajili kiuatilifu. Pia vinaonesha hatua za kufuatwa iwapo maombi ya usajili yamekataliwa.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>**Kanuni ya 4(8) na 4(9)** zina makosa ya uandishi kwa kutumia neno "*concern*". Hali hiyo inasababisha mkanganyiko wa maudhui yaliyokusidiwa na Kanuni hizi. | 3. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuondoa makosa ya uandishi kwa kufuta neno "*concern*" na badala yake kuweka neno "*concerned*" |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 4. **Kanuni ya 11(2)** inaweka masharti yanazoweza kusababisha kukataliwa kwa maombi ya kusajili viatilifu.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>**Kipengele (h)** kinaweka sababu ya kukataliwa kuwa ni kukiuka sharti jingine lolote ambalo Mamlaka inaweza kuona lina mashiko. Maudhui ya kipengele hiki yanasababisha kutokutabilika kwa masharti mengine na kusababisha kukosekana kwa muongozo juu ya | 4. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kuondoa sharti la kukata usajili kwa kuzingatia sababu nyingine yoyote ambayo Mamlaka itaona ina mashiko. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | masharti yanayokusudiwa. | |
| | | | | | 5. **Kanuni ya 14** inaweka masharti ya kuzingatiwa wakati ili kupatiwa usajili wa kudumu wa viautilifu.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni imechanganya masharti ya usajili wa kudumu na usajili wa majaribio (*experimental*) katika kanuni moja. | 5. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kutenganisha masharti ya usajili wa kudumu na usajili wa majaribio (*experimental*) |
| | | | | | 6. **Kanuni ya 22(1) (d)** inahusu kusitishwa kwa kibali cha usajili kwa sababu ya maslahi ya umma. | 6. Kanuni inayiwe marekebisho kwa kuweka ufafnuzi wa maslahi katika nyanja za kijamii, kiuchumi. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | **<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni haielezi bayana maslahi hayo ni yapi. Kutokuelezwa kwa masharti hayo kunasababisha kutokutabilika kwa masharti ya Kanuni hii. | |
| | | | | | 7. Kanuni ina makosa ya mtiririko wa kiuandishi kwa kuweka **Kanuni ya 29** mara mbili.<br>Kujirudia kwa Kanuni hiyo mara mbili kunaleta changamoto ya kiusomaji na urejeaji. | 7. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuondoa makosa ya kiuandishi |
| | | | | | 8. **Kanuni ya 30** inayozungumzia leseni ya muuzaji wa | 8. Kanuni ifanyiwe ili kuonesha uhishaji wa keseni |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | viuatilifu (*pesticides*) na viuatilifu vya kibaiolojia (*bio pesticides*) itafikia mwisho kila ifikapo tarehe 31 Disemba ya kila mwaka.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni haitofautishi tarehe za ukataji wa Leseni kwa wahusika walipoata Leseni kwa vipindi tofauti vya mwaka mmoja.<br><br>Hali hii inaweza kuleta madhara kwa walio na Leseni zilizopatikana kwa vipindi tofauti kwa mwaka kuisha kwa wakati wakati mmoja | utafanyika kila baada ya mwaka kwa kuzingatia tarehe ya kutolewa leseni. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 9. **Kanuni ya 31(2)** inaweka masharti kwa mzambazaji aliyesajiliwa kutunza na kuhuisha kumbukumbu za usambazaji na uuzaji wa viuatilifu.<br><br>**Kanuni 31(2) (e)** inamtaka msambazaji kutunza kumbukumbu ya taarifa nyingine yoyote kama itakavyoelekezwa na mamlaka.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni inaweka sharti la kutunza nyaraka nyingine yoyote bila kutaja nyaraka hizo. | 9. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kuondoa sharti la kumtaka msambazaji kutunza kumbukumbu ya taarifa nyingine yoyote kama itakavyoelekezwa na mamlaka. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Hali hii inaweza kusababisha kutokufahamika kwa nyaraka halisi zinazokusudiwa<br><br>10. **Kanuni ya 33(2)** inazungumzia kuhusu maombi ya kibali cha unyunyiziaji wa viautilifu kwa njia ya anga, kuwa maombi hayo yanapaswa kuambatishwa na nyaraka zilizoainishwa katika katika aya (a) hadi (e).<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Aya (e) inaweka sharti la kupata kibali cha kifaa anga cha unyunyiziaji kutoka kwa Mamlaka. Aya | 10. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kuzitaja bayana Mamlaka ya Usafiri wa Anga na Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | hii haifafanui ni mamlaka ipi inayokusidiwa kutoa kibali hicho. Hali inasababisha kutokuelewaka kwa sharti hilo. | |
| | | | | | 11. **Kanuni ya 51(2)** inaainisha la vipimo vya sehemu ya kuhifadhia viuatilifu kwa upana na urefu.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni haianishi vipimo vipimo vya urefu (*height*) vya sehemu ya kuhifadhia viauatilifu. Kutokuwekwa kwa vipimo vya urefu kunaweza kuleta changamoto ya utekelezaji wa | 11. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuweka sharti la vipimo vya urefu (*height*) vya sehemu ya kuhifadhia viauatilifu. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | masharti ya Kanuni hivyo kuleta usumbufu kwa wanaoguswa na Kanuni hizi. | |
| | | | | | 12. **Kanuni ya 55 (3) (a) (b)** ina makosa ya kiuandishi.<br><br>**Tatizo**<br>Kanuni imetumia neno "*save*" badala ya neno "*serve*". | 12. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuondoa makosa ya kiuandishi. |
| | | | | | 13. **Kanuni ya 95(1)** na **Kanuni ya 97(2)** zinarejea majedwali la hamsini na moja pamoja na hamsini na saba.<br><br>**Tatizo**<br>Majedwali yanayorejewa na | 13. Kanuni zifanyiwe marekebisho ili kurejea Majedwali sahihi. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Kanuni hizi hayapo katika Kanuni hizi<br><br>14. **Kanuni ya 117 (1)** inayohusu haki ya kukata rufaa kwa mtu ambaye hajaridhika na uamuzi wa mamlaka, inamtaka mtu huyo kukata rufaa kwa maandishi kwa Waziri ndani ya siku 30.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni haijitoshelezi kwa ufafanuzi wa hesabu ya siku thelathini za rufaa. Hali hii inaweza kusababisha kutokueleweka vizuri kwa haki ya kukata rufaa. | 14. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kuonesha kuwa siku thelathini zitahesabika kuanzia tarehe ya kupokea nakala ya uamuzi. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 15. **Kanuni ya 114(d)** imempa Waziri mamlaka ya kumsimamisha kazi mkaguzi kwasababu ambazo Waziri anaamini kwamba zinasababisha Mkaguzi kushindwa kutekeleza kazi zake.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni zimempa Waziri kuamua kwa utashi wake, hali inayoweza kusababisha matumizi mabaya ya mamlaka hayo.<br><br>16. **Kanuni ya 117 (5)** inaeleza kuhusu uamuzi unaoweza kutolewa na Mamlaka ya Afya ya | 15. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kufuta Kanuni ya 114(d)<br><br>16. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kufuta neno "*Authority*" na |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Mimea na Viuatilifu Tanzania baada ya kusikiliza rufaa.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni inaitaja Mamlaka kuwa ndio itatoa uamuzi wa rufaa ilhali mamlaka ndio mlalamikiwa. Hali hii ni kinyume na inayowekwa katika misingi ya haki ya asili, inayokataza mtu kuamua shauri ambalo yeye ni sehemu ya shauri hilo. | kuweka neno "*Minister*" |
| 2. | **(TS Na. 288)**<br><br>7 Aprili, 2023 | Kanuni za Egonomia,2023 (Zimetungwa chini ya kifungu cha 109) | Sheria ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi, (Sura ya 297) | Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) | 1. **Kanuni ya 5** inahusu wajibu wa wanaoweza kukumbwa na visababishi hatari za egonomia. Ambapo | 1. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kumjumuisha mtu yeyote anayeweza kukumbwa na |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | kanuni hii pia inaweka wajibu kwa muajiriwa.<br><br>**Tatizo**<br>Kuwekwa kwa wajibu wa mwajiriwa ni kinyume na **Kanuni ya 3** inayohusu wigo wa matumizi wa kanuni hizi. Hali hii inaweza kuathiri utekelezaji bora wa sheria mama.<br><br>2. **Kanuni ya 7(1)** inahusu tathmini ya athari za egonomia.<br><br>**Tatizo**<br>Kanuni imetumia “Mamlaka” pasipo kuweka tafsiri yake. Hali hiyo inasababisha | visababishi hatari vya egonomia.<br><br>2. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuweka tafsiri ya neno “Mamlaka” |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | kutokukamilika kwa ufafanuzi unaotarajiwa kutolewa na Kanuni hizi.<br><br>3. **Kanuni ya 11** inazungumzia kuhusu utunzaji wa kumbukumbu. Kanuni ya 11(b) inarejea Kanuni ya 11(1) (c).<br><br>**Tatizo**<br>Kanuni ya 11(1) (c) inayorejewa haipo katika Kanuni hizi. Hali hii inaleta mkanganyiko wakati wa usomaji wa Kanuni hizi. | 3. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kurejea kuweka rejea sahihi. |
| 3. | **(TS Na. 289)**<br><br>7 Aprili, 2023 | Kanuni za Mazingira ya kazi,2023 | Sheria ya Afya na Usalama Mahali Pa Kazi, | Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na | 1. **Kanuni ya 4(1)** inarejea Kanuni ya 4(2) kwa kuitaja yote. | 1. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (Zimetungwa chini ya kifungu cha 109) | (Sura ya 297) | Wenye Ulemavu) | **<u>Tatizo</u>**<br>Maudhui ya Kanuni ya 4(1) yanajirudia katika Kanuni ya 4(2)<br><br>2. **Kanuni ya 4(2)** inaweka sharti kwa mwajiri kutomruhusu mfanyakazi kufanya kazi katika mazingira ya jokofu ambapo kipimo cha hali ya joto ya balbu kavu iko chini ya nyuzi joto 0.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni haijataja iwapo kipimo cha nyuzi joto kilichokusudiwa ni nyuzi joto sifuri sentigredi au nyuzi joto farenheiti | kuondoa maudhui yanayojirudia.<br><br>2. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuonesha kipimo kinachokusudiwa ni sentigredi |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 3. **Kanuni ya 9** inahusu kiwango cha kelele kinachohitajika mahala pa kazi kuwa ni 85 dB (A).<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kipimo cha kelele kwa kina makosa ya aundishi kwa kuweka mabano katika herufi A. | 3. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuandika Kanuni kwa usahihi |
| 4. | **(TS Na. 327)**<br><br>5 Mei 2023 | *The Merchant Shipping (Medical Examinations) Regulations, 2023* (Zimetungwa chini ya Kifungu cha 157) | *The Merchant Shipping Act, (Cap. 165)* | Wizara ya Uchukuzi | 1. **Kanuni ya 5 (c)** inaweka sababu ya kufutwa ama kusitishwa kwa uteuzi pale ambapo kwa maoni ya TASAC na mazingira yanalazimu kusitisha au kufuta uteuzi.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Hali hiyo: - | 1. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kuifuta Kanuni ya 5(c) |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | a) Ni kinyume na misingi ya uandishi wa Kanuni, ambazo zinapaswa kutoa ufafanuzi zaidi wa masharti yaliyowekwa na Sheria Mama.<br><br>b) Inaweza kusababisha matumizi mabaya ya Madaraka yaliyotolewa na Kanuni hizo<br><br>2. **Kanuni ya 21** inaweka utaratibu wa kushughulikia malalamiko ya baharia ama nahodha ambaye hajaridhishwa na uamuzi, ambapo | 2. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuonesha hatua inayoweza kufuatwa na mtu ambaye hajaridhishwa na |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | anaweza kuiomba TASAC ifanye mapitio ya uamuzi uliotolewa dhidi yake.<br>**Kanuni ya 21 (3)** inaweka utaratibu wa TASAC ili kushughulikia malalamiko na kufikisha uamuzi wake kwa mlalamikaji ndani ya siku 14 tangu muda mabao malalamiko yalipokelewa.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni hailezi hatua inayoweza kufuatwa na mtu ambaye hajaridhishwa na uamuzi wa baada ya mapitio.<br>Hali ni inaweza sababisha | uamuzi wa baada ya mapitio. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | mkanganyiko kuhusu inayostahili kufuatwa baada ya uamuzi wa mapitio. | |
| 5. | **(TS Na. 349)**<br><br>12 Mei 2023 | Kanuni Za Ukusanyaji Na Uchakataji Wa Taarifa Binafsi,2023<br><br>(Zimetungwa chini ya kifungu cha 64) | Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi,<br><br>(Sheria Na. 11 ya 2022) | Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari | 1. **Kanuni ya 4(3)(c)** inataja moja ya sharti la kuzingatiwa wakati wa kuchakata maombi ya usajili wa ukusanyaji na uchakataji wa Taarifa binafsi<br><br>**Tatizo**<br>Kanuni ya 4(3) (c) inataja sharti la kuwasilisha nyaraka nyingine yoyote kama Tume itakavyohitaji wakati kuomba usajili wa ukusanyaji na uchakataji wa Taarifa binafsi. | 1. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuondoa sharti la Tume kuhitaji nyaraka nyingine yoyote. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 2. **Kanuni ya 9(2) (e)** inataja moja ya Taarifa za wakusanyaji na wachakataji zitazohifadhiwa katika rejista.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>**Kanuni ya 9(2) (e)** inataja taarifa nyingine yoyote kama Tume itakavyoelekeza. Sharti hilo: -<br>a) linasababisha kutotabalika taarifa zinazohitajika; na<br><br>b) linaondoa mantiki ya sheria ndogo kutoa ufafanuzi unaojitosheleza | 2. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuondoa sharti la Tume kuhitaji taarifa nyingine yoyote. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | kuhusu masharti ya sheria mama<br><br>3. **Kanuni ya 11** inaipa nguvu Tume ya kumruhusu mtu yeyote kupekua na kupakua Taarifa yoyote ilioingizwa katika rejesta.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Sharti lililowekwa na Kanuni hiyo linafifisha lengo kuu la sheria Mama ambalo ni kuimarisha ulinzi wa Taarifa binafsi zinazochakatwa na vyomba vya Serikali na vyombo binafsi.<br><br>4. **Kanuni ya 20 (2)** inahusu maombi ya kibali cha kusafirisha | <br><br><br>3. Kanuni ya 11 ifanyiwe marekebisho kwa kuondoa ruhusa kwa mtu yoyote kupekua na kupakua Taarifa yoyote ilioingizwa katika rejesta.<br><br><br><br><br><br><br><br><br><br><br>4. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuondoa sharti la |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | taarifa binafsi nje ya nchi.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>**Kanuni ya 20(2)(i)** inaweka kigezo kwa muomba kibali kuwasilisha taarifa nyingine yoyote kama itakavyohitajika na Tume. Sharti hilo: -<br>a) linasababisha kutotabalika taarifa zinazohitajika; na<br><br>b) linaondoa mantiki ya sheria ndogo kutoa ufafanuzi unaojitosheleza kuhusu masharti ya sheria mama. | Tume kuhitaji taarifa nyingine yoyote. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 5. **Kanuni ya 21** inahusu sababu za Tume kukataa maombi ya kusafirisha Taarifa binafsi nje ya nchi.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>**Kanuni ya 21(e)** inatoa mamlaka kwa Tume kukataa maombi kutokana na sababu nyingine yoyote ambayo itaona inaafa.<br>Sharti hilo: -<br>a) Linasababisha kutotabalika kwa sababu zinazoweza kusababisha Tume kukataa maombi;<br><br>b) linaondoa mantiki ya sheria ndogo | 5. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuondoa sharti la Tume kutumia sababu nyingine yoyote wakati wa kukataa maombi kusafirisha taarifa binafsi nje ya nchi. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | kutoa ufafanuzi unaojitosheleza kuhusu masharti ya sheria mama; na<br><br>c) Linaweza kusababisha kutumika kwa utashi binafsi wakati kukataa maombi ya kusafirisha taarifa binafsi nje ya nchi.<br><br>6. **Kanuni ya 27** inaweka msingi wa mambo muhimu ya kuzingatiwa na mkusanyaji ama mchakataji wa Taarifa Binafsi. Sehemu (i) inaweka msingi wa kulinda taarifa binafsi nyeti | 6. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuweka sharti la lazima la kuhifadhi taarifa binafsi nyeti tofauti na taarifa binafsi za aina nyingine. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | kwa hatua za kutosha na ikiwezekana kuhifadhi taarifa hizo tofauti na zinapohifahdhiwa taarifa binafsi nyingine.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni haijaweka sharti la lazima la kuhifadhi taarifa binafsi nyeti tofauti na taarifa binafsi za aina nyingine.<br>Hali hii inaweza kufifisha lengo lililowekwa na Sheria mama katika ulinzi wa taarifa binafsi. | |
| 6. | **(TS Na. 350)**<br><br>12 Mei 2023 | Kanuni za Taratibu za Kushughulikia Malalamiko ya | Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, | Wizara ya Habari, Mawasiliano | 1. **Kanuni ya 4(3)** inaelezea utaratibu wa kuwasilisha malalamiko ya mtu | 1. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kuweka utaratibu wa kuwasilisha |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ukiukwaji wa Misingi ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, 2023<br><br>(Zimetungwa chini ya Kifungu cha 64) | (Sheria Na. 11 ya 2022) | na Teknolojia ya Habari | au kikundi kuhusu ukiukaji wa ulinzi wa Taarifa binafsi au kutoridhishwa na uamuzi wa mkusanyaji au mchakataji kuhusiana na taarifa binafsi.<br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni imetambua utaratibu wa kupokea malalamiko ya kikundi ilhali Kanuni hazitambui malalamiko ya kikundi.<br><br>2. **Kanuni ya 4(5)** inazungumzia utaratibu wa Tume kupitia malalamiko ili kujiridhisha usahihi wake na uzingatiaji wa sheria ili Tume | malalamiko ya kikundi<br><br>2. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuonesha muda ambao Tume itatumia kujiridhisha na usahihi wa |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | iweze amua kuruhusu kupokea malalamiko ama vinginevyo.<br><br>**<u>Tatizo la kwanza</u>**<br>Kanuni haioneshi muda ambao Tume itatumia kujiridhisha na usahihi wa malalamiko tangu kuyapokea.<br>Hali hii inaweza kuleta changamoto ya ucheleweshaji wa Haki ya mlalamikaji na kuendeleza madhara anayoyalalamikia<br><br>**<u>Tatizo la Pili</u>**<br>Kanuni hazioneshi muda ambao malalamikaji atapaswa kuwa amefikisha | malalamiko tangu kuyapokea. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | malalamiko yake kwa Tume tangu muda ambao uamuzi wa mtunza taarifa ama mchakata taarifa unaolalamikiwa umetokea.<br>Hali hii ni kinyume na kanuni za upatikanai wa haki na uchakataji wa malalamiko.<br><br>3. **Kanuni ya 5(1) (b)** inaeleza sababu ya kukata lalamiko kutokana na muda wa kuwasilisha kuwa umepita.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni haijabainisha muda wa kuwasilisha malalamiko. | 3. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuonesha muda wa kuwasilisha malalamiko |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 4. **Kanuni ya 8** inamtaka mlalamikaji kuandaa na kuwasilisha kwa Tume majibu dhidi ya Utetezi wa mlalamikiwa ndani ya muda uliotolewa baada ya kupokea utetezi.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni haioneshi muda ambao mlalamikaji atapewa ili kuandaa majibu dhidi ya utetezi wa mlalamikiwa.<br>Hali hii inaweza kurefusha muda wa uchakataji wa malalamiko hivyo, kuathiri upatikanaji wa haki kwa wakati. | 4. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kuweka muda ambao mlalamikaji atapaswa kutumia kuandaa majibu dhidi ya utetezi wa malalamikiwa. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 5. **Kanuni ya 12 (3)** inazungumzia utaratibu wa kufuatwa mara baada mlalamikaji au mlalamikiwa kuruhusiwa kufanya marekebisho ya malalamiko, utetezi au majibu.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni haioneshi muda ambao Tume itampa mwombaji wa kibali kufanya marekebisho yanayohusika, jambo linaloweza kusababisha: -<br>a) Mhusika kutumia muda mrefu kufanya marekebisho na kuchelewesha | 5. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kuweka muda mahsusi atakaopewa muombaji kwa ajili ya kufanya marekebisho. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | haki kwa upande mwingine;<br><br>b) Kukosekana kwa mwongozo kuhusu muda wa kufanya marekebisho na kuathiri uthabiti wa kushugulikia malalamiko; na<br><br>c) Kutotimia kwa dhima ya sheria ndogo kukamilisha ufafanuzi wa dhamira ya sheria mama.<br><br>6. **Kanuni ya 13(1)** inahusu uchunguzi wa malalamiko | 6. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kukamilisha maudhui yaliyokusudiwa |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | **<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni haijakamilika kimaudhui, hivyo kusababisha kutofikiwa kwa lengo lililokusudiwa na Kanuni. | |
| 7. | **(TS Na. 381)**<br><br>2 Juni 2023 | *The Tanzania Shipping Agencies (Cargo Security and Safety of Terminal Operations) Regulations, 2023* (Zimetungwa chini ya Kifungu cha 61(2)(g) and (j)) | *The Tanzania Shipping Agencies Act, (Cap. 415)* | Wizara ya Uchukuzi | 1. **Kanuni ya 3** inaweka tafsiri ya maneno mbalimbali yaliyotumika katika Kanuni hizi.<br><br>**<u>Tatizo la Kwanza</u>**<br>Kanuni haijaweka tafsiri ya maneno kama vile *regulator*, *competent* na director general ambayo yametumika katika maeneo mbalimbali ndani ya Kanuni kama vile Kanuni ya 5(2), 12, 15(2), 51(4). | 1. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuweka tafsiri ya maneno “regulator, “competent” na “director general” |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 2. **Kanuni 5** inahusu mamlaka ya msimamizi kuruhusu au kutoruhusu mtu au mzigo kuingia au kutoka katika eneo la bandari.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni haijabainisha sababu zinazoweza kusababisha mtu au mzigo kukataliwa kuingia au kutoka, badala yake Kanuni imeruhusu utashi binafsi kwa msimamizi kuweka sababu yoyote atakayoona inafaa. | 2. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuonesha sababu zinazoweza kusababisha mtu au mzigo kukataliwa kuingia au kutoka bandarini. |
| | | | | | 3. **Kanuni ya 20** inaweka wajibu kwa msimamizi kuhakikisha watu | 3. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kufuta kanuni ya 20(1)(d) |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | wantembea katika eneno la bandari wanavaa vifaa vya usalama.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni ya 20(1) (b) (d) inawasilisha ujumbe mmoja, ambapo (b) tayari imetaja matumizi ya viatu salama ambavyo si vile vinavyotajwa katika aya (d).<br><br>4. **Kanuni 23 (1) (b)** msimamizi atahakikisha kuwa vifaa vya kuzimia moto haviondolewi katika maeneo yake isipokuwa vitakapokuwa vikitumika wakati wa | 4. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kuweka sharti la kuweka vifaa mbadala wakati vifaa vimeondolewa kwa ajili ya matengenezo. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | matumizi yake, wakati wa majaribio au wakati wa matenegezo.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni haizioneshi sharti la kuweka vifaa mbadala wakati vifaa vimeondolewa kwa ajili ya matengenezo.<br><br>5. **Kanuni ya 23 (4)** inaweka sharti kwamba, vali zuizi (block valves) zinapaswa kuwa wazi muda wote.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Masharti yaliyowekwa na Kanuni ya 23 (4) hayana uhalisia | <br><br><br><br><br><br><br><br><br><br><br>5. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kufuta maneno "*kept open*" na badala yake kuweka maneno "*accessible and readly available for use*" |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 6. **Kanuni ya 35** inampa wajibu msimamizi kuhakikisha miundombinu ipo katika ubora na mazingira mazuri.<br><br>**Tatizo**<br>Kanuni ina makosa ya uandishi kwa kufanya rejea ya Kanuni ya 35, hali hiyo inaleta changamoto ya usomaji wa kanuni. | 6. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kurejea Kanuni ya 33 na 34 ili kuondoa makosa ya kiuandishi |
| | | | | | 7. **Kanuni ya 55 (3)** inamtaka msimamizi pale inapotokea upotevu wa mizigo na kutoa taarifa, kutoa taarifa kwa shirika na kufanya uchunguzi wa awali | 7. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuonesha kuwa unaokusudiwa ni uchunguzi wa awali. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | na kutoa taarifa ya uchunguzi.<br><br>**Tatizo**<br>Kanuni inaweka sharti kwa msimamizi kutoa taarifa ya uchunguzi badala ya kutoa taarifa ya uchunguzi wa awali.<br><br>8. Kanuni ina makosa ya uandishi wa namba za vifungu, ambapo imeruka Kanuni ya 58.<br><br>**Tatizo**<br>Kurukwa kwa Kanuni hiyo kunaweza kuwa ni: -<br>a) makosa ya kiuandishi; au | 8. Kanuni ifanyiwe mareklbisho kwa kuweka mpangilio sahihi wa namba za vifungu. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | b) Kutokuwekwa kwa Kanuni iliyokusudiwa.<br><br>Mambo hayo yanaweza weza kusababisha kutokutimia kwa malengo yaliyokusudiwa. | |
| | | | | | 9. **Kanuni ya 57** inaweka adhabu ya jumla pale ambapo hakuna adhabu iliyotamkwa kwa kuvunja masharti yaliyopo katika Kanuni, kuwa ni adhabu ya faini isiyopungua shilingi milioni mbili na isiyozidi shilingi milioni ishirini ama kifungo kisichopungua | 9. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuendana na masharti ya adhabu yanyowekwa na kifungu cha 56 cha sheria mama. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | mwaka mmoja na kisichozidi miaka mitano ama adhabu zote kwa pamoja.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Adhabu ya jumla inayotamkwa na kanuni hii ni kinyume na adhabu iliyowekwa na sheria mama chini ya kifungu cha 56 kinachoweka adhabu ya jumla kwa makosa ambayo hayajawekewa adhabu. Kifungu hiko kinataja adhabu ya faini isiyopungua shilingi za kitanzania milioni ishirini na isiyozidi shilingi milioni | |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | arobaini au kifungo kisichopungua miaka miwili na kisichozidi miaka mitano ama adhabu zote kwa pamoja.<br>Hali hiyo inasababisha mashaka kuhusu kuzingatiwa kwa masharti ya kifungu cha 36 (6) cha sheria ya tafsiri ya sheria kuhusu masharti ya kuweka adhabu katika sheria ndogo. | |
| 8. | **(TS Na. 382)**<br><br>2 Juni 2023 | *The Tanzania Shipping Agencies (Shippers Registration) Regulations, 2023* (Zimetungwa chini ya Kifungu | *Tanzania Shipping Agencies Act (Cap. 415)* | Wizara ya Uchukuzi | 1. **Kanuni ya 6(2)** inaipa TASAC sharti la hiari ya kutoa cheti cha usajili kwa muombaji aliyetimiza masharti yaliyowekwa kwa mujibu wa sheria. | 1. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuweka sharti la lazima kwa TASAC ili kumpatia cheti muombaji aliyetimiza masharti. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | cha 12(1)(k) and 61) | | | **Tatizo**<br>Kanuni imeweka sharti la hiari kwa TASAC kumpatia cheti muombaji aliyetimiza masharti, badala ya kuweka sharti la lazima<br><br>2. **Kanuni ya 11 (1) (b)** inamtaka muombaji wa nakala rudufu ya cheti kilichopotea ama kuharibiwa, kuambatisha maombi yake na hati uthibitisho wa polisi ya upotevu na nyaraka nyingine yoyote kama itakavyohitajika na Shirika. | 2. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuondoa maneno "nyaraka nyingine yoyote kama itakavyohitajika na TASAC" |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | **<u>Tatizo</u>**<br>**Kanuni ya 11 (b)** inalipa Shirika nguvu ya kutaka nyaraka nyingine yoyote bila kutaja nyaraka hizo. Hali hii inaweza kusababisha kutokufahamika kwa nyaraka halisi zinazokusudiwa.<br><br>3. **Kanuni ya 19 (3)** inaoesha masauala ambayo yatazingatiwa ili kuonesha kwamba, notisi imefikishwa kwa mlengwa.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni ina makosa ya uandishi kwa kurejea i aya (a) na (b) mara mbili. Hali | 3. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuweka mpangilio wa vifungu. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | hiyo inaleta changamoto ya usomaji na namna ya kufanya rejea.<br><br>4. Kanuni imerejea kuanzishwa chini ya **kifungu cha 12 (1) (k) na 61**.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>**Kifungu cha 12 (1) (k)** kilichorejewa hakihusiani na mamlaka ya Waziri kutunga Kanuni. Hali hii inakanganya chimbuko la mamlaka ya kutungwa kwa kanuni hizi.<br><br>5. Kanuni zina makosa ya uandishi katika | 4. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuondoa Kanuni ya 12(1) (k) ambayo haihusiani na mamlaka ya Waziri ya kutunga Kanuni.<br><br>5. Kanuni ifanyiwe marekbisho kwa kuweka mpangilio |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | mpangilio wa vifungu.<br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni ya 4 imetokea mara mbili ikiwa na maudhui yanayotofautiana. Athari yake ni: -<br>a) Inaleta mkanganyiko katika rejea ya Kanuni; na<br>b) Inatatiza ufafanuzi wa masharti ya sheria mama. | sahihi wa namba za vifungu. |
| | | | | | 6. **Kanuni ya 4 (2)** inataja matakwa ya kuzingatiwa wakati wa kuomba usajili wa wasafirishaji kwa njia ya maji. **Kanuni ya 4(2) (a) (iv)** inataja nyaraka zingine | 6. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuondoa uwezo wa TASAC kutaka nyaraka nyingine yoyote. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | zozote kama zitavyohitajika na TASAC.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>**Kanuni ya 4 (2) (a) (iv)** inaipa TASAC nguvu ya kutaka nyaraka nyingine yoyote bila kutaja nyaraka hizo.<br>Hali hii inaweza kusababisha kutokufahamika kwa nyaraka halisi zinazokusudiwa.<br><br>7. **Kanuni ya 4 (2) (b) (iv)** inazungumzia vigezo vya usajili wa wasafirishaji kwa njia ya Maji kwa upande wa Taasisi na Mtu binafsi. | <br><br><br><br><br><br><br><br><br><br><br><br><br><br>7. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuondoa uwezo wa TASAC kutaka nyaraka nyingine yoyote. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | **<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni haitaji nyaraka zilizokusudiwa.<br>Hali hii inaweza kusababisha kutokufahamika kwa nyaraka halisi zinazokusudiwa<br><br>8. **Kanuni ya 6 (3)** inazungumzia utaratibu wa TASAC kutoa notisi iwapo imekataa maombi ya usajili.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni haioneshi muda mahsusi ambao Notisi itapaswa kutolewa tangu TASAC | 8. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuonesha muda mahsusi ambao Notisi itapaswa kutolewa tangu TASAC kupokea maombi ya usajili. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | kupokea maombi hayo.<br>Hali hii:-<br>a) Inaweka utata kuhusu muda wa kusubiria notisi;<br>b) Inaikosesha TASAC mwongozo kuhusu muda wa kutoa notisi.<br><br>9. **Kanuni ya 16 (2)** inaweka adhabu ya faini isiyopungua shilingi laki mbili na elfu hamsini na isiyozidi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi sita na kisichozidi mwaka mmoja au adhabu zote kwa pamoja. | 9. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuendana na adhabu zilizowekwa kwatika sheria mama. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | **Tatizo**<br>Adhabu hiyo imevuka ukomo wa sheria za nchi.<br>Hali hiyo inasababisha mashaka kuhusu kuzingatiwa kwa masharti ya kifungu cha 36 (6) cha sheria ya tafsiri ya sheria kuhusu masharti ya kuweka adhabu katika sheria ndogo. | |
| | | | | | 10. Kanuni ina Majedwali saba yanayotoa ufafanuzi wa Kanuni mbalimbali<br><br>**Tatizo**<br>Majedwali yana makosa ya uandishi kwa kurejea Kanuni | 10. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kurejea kanuni sahihi zinazoanzisha majedwali. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | zinazoyaanzisha ambazo si sahihi | |
| 9. | **(TS Na. 384 la 2023)**<br><br>2 Juni 2023 | Kanuni za Usajili wa Wasafirishaji kwa njia ya Maji, 2023 | Sheria ya Uwakala Wa Meli Tanzania (Sura 415) | Wizara ya Uchukuzi | **Kanuni ya 12** inaweka utaratibu wa Msafirishaji kuomba nakala iliyodurufiwa ya Cheti chake alichopoteza. Kanuni ya 12 (b) inamtaka muombaji kuambatisha maombi hayo pamoja na nakala ya taarifa ya upotevu na nayaraka nyingine yoyote kama itakavyohitajika na TASAC.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni haitaji nyaraka zilizokusudiwa.<br>Hali hii inaweza kusababisha kutokufahamika kwa nyaraka halisi zinazokusudiwa | Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuondoa sharti la TASAC kuomba nyaraka nyingine yoyote. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 10. | **(TS Na. 387)**<br><br>2 Juni 2023 | Kanuni za Ulinzi wa Mizigo na Usalama Katika Utendaji Kazi wa Bandari na Bandari Kavu, 2023<br><br>(Zimetungwa chini ya kifungu cha 5 (b), (c), (d) na 61(2) (g), ( j)) | Sheria ya Uwakala Wa Meli Tanzania (Sura 415) | Wizara ya Uchukuzi | 1. Kanuni imetumia neno "bila kujali" katika maeneo mbalimbali.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Matumizi ya neno bila kujali yanaondoa maana iliyokusudiwa katika masharti yaliyowekwa na sheria ndogo.<br><br>2. **Kanuni ya 12** inazungumzia mizigo iliyopigwa marufuku bandarini na inaelezewa kuanzia sehemu (a) mpaka sehemu (d). Sehemu (a) inazungumzia mzigo usioruhusiwa iwapo umeshambuliwa, | 1. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kufuta maneno "bila kujali" na badala yake kuweka maneno "bila kuathiri"<br><br>2. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuondoa dosari ya kiuandishi |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | wenye sumu kali, kuoza au kuharibiwa na ukungu na hauwezi kuharibika ukiwa ndani ya bandari au bandari kavu.<br><br>**<u>Tatizo la Kwanza</u>**<br>Tatizo la kimaandishi baada ya kutumia neno “unaweza kuharibika’’ imeandikwa ‘’hauwezi kuharibika’’ hali hii inaweza kuathiri lengo lililokusudiwa na sheria mama.<br><br>**<u>Tatizo la Pili</u>**<br>Kanuni imetua neno umeshambuliwa pasipo kulifafanu. Hali hiyo inaleta | |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | mkanganyiko wa maana iliyokusudiwa.<br><br>3. **Kanuni ya 14 (4)** inaelekeza utaratibu wa namna ya kushusha na mizigo hatarishi katika bandarini.<br><br>**Tatizo**<br>Kanuni zimetaja lori kama chombo cha kupokea mzigo hatarishi kutoka katika meli. Hii inasababisha kutokutambulika kwa vyombo vingine vinavyotumika kupakia mizigo bandarini | <br><br><br><br>3. Kanuni ya 14(4) ifanyiwe marekebisho ili kuongeza vyombo vingine vya usafirishaji. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 4. **Kanuni ya 53 (2)** inahusu mafunzo ya rejea na endelevu kwa afisa ulinzi<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni haijafafanua kwamba mafunzo yatakayotolewa yatahusiana na fani inayohusika. | 4. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuonesha mafunzo yatakayotolewa yatahusiana na fani inayohusika |
| 11. | **(TS Na. 426)**<br><br>30 Juni 2023 | *The Water Supply and Sanitation (Commercial and Community Boreholes Operations) Rules, 2023*<br><br>(Zimetungwa chini ya Kifungu cha 29(1) (m)) | *The Water Supply and Sanitation Act, (Cap. 272)* | Wizara ya Maji | Kanuni inahusu watoa huduma ya usambazaji wa maji kibiashara na kijamii.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni zimeweka vifungu mbalimbali vya namna ya kushughulikia malalamiko pasipo kuirejea Kanuni za kushughulikia malalamiko ya Wateja, 2020, kuwa ndio | Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kurejea Kanuni hizo. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | itatumika pale kunapotokea malalamiko katika huduma inayodhibitiwa. | |
| 12. | **(TS Na. 452)**<br><br>7 Julai 2023 | Kanuni za Shughuli za Uzalishaji, Upelekaji na Usambazaji Umeme, 2023<br><br>(Zimetengenezwa chini ya vifungu vya 14(5), 22(1) na 45) | Sheria ya Umeme, (Sura ya 131) | Wizara ya Nishati | 1. Kanuni imetumia neno “bila kujali” katika maeneo mbalimbali.<br><br>**Tatizo**<br>Matumizi ya neno bila kujali yanaondoa maana iliyokusudiwa katika masharti yaliyowekwa na sheria ndogo.<br><br>2. **Kanuni ya 2(b)** inayohusu matumizi ya Kanuni.<br><br>**Tatizo**<br>Kanuni ina makosa ya kiuandishi kwa | 1. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kufuta maneno “bila kujali” na badala kuweka maneno “bila kuathiri”<br><br>2. Kanuni ifanyiwe marekebisho ya kiuandishi kwa kuongeza aya (c) iliyokosekana |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | kukosa ukamilifu, hali inayosababisha kutokufikia lengo lililokusudiwa.<br><br>3. **Kanuni ya 3** inatoa tafsiri ya maneno mbalimbali.<br><br>**Tatizo**<br>Kanuni ina makosa ya kiuandishi kwa kutofuata mpangilio wa maneno katika mtiririko wa kialfabeti.<br><br>4. Kanuni inatajwa kuanzishwa chini ya **kifungu cha 14 (5), kifungu cha 22 (1)** na **kifungu cha 45** cha sheria mama. | 3. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuweka maneno yaliyo katika tafsiri kwenye mpangilio wa kialfabeti.<br><br>4. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kufuta rejea ya **Kanuni ya14(5)** |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | **<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni inataja cha Kifungu cha **14(5)** kama vifungu anzishi. Vifungu hivyo hakihusiani na uanzishaji wa Kanuni hizi.<br>Hali hii ni kinyume na matakwa ya sheria ya tafsiri ya sheria Sura ya 1. | |
| | | | | | 5. **Kanuni ya 5** inaweka utaratibu wa kuomba leseni pamoja na nyaraka muhimu kama zinavyoorodheshwa katika sehemu (a) mpaka (f).<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Sehemu ya (f) ya kanuni hii inaweka | 5. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuweka sharti la kuomba nyaraka zinazohusu shughuli zinazosimamiwa na EWURA |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | takwa la Taarifa yeyote kama itakavyohitajika na mamlaka.<br>Hali hii inaweza kuleta usumbufu usio wa lazima kwa waombaji hivyo kufifisha lengo la sheria mama.<br><br>6. **Kanuni ya 5(2) (b)** inahusu utaratibu wa kuomba leseni ya upelekaji umeme.<br><br>**Tatizo**<br>Kanuni ya 5(2) (b) (v) ina makosa ya kiuandishi kwa kukosa ukamilifu, hali inayosababisha kutokufikia lengo lililokusudiwa. | 6. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuondoa kasoro za uandishi ya mpangilo wa Kanuni |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 7. **Kanuni ya 5(2) (c)** (ix) inahusu ripoti ya utendaji kazi.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni ina makosa ya uandishi wa namba kuanzia namba (ix)<br><br>8. **Kanuni ya 7(5)** inahusu maombi ya kuomba upya au kuongezewa muda wa leseni.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni inaweka sharti la kutaka nyaraka nyingine yoyote bila kutaja nyaraka hizo.<br>Hali hii inaweza kusababisha kutokufahamika kwa | 7. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuondoa makosa ya uandishi ya mpangilio wa namba za Kanuni<br><br>8. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuweka sharti la kuomba nyaraka zinazohusu shughuli zinazosimamiwa na EWURA |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | nyaraka halisi zinazokusudiwa. | |
| | | | | | 9. **Kanuni ya 10(3)** inahusu maombi ya kuomba upya au kuongezewa muda wa leseni ya muda.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni inaweka sharti la kutaka nyaraka nyingine yoyote bila kutaja nyaraka hizo.<br>Hali hii inaweza kusababisha kutokufahamika kwa nyaraka halisi zinazokusudiwa | 9. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuweka sharti la kuomba nyaraka zinazohusu shughuli zinazosimamiwa na EWURA |
| | | | | | 10. **Sehemu ya Nne** inahusu masharti ya Fedha | 10. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuondoa dosari ya kiuandishi |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | **Tatizo**<br>Sehemu ya Nne ina makosa ya kiundishi kwa kuandika neno "mashaeti" badala ya neno "masharti"<br><br>11. **Kanuni ya 14** inaweka wajibu kwa mamalaka kumjulisha muombaji kuhusu uamuzi wake kwa maandishi.<br><br>**Tatizo**<br>Kanuni haioneshi muda ambao mamlaka itapaswa kutoa sababu za maamuzi yake dhidi ya ombi la muombaji. Hali hii ni kunyume na misingi ya utoaji haki. | 11. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuweka ukomo wa muda wa siku kumi na nne ambazo Mamlaka itapaswa kumjulisha mwombaji kuhusu uamuzi wake. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 12. **Kanuni ya 17** inazungumzia uwezo wa mamlaka kusimamisha na kufuta leseni. Kanuni ndogo ya (3) (b) inaipa uwezo wa mamlaka mara baada ya kufuta leseni kuweza kuteua msuluhishi kulingana na miongozo pamoja na kuanza kushughulikia mambo yake katika kipindi ambacho itakiona kinafaa.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni zimeipa mamlaka EWURA kuteua msuluhishi | 12. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kufuta neno msuluhishi na badala yake kuandika neno "msimamizi" lilokusudiwa. Pia Kanuni iweke tafsiri ya msimamizi, kuonesha sifa za uteuzi, majukumu yake, namna ya uendeshaji wa shughuli zake. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 13. **Kanuni ya 32 (a)** inahusu kukataza ruzuku kati ya shughuli zinazodhibitiwa.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Masharti yaliyowekwa hayazingatii uhalisia kwa kuwa zipo shughuli zenye ruzuku ambazo ni sehemu ya shughuli zinazodhibitiwa.<br><br>14. **Kanuni ya 35** inahusu notisi ya kuingilia huduma.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni ina makosa ya uandishi kwa kuonesha mida miwili tofauti ya | 13. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kutambua shughuli zilizo na ruzuku ambazo zinadhibitiwa na EWURA<br><br>14. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kukiandika upya Kanuni ili kutofautisha muda unaokusudiwa. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | utoaji wa notisi, ambapo muda wa kwanza ni saa ishirini na nne na muda wa pili ni siku saba. Hali hii inasababisha kutokueleweka kwa muda uliokusudiwa hivyo kuathiri utekelezaji wake.<br><br>15. **Kanuni ya 48 (1)** inahusu kuwasilisha taarifakwa mwendesha mfumo na soko la umeme<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni ina makosa ya kiuandishi kwa kujirejea yenyewe | <br><br><br><br><br>15. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuondoa kasoro ya Kanuni kujirejea yenyewe |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 16. **Kanuni ya 79(2)** inaweka utaratibu wa kutoa taarifa kwa maandishi kwa mtu ambaye hajaridhishwa na matendo ya mwalikishi wa Mamlaka wakati wa ukaguzi<br><br>**Tatizo**<br>Kanuni haijaonesha mfano wa fomu itayotumika kuwasilisha malalamiko. | 16. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuweka fomu ya kuwasilisha malalamiko |
| 13. | **(TS Na. 477)**<br><br>21 Julai 2023 | *The Tanzania Investment Regulations, 2023*<br><br>(Zimetungwa chini ya Kifungu cha 5(4) na 35) | *The Tanzania Investment Act, (Cap. 38)* | Wizara ya Mipango na Uwekezaji | 1. **Kanuni ya 2** inatoa tafsiri ya maneno mbalimbali.<br><br>**Tatizo**<br>Kanuni ina makosa ya kiuandishi kwa kutofuata mpangilio | 1. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuondoa dosari za kiuandishi |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | wa maneno katika mtiririko wa kialfabeti.<br><br>2. **Kanuni ya 35** inaweka utaratibu wa rufaa dhidi ya maamuzi ya Kituo.<br><br>**Tatizo la Kwanza**<br>Kanuni haioneshi muda maalum ambao Waziri atatumia kufanya maamuzi dhidi ya Rufaa aliyoipokea.<br><br>**Tatizo la Pili**<br>**Kanuni ya 35 (3)** inaiondoa mahakama katika utoaji wa kauli ya mwisho katika masuala ya Haki | 2. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili:-<br>i. kuonesha Waziri atashughulikia shauri la rufaa ndani ya siku thelathini; na<br><br>ii. Kuongeza sharti linalotoa fursa kwa ambaye hajaridhika na uamuzi wa Waziri, kupeleka shauri Mahakama Kuu kwa mapitio. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 14. | **(TS Na. 482)**<br><br>21 Julai 2023 | *The Merchant Shipping (Establishment and Operation of Aids to Navigation) Regulations, 2023*<br><br>(Zimetungwa chini ya Kifungu cha 217 na 222) | *The Merchant Shipping Act, (Cap. 165)* | Wizara ya Uchukuzi | 1. **Kanuni ya 3** inatoa tafsiri ya maneno mbalimbali.<br><br>**Tatizo**<br>Kanuni ina makosa ya kiuandishi kwa kutofuata mpangilio wa maneno katika mtiririko wa kialfabeti.<br><br>2. **Kanuni ya 19** inahusu utatuzi wa migogoro inayohusu malipo ya madeni.<br><br>**Tatizo**<br>Kanuni inaelekeza migogoro ya namna hiyo isikilizwe na kuamuliwa na mahakama pasipo kuweka mfumo mwingine wa kusikiliza mashauri | 1. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuondoa dosari za kiuandishi<br><br>2. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuonesha utaratibu wa kusikiliza malalamiko. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | kabla ya kufika mahakamani.<br><br>3. **Kanuni ya 21** inampa Waziri mamlaka ya kutoa msamaha wa gharama yote au sehemu kwa vifaa vya kuongozea meli<br><br>**Tatizo**<br>Kanuni haijaonesha vigezo ambavyo Waziri atazingatia ili kutoa msamaha. Kutokuwekwa kwa vigezo, utoaji wa misahama isiyo na muongozo.<br><br>4. **Kanuni ya 26** inazungumzia ulinzi dhidi ya matendo yaliyofanywa na TASAC ama afisa wa | 3. Kanuni ifanyie marekebisho ili kuainisha vigezo vitakavyozingatiwa na Waziri ili kutoa msamaha.<br><br>4. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kufuta Kanuni ya 26. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | TASAC katika uwajibikaji chini ya kanuni hizi kwa kigezo cha matendo hayo kufanyika kwa nia njema.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni inaweka sharti la kuondoa uwajibikaji kwa upande wa TASAC ama afisa wa TASAC kwenye matendo yaliyoonekana kufanyika kwa nia njema.<br>Hali hii ni kinyume na misingi ya haki. | |
| 15. | **(TS Na. 486)**<br><br>21 Julai 2023 | *The Accountants and Auditors (Training and Examinations) By Laws, 2023* | *The Accountants and Auditors (Registration) Act, (Cap. 286)* | Wizara ya Fedha | 1. Sheria ndogo zina makosa katika jina kwa kurejea mwaka 2022 badala ya mwaka 2023. | 1. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kufuta mwaka 2022 na badala yake kuweka mwaka 2023. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (Zimetungwa chini ya Kifungu cha 45) | | | 2. **Kanuni ya 8** inahusu usajili wa mitihani<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>**Kanuni 8(2)(b)** inaweka sharti la lazima kwa mtu anayetaka kusajiliwa kwa ajili ya mitihani kuwa amepita kwa mto huduma ya mafunzo "*tution provider*"<br><br>3. **Kanuni ya 13** inahusu wanafunzi wenye mahitaji maalum.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni inawataka wenye mahitaji maalum kuwasilisha maombi ya mahitaji yao angalau siku kumi na nne kabla ya | 2. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuondoa sharti la lazima na badala yake kuweka sharti la hiari kupata huduma ya mafunzo.<br><br>3. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kutambua mahitaji maalumu wakati wa usajili. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | mitihani. Kanuni haijatambua misingi ya elimu shirikishi ya kutambua wtu wenye mahitaji muhimu wakati wa usajili.<br><br>4. **Kanuni 16(5)** imeipa Bodi sharti la hiari ya kupeleka mbele nusu ya gharama ya malipo ya mitihani kwa mwanafunzi ambaye ana sababu za msingi za kuahirisha mitihani.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Uhiari uliowekwa na Kanuni unaweza kusababisha Bodi kutopeleka mbele malipo ya wanafunzi waliokidhi vigezo. | 4. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuweka sharti la lazima kwa Bodi kupeleka mbele gharama ya malipo ya mitihani |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Hali hii inaweza kuathiri ustawi wa wanafunzi. | |
| | | | | | 5. **Kanuni ya 35 na 36** zinahusu uchakataji wa matokeo ya mitihani na *script moderation*.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni ina makosa ya uandishi kwa kuanza na uchakataji wa matokeo ikifuatiwa na script moderation badala kuanza na script moderation na kufuatiwa na uchakataji wa matokeo | 5. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuweka mtiririko sahihi wa hatua za uchakataji matokeo. |
| | | | | | 6. **Kanuni ya 37** inaweka utaratibu | 6. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | wa mapitio ya matokeo ya mitihani ya Bodi. **Kanuni ya 37 (2)** inaweka utaratibu ambao mwanafunzi ambaye hajaridhishwa na matokeo anaweza kuomba mapitio ndani ya siku 7 tangu kutangazwa kwa matokeo.<br><br>**<u>Tatizo la Kwanza</u>**<br>Bodi imepewa mamlaka ya mwisho ya uamuzi dhidi ya maombi ya mapitio yaliyoletwa mbele yake.<br>Hali hii ni kinyume na misingi utoaji wa haki iliyowekwa na Katiba ambayo itambua mahakama kama | kuonesha uamuzi utakuwa wa mwisho na pia kuonesha muda ambao Bodi itashughulikia mapitio ya matokeo ya mitihani |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | chombo cha mwisho cha utoaji haki<br><br>**<u>Tatizo la Pili</u>**<br>Kanuni haionyeshi muda ambao Bodi itafanya mapitio na kutoa uamuzi wake.<br><br>7. **Kanuni ya 44** inahusu kusimamishwa utahiniwa kwa sababu za utovu wa nidhamu na makosa kukiuka kanuni za mitihani.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Adhabu iliyowekwa na Kanuni inamzuia mtahiniwa kurejeshewa tena usajili wake. | 7. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuondoa katazo la kudumu na badala yake kuweka vipindi vya zuio la kufanya mtitihani |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA BUNGENI KATIKA MKUTANO WA KUMI NA TATU** | | | | | | |
| 16. | **(TS Na. 594)**<br>25 Agosti,2023 | *Rules Under the Energy and Water Utilities Regulatory Authority, 2023*<br><br>(Zimetungwa chini ya Kifungu 40 (1) (j)) | *EWURA ACT (Cap 414)* | Wizara ya Nishati | 1. **Kanuni ya 4** inahusu maombi ya mapitio ya shauri kuwa yatafanyika ndani ya siku kumi na nne baada ya kupokea uamuzi.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>**Kanuni ya 4** inakinzana na **Kifungu cha 27(1)** cha Sheria Mama kinachoeleza muda wa kuomba mapitio kwa kigezo cha kupokea kumbukumbu za uamuzi.<br><br>2. **Kanuni ya 4(1)** inaelekeza maombi ya mapitio | 1. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuonesha kuwa muda wa kuomba mapitio utahesabika baada ya kupokea kumbukumbu za uamuzi.<br><br>2. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuonesha kuwa maombi ya mapitio |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | yawasilishwe EWURA aidha, **Kanuni ya 7(2)** inaekeleza mombi ya kuwasilisha mapitio nje ya muda kwamba yatawasilishwa kwa Mkurugenzi Mkuu<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni inataja sehemu mbili za kuwasilisha maombi, hali inayoweza kusababisha kutokueleweka kwa sehemu iliyokusudiwa kuwasilisha maombi.<br><br>3. **Kanuni ya 7** inazungumzia utaratibu wa kuomba mapitio nje ya muda. | nje ya muda yatawasilishwa EWURA<br><br>3. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuweka fomu maalumu ya kuwasilisha maombi |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | **<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni imeweka utaratibu wa maombi ya mapitio nje ya muda bila kuweka fomu maalum ambayo itahusika katika maombi yanayohusika.<br>Hali hii inaweza kuleta kutoeleweka kwa utaratibu wa namna ya kuwasilisha maombi ya marejeo nje ya muda. | ya mapitio nje ya muda |
| | | | | | 4. **Kanuni ya 20(1)(a)** inatajwa wasifu wa mjumbe wa jopo la mapitio kuwa atatakiwa na ujuzi wa sheria | 4. Kanuni ifanyiwe marekebisho kuonesha ujuzi wa sheria unaokusudiwa |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | **Tatizo**<br>Kanuni haifafanui ni ujuzi upi wa fani ya sheria unaokusudiwa.<br><br>5. **Kanuni ya 21** inatamka adhabu ya faini isiyozidi shilingi milioni tatu au kifungo kisichozidi miaka mitatu au adhabu zote mbili kwa pamoja kwa mtu yeyote atakayezuia uendeshwaji wa mashauri ndani ya kamati.<br><br>**Tatizo**<br>Kanuni inaanzisha adhabu inayokinzana na adhabu inayowekwa | kuwa ni Wakili wa Mahakama Kuu<br><br>5. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuendana na masharti yaliyowekwa na Kifungu cha 42(1) |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | na **Kifungu cha 42(1)** cha sheria mama kinachotamka adhabu ya faini isiyozidi shilingi milioni tatu au Kifungo kisichozidi miaka mitano au au adhabu zote kwa pamoja kwa mtu atakayekiuka masharti yaliyowekwa na sheria mama.<br><br>Hali hii ni kinyume na Kifungu cha 36 cha sheria ya Tafsiri ya Sheria Sura ya 1. | |
| 17. | **(TS Na. 620)** 1 Septemba,2023 | *Rules under Petroleum (Settlement of Disputes Arising from Upstream* | Sheria ya Petroli (Sura ya 392) | Wizara ya Nishati | 1. **Kanuni ya 18 (1)** inamtaka Mkurugenzi Mkuu baada ya kumaliza uchunguzi wa awali, kuwasilisha shauri kwa mpatanishi | 1. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kufuta rejea ya Kanuni ya 18 na badala yake |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | *Operations), 2023*<br><br>(Zimetungwa chini ya Kifungu cha 246) | | | ndani ya siku thelathini kwa ajili ya upatanishi.<br><br>**Tatizo**<br>Kanuni imerejea **Kanuni ya 18** badala ya **Kanuni ya 17** hali inayoweza kuleta mkanganyiko wakati wa utekelezaji wa jukumu hilo.<br><br>2. **Kanuni ya 23 (1)** inaipa kamati uwezo wa kuamua kuhusu muda wa kushughulikia shauri (*speed track*) wakati wa kuendesha shauri.<br><br>**Tatizo**<br>Kanuni haiweki muda wa kushughulikia shauri (*speed track*) | kurejea Kanuni ya 17<br><br>2. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuweka speed track kwa mujibu wa Sheria ya Mashauri ya Daawa |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | ambao utazingatiwa katika kuamua muda husika.<br>Hali hii inaweza kuathiri upatikanaji wa haki kwa wakati kinyume na masharti yaliyowekwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977. | |
| | | | | | 3. **Kanuni ya 45** inaanzisha adhabu ya jumla kwa mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kanuni hizi pale ambapo hakuna adhabu mahsusi imetajwa na kwamba ukiukwaji huo utaadhibiwa kwa adhabu ya faini isiyopungua shilingi milioni tatu. | 3. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuendana na msahrti ya Kifungu cha 240(1)(vii) cha sheria mama. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | **Tatizo**<br>Adhabu inayoanzishwa na kanuni hizi inakinzana na adhabu ya jumla iliyowekwa na **kifungu cha 240(1) (vii)** cha sheria mama ambayo ni faini isiyopungua shilingi milioni kumi au kifungo kisichozidi miaka miwili au adhabu zote mbili kwa pamoja.<br>Hali ni kinyume na misingi inayowekwa na Kifungu cha 36 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria Sura ya 1. | |
| 18. | **(TS Na. 626)**<br>1 Septemba,2023 | Kanuni za utoaji wa Leseni za Biashara za Mwaka 2023 | Sheria ya Utoaji wa Leseni za Biashara (Sheria Na.25 ya 1972) | Wizara ya Viwanda na Biashara | 1. **Kanuni ya 3** inahusu maombi ya leseni ya biashara | 1. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuonesha taarifa zitakazohitajika ni zile zinazohusiana |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | zimetungwa chini ya Kifungu cha 29 (1) | | | **<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni inamtaka muombaji kuambatisha taarifa nyingine zozote. Hali hiyo inasababisha kutokutabirika kwa masharti ya kuzingatia wakati wa kuomba leseni ya biashara<br><br>2. **Kanuni ya 6** inaweka utaratibu wa kuomba nakala ya leseni kwa mmiliki wa leseni ambaye ameithibitishia mamlaka upotevu wa leseni hiyo.<br><br>**<u>Tatizo la Kwanza</u>**<br>Kanuni hii imeweka masharti ya hiari kwa mamlaka kutoa | na maombi ya leseni ya biasahara.<br><br>2. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa: -<br>a) kuweka sharti la lazima kwa mamlaka kutoa nakala kwa mmiliki wa leseni ambaye amethibitika kupoteza nakala halisi ya leseni; na |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | nakala ya leseni kwa muombaji aliyethibitisha kupotelewa na leseni yake.<br><br>Hali hii inaweza ikamuathiri mmiliki wa leseni pale ambapo mamlaka ikaona haina haja ya kutoa nakala husika hata baada ya kuthibitishwa kupotea kwa nakala halisi.<br><br>**<u>Tatizo la pili</u>**<br>Kanuni hii haijatoa muda maalumu wa mamlaka inayohusika kushughulikia na kutoa nakala ya leseni iliyoripotiwa | b) kuweka muda wa siku tatu za kazi kushughulikia na kutoa nakala ya leseni iliyoripotiwa kupotea, kuharibika, kutokusomeka vizuri au kuchanika |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | kupotea, kuharibika, kutokusomeka vizuri au kuchanika. Hali hii inaweza kusababisha ucheleweshwaji wa maombi ya leseni.<br><br>3. **Kanuni ya 11** inaweka utaratibu wa kurejesha ada ya leseni kwa mwombaji.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>**Kanuni ya 11(2)** inaweka sharti la kutorejesha ada iliyolipwa kwa kosa lililosababisha na uzembe.<br><br>4. **Kanuni ya 13(2)** inaeleza kuwa kila rufaa itafanyika | 3. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kufuta neno “uzembe“ na badala yake kuweka maneno “ukosefu wa umakini“<br><br>4. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kufuta neno |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | ndani ya siku thelathini.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>neno itafanyika lililotumika katika Kanuni linaleta mkanganyiko iwapo neno hilo lina maana ya:-<br>a) Rufaa kuwasilishwa kwa mamlaka; au<br><br>b) Rufaa kushughulikiwa na mamlaka. | "itafanyika" na badala yake kuweka maneno "itawasilishwa kwenye mamlaka ya rufaa". |
| | | | | | 5. **Kanuni ya 16** inaweka katazo la uwakilishi wa wakili pale ambapo mamlaka imeruhusu mrufani kufika mbele yake kwa ajili ya | 5. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kuondoa katazo la uwakilishi wa wakili katika mashauri ya rufaa |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | kusikiliza shauri la rufaa.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Masharti yanaowekwa na kanuni hii ni kinyume na masharti ya Ibara ya 13 (6) (a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977).<br><br>6. **Kanuni ya 17** inataja Kanuni zinazofutwa<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni haioneshi rejea iliyo kamili ya Kanuni inayofutwa.<br><br>7. Sehemu ya mwisho ya Kanuni imemtaja Waziri mwenye | 6. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuondoa makosa ya uandishi kwa krejea kwa ukamilifu Jina la Kanuni inayofutwa<br><br>7. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kuandika jina la Wizara kwa lugha |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | dhamana na Kanuni hizi.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni imeandika jina la Wizara kwa lugha ya kiingereza, ilhali Kanuni hizi zimeandikwa kwa lugha ya Kiswahili | ya Kiswahili ili kuendana na lugha iliyotumika katika Kanuni |
| 19. | **(TS Na. 649)**<br>8 Septemba,2023 | *The Capital Markets and Securities Tribunal Rules, 2023*<br>(Zimetungwa chini ya Kifungu 136 (j)) | *The Capital Markets and Securities Act (CAP 79)* | Wizara ya Fedha | 1. **Kanuni ya 20 (2)** inaweka zuio la kufungua upya rufaa kwa mrufani ambaye hakutokea siku iliyopangwa kusikilizwa kwa shauri lake na shauri hilo kutupiliwa mbali kutokana na kutokuwepo kwake.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Sharti linalowekwa na kanuni hii ni | 1. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuondoa zuio la kufungua upya rufaa kwa mrufani ambaye hakutokea siku iliyopangwa. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | kinyume na sheria ya uendeshwaji wa mashauri ya madai<br><br>Hali hii ni kinyume na misingi ya utoaji na upatikanaji wa haki.<br><br>2. **Kanuni ya 6** inataja wahusika wanaounda sekretarieti ya Baraza<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>**Kanuni ya 6(1)(f)** inamtaja dereva kuwa ni sehemu ya sekretarieti ya Baraza hali ya kuwa ni mtumishi wa kada saidizi.<br><br>3. **Kanuni ya 16 (2)** utaratibu wa kusambaza nakala | 2. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kumuondoa dereva katika Sekretarieti ya Baraza<br><br>3. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kufuta neno |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | ya notisi ya kuondoa shauri la rufaa kwa mrufaniwa au mtu yoyote atakayeathiriwa na rufaa inayohusika.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni imetumia neno "*before*" ambalo linasabisha kutoelewekwa kwa muda sahihi wa kusambaza nakala za notisi ya kuondoa shauri kwa wanaohusika. | "before" ili kuweka maana iliyokusudiwa na Kanuni |
| | | | | | 4. **Kanuni 27** ina makosa ya uandishi kwa kuandika maneno "*taken down*" | 4. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kufuta maneno "taken down" ili kuleta maana iliyokusudiwa |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | **<u>Tatizo</u>**<br>Maneno yanaonesha muktadha tofauti na muktadha uliokusudiwa.<br><br>5. **Kanuni ya 38** inahusu Baraza kuwezeshwa na vyombo vingine wakati wa utekelezaji wa uamuzi kama ilivyo katika utekelezaji wa uamuzi wa Mahakama<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni ina makosa ya uandishi kwa kurejea Kifungu cha 38 badala ya Kifungu cha 37 kilichokusudiwa. | <br><br><br><br><br><br>5. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kufuta rejea ya Kifungu cha 38 na badala yake kurejea Kifungu cha 37 |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 20. | **(TS Na. 714)**<br>22 Septemba,2023 | Kanuni za Umiliki Manufaa za Mwaka 2023<br><br>(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 22) | Sheria ya Majina ya Biashara (Sura ya 213) | Wizara ya Viwanda na Biashara | 1. **Kanuni ya 9 (2)** inaweka sharti la lazima kwa msajili kuwajulisha watuma maombi iwapo maombi yao ya kusajili nyaraka za jina la biashara yamekataliwa.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni haijaweka muda maalum ambao msajili atapaswa kuwajulisha wahusika juu ya uamuzi wake wa kukataa kusajili nyaraka za jina la biashara zao.<br>Hali hii ni kinyume na misingi ya haki iliyowekwa wa mujibu na Katiba. | 1. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuweka sharti kwa Msajili kuwajulisha watuma maombi ndani ya siku tatu za kazi kuhusu kukataliwa kwa maombi ya kusajili nyaraka zinazohusika. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 2. Kanuni hazioneshi utaratibu wa rufaa dhidi ya maamuzi mbalimbali yatakayofanywa na msajili. Kutokuoneshwa kwa utaratibu wa rufaa kunaweza kutatiza walengwa kuhusu namna ya kukata rufaa pale ambao hawajaridhishwa na uamuzi wa awali, hivyo kuathiri haki zao.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Hali hii ni kinyume na misingi ya haki kama ilivyoanzishwa na Katiba. | 2. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kutambua haki ya kukata rufaa na kuonesha utaratibu wa namna kuwasilisha rufaa. |
| 21. | **(TS Na. 726)**<br>6 Oktoba,2023 | *The Banking and Financial Institutions* | *The Banking and Financial Institutions Act* | Wizara ya Fedha | 1. **Kanuni ya 5 (1) (a)** inazungumzia muda wa kuwasilisha | 1. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuweka ukomo wa |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | *(Prompt Corrective Actions) Regulations, 2023*<br><br>(Zimetungwa chini ya Kifungu cha 71) | *(CAP 342)* | | mpango wa maandishi kuhusu hatua za marekebisho *"written plan of corrective actions"* utaratibu wa kuandaa ratiba inayopendekezwa ya kusahihisha makosa kama yalivyotambulika.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni haijataja muda unaokusudiwa kuwasilisha mpango wa maandishi kuhusu hatua za marekebisho *"written plan of corrective actions".* Hali hii inaweza kusababisha kukosekana kwa muongozo | muda wa kuwasilisha mpango wa maandishi kuhusu hatua za marekebisho "*written plan of corrective actions*". |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
| --- | --- | --- | --- | --- | --- | --- |
| | | | | | unaoeleweka kuhusu muda unaokusudiwa.<br><br>2. **Kanuni ya 6 (c)** inazungumzia hatua zinazoweza kuchukuliwa na Benki Kuu dhidi ya taasisi ya kifedha ama benki yenye mtaji wa kutosha itakayokiuka maelekezo kuwa inaweza kusimamisha wakurugenzi wake au kuondoa kwenye nafasi zao.<br><br>**Tatizo**<br>Kanuni haioneshi ukomo wa adhabu ya kusimamishwa kazi au sababu zinazoweza | 2. Kanuni ifanyiwe marekebisdho ili kuonesha wa muda wa adhabu ya kusimamishwa kazi. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | kupelekea adhabu kuisha. | |
| 22. | **(TS Na. 729)**<br>6 Oktoba,2023 | *Foreign Exchange (Bureau De Change) Regulations, 2023* | *Foreign Exchange Act (CAP 271)* | Wizara ya Fedha | 1. **Kanuni ya 5(1)** inaonesha vigezo vya kuomba leseni ya duka la kubadilishia fedha za kigeni<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni imetumia neno "isipokuwa" ambalo linaondoa maana iliyokusudiwa kuhusu wanaoweza kuomba leseni zinazohusika<br><br>2. **Kanuni ya 6(2)** inaweka sharti kwa muombaji wa leseni A na B ambaye si Kampuni, kuwasilisha maombi | 1. Kanuni ya 5(1) irekebishwe kwa kwa kufuta neno "isipokuwa" ili kuleta maana iliyokusudiwa na Kanuni<br><br>2. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kuweka tafsiri ya neno "Mkurugenzi" |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | yaliyosainiwa na Mkurugenzi.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni haijaweka tafsiri ya neno Mkurugenzi anayekusudiwa. Hali hii inaweza kuleta mkanganyiko wa tafsiri ya Mkurugenzi aliyekusudiwa na Sheria hii.<br><br>3. **Kanuni ya 7(1)** inazungumzia kuhusu jina la biashara litapaswa kujumuisha maneno "*Bureau de Change*, "*Forex Bureau*" au "*Foreign Exchange Bureau*" | <br><br><br><br><br><br><br><br><br><br><br><br>3. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuonesha kuwa mtu anaweza kuchagua moja kati ya majina matatu yaliyoainishwa katika Kanuni |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | **Tatizo**<br>Kanuni haioneshi kuwa mtu anapaswa kuchagua moja kati ya majina hayo. Hali hii inaleta mkanganyiko kuhusu azma iliyokusudiwa na Kanuni hii kuhusu majina ya biashara ya maduka ya kubadilishia fedha.<br><br>4. **Kanuni ya 40** inataja adhabu ya kutoza faini sawa na kiwango kisichozidi dola za kimarekani elfu tatu pale ambapo Benki itajiridhisha kwamba duka la kubadilisha fedha za kigeni limekiuka masharti ya Sheria, au Kanuni hizi. | <br><br><br><br><br><br><br><br><br><br><br><br>4. **Kanuni ya 40** ifanyiwe marekebisho ili kuonda sharti la malipo kwa kutumia dola za kimarekani |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria Mama | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | **<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni hii imeweka viwango vya adhabu kwa dola za kimarekani badala ya shilingi za kitanzania ambavyo vimetajwa na katika maeneo mengine ya Kanuni hizi.<br>Hali hii ni kinyume na Muongozo wa Gavana wa Benki Kuu wa tarehe 20 Juni, 2023 kuhusu kuzuia matumizi ya fedha za kigeni kwa malipo mbalimbali yanayofanyika nchini. | |

**MHE. BALOZI LIBERATA R. MULAMULA:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Sasa kwa utaratibu wetu taarifa ikishasomwa namna hii aidha, Wabunge wapewe nafasi ya kuchangia halafu hoja ihitimishwe au tupeleke haya maazimio ambayo yapo hapa kwa kulihoji Bunge halafu Serikali ikayafanyie kazi.

Sasa kuna mambo machache humu ambayo yamezungumzwa hasa yale ambayo Kamati ilishafanya kazi huko nyuma na taasisi mbalimbali ambazo zimekasimiwa hayo madaraka na Bunge hazijaweza kurekebisha na naona yapo mengi sana hapa. Kwa muktadha huo, kwa sababu yapo haya ambayo hayajafanyiwa marekebisho na mchapaji wa hizi sheria ndogo ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali, nimpe nafasi yeye aseme kwa nini hawafanyi haya ambayo Bunge linakuwa limeagiza kwenye changamoto zinazokuwa zinaoneshwa na Kamati yetu ya Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali karibu. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukushukuru kwa nafasi uliyonipatia, lakini pia nishukuru sana kazi kubwa iliyofanywa na Kamati ya Bunge na kuweza kuwasilisha maeneo mbalimbali waliyoyapitia na kufanya uchambuzi.

Mheshimiwa Spika, zipo dosari ambazo zimeanishwa kwenye Taarifa ya Kamati. Nikuhakikishie tu wewe pamoja na Bunge lako Tukufu kwamba mara baada ya taarifa hizi zinapowasilishwa Bungeni na Kamati husika, Serikali kwa ujumla wake ikiwemo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, tumekuwa tukichukua hatua mbalimbali za kuhakikisha tunaepusha kadhia iliyojitokeza kwa aidha kuwa na sheria ndogo zinazokinzana na Katiba au masharti ya sheria mama au kuwa na upungufu kwenye uandishi.

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha wa taarifa iliyowasilishwa imetoa *timeline* Serikali iweze kuwasilisha taarifa yake ifikapo mwezi Machi. Sasa hatua ambazo tumekwishakuanza kuzichukua tukiwa kwenye michakato kama Kamati wenyewe walivyokiri kwamba ofisi yangu imekuwa ikishirikiana na wao moja kwa moja, ofisi yangu kwa kushirikiana na zile mamlaka zilizokasimiwa mamlaka ya kutunga sheria ndogo chini ya Ibara ya 97(5) tumeweka mkakati wa kuwa na vikundi vya timu za wataalamu kuona namna ambavyo tunaongeza kasi ya kurekebisha hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini tulianza kwa kuandaa miongozo ambayo nikiri mpaka sasa imeanza kutusaidia na imeanza kuleta tija; Mwongozo wa Uandishi wa Sheria Ndogo na Sheria Mama, lakini pia kuzihusisha mamlaka kwa maana ya Wizara na Taasisi za Serikali zenye dhamana. Kwa mwaka ujao wa fedha tayari Serikali kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, mkakati mmoja ni kuhakikisha kwamba Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria kwa mara ya kwanza tumeomba itengewe fungu ambalo litaiwezesha kuwa na Mawakili wa Serikali upande wa uandishi wa sheria ambao watakuwa wanakaa kwa muda wa kutosha na hizi mamlaka zilizokasimiwa kuandaa hizi sheria ndogo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo itoshe tu kusema kwamba Serikali haipendezwi na kuendelea kuwepo kwa dosari hizi, lakini pia tunachukulia kwa uzito umuhimu wa kuwepo kwa Kamati hii kwa sababu ni vizuri kuwa na *checks and balance,* kwa sababu azma yetu sisi kama Serikali na kama alivyosema Mheshimiwa Mwenyekiti ni kuhakikisha kwamba sheria zinazotungwa na Bunge hili basi inapolazimu zitungiwe sheria ndogo ziwe ni zile sheria kwa mujibu wa makusudio yaliyokuwepo labla hazijatungwa.

Mheshimiwa Spika, lakini kuwezesha sheria mama pamoja na sheria ndogo ziweze kuwa chachu ya maendeleo kwa wananchi wetu bila kuleta kero hasa kwa kuondokana na yale maeneo ambayo kwa mfano, ukiukwaji wa misingi ya uandishi au kukiuka uandishi wa majedwali ambayo yanasomeka pamoja na sheria mama au kuwa na sheria ndogo ambazo haziakisi ule uhalisia katika utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, nikuahidi tu kwamba Serikali ndiyo maana tumesimama kuunga mkono taarifa hii na tutaichukulia kwa uzito wake ili tuone tutaleta tofauti ya maboresho na matokeo chanya kadri tunavyoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana kwa maelezo hayo Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mwenyekiti wa Kamati uje uhitimishe hoja yako. *(Makofi)*

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuja kuhitimisha hoja ya Kamati, lakini nimshukuru pia Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa maelezo yake ambayo yameongezea nyama na kujibu baadhi ya hoja.

Mheshimiwa Spika, cha msingi ni kwamba kazi ya kutunga sheria ni ya Bunge, ziwe sheria mama, ziwe sheria za nchi, ziwe sheria ndogo jukumu ni la Bunge. Kwa hiyo, tunapokasimu kwa mamlaka nyingine, kwa mashirika, kwa Mawaziri na kwa watu wengine tunakasimu jukumu letu, lakini endapo itatokea kwamba kuna dosari kama ambavyo zipo kwa sasa lawama ni ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni wajibu wa Bunge kuhakikisha kwamba sheria hizi zinabaki na zinakuwa nzuri, ziwe sheria mama, ziwe sheria ndogo lazima ziwe sheria nzuri ambazo zinasaidia kuongeza ufanisi na wananchi wasipate dosari na athari mbalimbali.

Kwa hiyo, kwa vile Mwanasheria Mkuu wa Serikali amekubali kwamba ipi itafanyika, basi nisisitize kwamba zifanyike haraka kama tulivyosema *timeline* yetu ile, lakini si hiyo pekee yake hata Wizara nyingine ambazo tunawaita kwenye Kamati, tunakaa nao na wanakubali kwamba wanafanyia kazi basi wafanye kazi hiyo kwa weledi na kwa muda mfupi na tumalize jambo hili vizuri.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge liipokee na kuyakubali maoni na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati kama ambavyo nimeyasoma hapo awali.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**MHE. BALOZI LIBERATA R. MULAMULA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana. Sasa kwa utaratibu wetu nitawahoji kuhusu Hoja ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2023.

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Kwa hiyo, Maazimio yaliyoandikwa humu na Kamati yetu yanakuwa sasa Maazimio ya Bunge na Serikali kama alivyosema Mwanasheria Mkuu wa Serikali, waende wakayafanyie kazi hasa kwa kuzingatia kwamba kwa sababu mamlaka ya kutunga sheria ni ya Bunge na Bunge limekasimu kwa hawa kile inachosema Bunge ndicho wanachopaswa kufuata; na katika hali ya kawaida ni kwa vile tu mahusiano ya Bunge na taasisi hizi bado tunategemeana, lakini ilipaswa Kamati yetu ya Sheria Ndogo ikifika hapa iseme inafuta hii, inafuta hii, ili wakatengeneze upya hiyo nyingine isiwepo kabisa.

Waheshimiwa Wabunge, lakini utaratibu uliopo nadhani unaendelea kufanya kazi vizuri kwa sababu sote tunafahamu Kamati hii inafanya kazi kubwa sana, lakini haijakuwepo miaka mingi. Kwa hiyo, utaratibu huu uliopo unaendelea kutoa hiyo fursa ya wote kuendelea kushirikiana vizuri. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mwanasheria Mkuu wa Serikali tunaamini taarifa ijayo haya ambayo wamependekeza hapa yatakuwa yamekuja kwa ajili ya yale mapya kwa zile sheria ndogo mtakazokuwa

mmezileta mpya lakini yale ambayo walishasema yabadilishwe basi yaende yakabadilishwe.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge sasa nimwite Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE**

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 35(2) naomba kutoa taarifa kwamba shughuli zote zilizokuwa zimewekwa kwenye orodha ya shughuli za Mkutano wa Kumi na Nne sasa zimemalizika.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja ya kuahirisha Bunge. Nimwite sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa aje atoe hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, wakati tukielekea kuhitimisha shughuli zote za Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge la Kumi na Mbili hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia kuwa na afya njema kwa kipindi chote cha majuma matatu ya kutekeleza majukumu ya shughuli za Bunge kwa mujibu wa ratiba. Vilevile tuendelee kumuomba Mwenyezi Mungu atujalie heri na baraka katika mwaka 2024 na kutuwezesha kutekeleza majukumu yote ya kitaifa kama yalivyopangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maono yake makubwa ambayo yameendelea kuchagiza kasi ya maendeleo ya Taifa letu. Sote tumeshuhudia jitihada na dhamira yake njema ya kuleta mageuzi katika uchumi, utoaji wa huduma za jamii na kuimarisha ustawi wa kila mwananchi wa Tanzania. Niwasisitize Watanzania wenzangu tuendelee kumuunga mkono Mheshimiwa Rais katika utekelezaji wa maono yake kwa mustakabali wa maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Phillip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoifanya katika kumsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kukushukuru na kukupongeza sana wewe binafsi kwa kuendelea kuliongoza vema Bunge lako Tukufu, sina shaka Waheshimiwa Wabunge wenzangu mtakubaliana nami kuwa Mheshimiwa Spika ameendelea kuonesha ukomavu, ustahimilivu na weledi wa hali ya juu katika kusimamia shughuli za Bunge pamoja mijadala yote kama ilivyopangwa katika Mkutano huu wa Kumi na Nne tutakaouhitimisha muda mfupi ujao. Hongera sana Mheshimiwa Spika kwa kutekeleza majukumu yako kwa viwango vya hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge na Naibu Spika kwa umahiri ambao ameendelea kuuonesha katika kutekeleza majukumu ya kukusadia wewe Mheshimiwa Spika kuliongoza Bunge lako Tukufu. Kipekee niwapongeze pia Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge ambao ni Mheshimiwa Najma Murtaza Giga na Mheshimiwa Daniel Baran Sillo kwa kazi nzuri wanayoifanya, ama kwa hakika wamekuwa nguzo kubwa na muhimu katika kutekeleza Shughuli za Mkutano huu wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu salamu za pole; wakati tukiendelea na Mkutano huu wa Kumi na Nne wa Bunge lako Tukufu, mnamo tarehe 10 Februari, 2024 tuliondokewa na

mpendwa wetu, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, mwanasiasa mahiri aliyewahi kuwa Mbunge wa Jimbo la Monduli na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nami niungane na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoa salamu za pole kwa familia, kipekee kwa Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Fredrick Lowassa, ndugu, jamaa na marafiki wa marehemu, wana-CCM na Watanzania wote kwa ujumla. Hayati Mheshimiwa Edward Lowassa atakumbukwa kwa uthubutu wake, uwezo, mvuto na ushawishi mkubwa wa kisiasa ndani na nje ya nchi yetu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aendelee kumpa marehemu pumziko la amani, Amina.

Mheshimiwa Spika, niruhusu sasa nizungumze machache kuhusu utumishi wa mpendwa wetu Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa ndani ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Edward Lowassa akiwa Mbunge wa Jimbo la Monduli, alilitumikia Bunge la Kumi katika nafasi ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama katika nusu ya kwanza ya uhai wa Bunge la Kumi na katika nusu ya pili, akawa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa chini ya uongozi wa Mheshimiwa Edward Lowassa ilifanikiwa kutatua changamoto za baadhi ya Ofisi za Balozi zetu kuchelewa kupata mawasiliano hususan pale Balozi anapohitimisha muda wake. Aidha, iliweza kuhakikisha kunakuwepo na mawasiliano ya haraka pamoja na kutatua suala la *"Diplomatic Bags"* kutoa majibu kwa haraka. Vilevile Kamati hiyo ilianzisha utaratibu wa kutembelea Ofisi za Balozi zetu katika nchi mbalimbali, jambo ambalo lilisaidia kubaini changamoto na kuzitafutia ufumbuzi wake.

Mheshimiwa Spika, licha ya hayo kati ya mwaka 1990 na 2005 Mheshimiwa Edward Lowassa amewahi kuwa Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Sera, Uratibu, Mahakama, Masuala ya Bunge na Uratibu wa Maafa, lakini pia

alikuwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, amekuwa Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia Muungano, Mazingira na Kuondoa Umaskini; na baadaye alikuwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo nafasi ambazo alizitumikia kwa weledi na ameacha alama kubwa kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa alikuwa Waziri Mkuu wa Tisa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akipokea nafasi hiyo kutoka kwa Mheshimiwa Fredrick Tluway Sumaye.

Mheshimiwa Spika, Taifa litaendelea kumkumbuka Hayati Edward Ngoyai Lowassa kwa rekodi kubwa ya usimamizi wa shughuli za Serikali ikiwemo masuala yafuatayo: -

(i) Kusimamia ujenzi wa shule za sekondari katika kila Kata ambao uliwezesha watoto wengi waliofaulu elimu ya msingi kujiunga na elimu ya sekondari; *(Makofi)*

(ii) Kusimamia uamuzi wa kubadili Vyuo vya Ualimu vya Mkwawa na Chang'ombe ili viwe Vyuo Vikuu vya Ualimu;

(iii) Kuruhusu biashara ya pikipiki kubeba abiria jambo ambao lilisaidia vijana kupata ajira;

(iv) Kuhimiza ujenzi wa zahanati katika kila kijiji na ujenzi wa vituo vya afya katika kila Kata; *(Makofi)*

(v) Kusimamia kikamilifu kuanzishwa kwa Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari (MMES); *(Makofi)*

(vi) Kuhamasisha jamii ya wafugaji kupenda elimu kwa kuanzisha shule nyingi za sekondari katika maeneo yao wafugaji; *(Makofi)*

(vii) Kutilia mkazo suala la elimu na kupiga vita mimba kwa wanafunzi; *(Makofi)*

(viii) Kusimamia uanzishwaji wa *SACCOS* hapa nchini; na

(ix) Mheshimiwa Waziri Mkuu, Edward Lowassa katika kipindi chake alikuwa ana uwezo mkubwa kufuatilia kwa karibu utendaji wa kazi ndani ya Serikali, ukaguzi wa miradi na kutamani kuona matokeo ya papo kwa papo; lakini pia na kuchukua hatua pale ambapo kuna ubadhirifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati Taifa letu likiendelea na maombolezo, tumepokea kwa masikitiko makubwa taarifa za kuondokewa na waliokuwa Waheshimiwa Wabunge ambao waliwahi kushika nafasi mbalimbali za Uwaziri. Mnamo tarehe 12 Februari, 2024 tulipokea taarifa ya kuondokewa na Mheshimiwa Balozi Diodorus Kamala aliyefariki Jijini Dar es Salaam. Mheshimiwa Kamala aliwahi kuwa Mbunge wa Jimbo la Nkenge Mkoani Kagera na pia alikuwa Waziri wa Afrika Mashariki na baadaye kuwa Balozi wa Tanzania nchini Ubelgiji na Uholanzi. Vilevile, tarehe 13 Februari, 2024 tulipokea taarifa ya kuondokewa na Dkt. Ibrahim Msabaha, aliyewahi kuwa Mbunge wa Jimbo la Kibaha na Waziri wa Madini na Nishati, lakini pia Waziri wa Afrika Mashariki. Ninatoa pole kwa familia, ndugu, jamaa, marafiki, wana-CCM na Watanzania wote kwa kuondokewa na wapendwa wetu.

Mheshimiwa Spika, hakika michango yao katika utumishi wa umma, utendaji Serikalini pamoja na kuwawakilisha Watanzania itaendelea kukumbukwa daima. Ninamuomba Mwenyezi Mungu awape marehemu pumziko la amani, Amina.

Mheshimiwa Spika, vilevile nitumie nafasi hii kutoa salamu za pole kwa waathirika wote maafa yaliyotokea Hanang, Mkoani Manyara kufuatia maporomoko ya udongo katika Mlima Hanang yaliyogharimu maisha ya Watanzania wenzetu pamoja na kusababisha uharibifu wa mali na majeruhi. Ninawasihi sana Watanzania wote tuendelee kuonesha uvumilivu, mshikamano na umoja wakati maafa yanapojitokeza ili kwa pamoja tuwe sehemu ya kurejesha hali kwa waathirika wote.

Mheshimiwa Spika, katika siku za hivi karibuni nchi yetu pia ilikumbwa na mafuriko yaliyosababisha athari mbalimbali ikiwemo

vifo, uharibifu wa mali na miundombinu. Ninatoa pole kwa Watanzania wote waliopoteza wapendwa wao na wengine kujeruhiwa kutokana na mafuriko, lakini pia ninatoa pole kwa waathirika wa matukio mengine yakiwemo majanga ya moto na ajali za vyombo vya usafiri. Tuendelee kumuomba Mwenyezi Mungu awajalie majeruhi afya njema na awape marehemu pumziko la amani, Amina.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maswali na majibu; katika Mkutano huu wa Kumi na Nne wa Bunge la Kumi na Mbili, jumla ya maswali 224 ya msingi na mengine 871 ya nyongeza yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kujibiwa na Serikali. Pia, jumla ya maswali 12 yalielekezwa kwa Waziri Mkuu na kujibiwa kwenye kipindi cha Maswali ya Papo kwa Papo. Niwapongeze Waheshimiwa Wabunge kwa umahiri waliouonesha katika kufuatilia na kuisimamia Serikali, kwani maswali hayo yanasaidia kuikumbusha na kuifanya Serikali itoe ufafanuzi na kuchukua hatua katika masuala mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kupitia Mkutano huu Bunge lako Tukufu kwa sehemu kubwa lilikuwa na kazi ya kupokea na kujadili taarifa 16 za Kamati za Kudumu za Bunge. Taarifa hizo ni kama zifuatazo:-

(i) Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu;

(ii) Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini;

(iii) Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii;

(iv) Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo;

(v) Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii;

(vi) Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira;

(vii) Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama;

(viii) Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI;

(ix) Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo;

(x) Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;

(xi) Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria;

(xii) Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma;

(xiii) Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kamati ya Bajeti;

(xiv) Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kamati ya Hesabu za Serikali;

(xv) Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kamati ya Hesabu ya Serikali za Mitaa; na

(xvi) Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kamati ya Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Spika, katika mkutano huu pia Bunge limeweza kutoa maazimio; Azimio la Bunge ambalo limeweza kuondoa kigezo cha kupitia JKT na JKU kama sifa ya msingi ya kujiunga na vyombo vya ulinzi na usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika taarifa hizi muhimu zilizowasilishwa na Kamati zetu, tumeshuhudia mijadala mizuri ambayo ilijielekeza kwenye kupanga maendeleo ya pamoja ya Taifa letu. Aidha, Serikali imepokea maoni na mapendekezo yaliyotolewa na

Waheshimiwa Wabunge katika mkutano huu na inaahidi itayafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu miswada ya sheria; katika mkutano huu, Bunge lako Tukufu limepokea miswada minne ya sheria na imepitishwa kwa hatua zote kama ifuatavyo: -

(i) Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka 2023;

(ii) Muswada wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi ya mwaka 2023;

(iii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Vyama vya Siasa ya mwaka 2023; na

(iv) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali (Na.5) ya mwaka 2023.

Mheshimiwa Spika, tarehe 1 Februari, 2024 nilitumia Kanuni ya Kudumu ya Bunge Toleo la Februari, 2023, Kanuni ya 44(4) ambayo inatoa fursa kwa Waziri Mkuu kupitia kipindi cha Maswali ya Papo kwa Papo kutoa taarifa kwenye jambo lenye maslahi kwa Taifa. Hivyo, nilitumia fursa hiyo kutoa taarifa kuhusiana na hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, Toleo la mwaka 2023 na Mitaala ya Elimu Ngazi ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Elimu ya Ualimu.

Mheshimiwa Spika, naomba nieleze taarifa ya maandalizi ya Dira Mpya ya Taifa ya Maendeleo; ajenda ya maendeleo ya Taifa letu imefafanuliwa na inaongozwa na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025 ambayo utekelezaji wake unatarajiwa kufikia ukomo mwezi Juni, 2026. Hivyo, Serikali imeanzisha mchakato wa kuandaa Dira Mpya ya Taifa ya Maendeleo ambayo inatarajiwa kutoa mwongozo wa mwelekeo wa maendeleo ya nchi kwa kipindi cha miaka zaidi ya 25 ijayo.

Mheshimiwa Spika, kazi zinazofuata katika maandalizi ya Dira mpya ya Taifa ya Maendeleo ni pamoja na: -

(i) Kutoa elimu kwa umma kupitia Kampeni ya Kitaifa ya Uhamasishaji wananchi kushiriki katika maandalizi ya dira mpya;

(ii) Kukamilisha na kusambaza taarifa ya ukusanyaji maoni;

(iii) Uchambuzi wa taarifa ya tathmini ya utekelezaji wa Dira 2025 kwa ajili ya maandalizi ya maandiko mahsusi ya kisera kwa ajili ya kuzingatiwa katika dira mpya pamoja na kuainisha;

(iv) Kufanya tafiti katika maeneo mbalimbali ambazo zitatoa taarifa katika uandishi wa dira mpya;

(v) Uchambuzi na majadiliano ya kina ya kitaalam na wabobezi kwenye maeneo yatakayoongoza uandishi wa dira;

(vi) Kujifunza uzoefu wa nchi mbalimbali zilizofanikiwa kufanya mageuzi makubwa ya kimaendeleo katika maeneo ya sekta mbalimbali;

(vii) Uandishi wa Dira mpya na Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu; na

(viii) Uidhinishaji wa Dira na Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu.

Mheshimiwa Spika, nitoe rai kwa Watanzania wote bila kujali itikadi za kisiasa, kidini na kikabila kushiriki kikamilifu kutoa maoni ili kuhakikisha uwepo wa Dira mpya ya Taifa ya Maendeleo ambayo ni jumuishi na shirikishi. Aidha, viongozi wa Mikoa, Wilaya, Halmashauri, Kata/Shehia, Mitaa, Vijiji na Vitongoji vyote wahamasishe na kuelimisha wananchi wanaoishi katika maeneo yao ili washiriki kikamilifu katika kutoa maoni ya Dira mpya ya Taifa ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, vilevile vyombo vya habari vitenge muda na kuweka kipaumbele katika kuelimisha na kuhamasisha wananchi kuhusu umuhimu wa kushiriki kikamilifu katika zoezi la

kutoa maoni, andaeni vipindi na makala maalum ili kila mwananchi aweze kupata taarifa. Redio za Jamii nazo zihusike kikamilifu kuelimisha umma.

Mheshimiwa Spika, kadhalika sekta binafsi, asasi za kiraia, makundi maalum kama vile vijana, wanawake, wazee, watu wenye ulemavu na mashirikisho mengine yashirikiane na Tume ya Mipango katika uratibu wa ukusanyaji wa maoni ya wanachama na wadau wao ambao nao pia wana nafasi kubwa ya kutoa maoni yao. Hii itasaidia kuhakikisha kuwa maoni ya makundi husika yanapokelewa na kujumuishwa katika maandalizi ya Dira mpya ya Taifa ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa tahadhari kuhusu hali ya chakula kufuatia mvua kubwa zinazofuatia; kufuatia mvua kubwa zinazoendelea kunyesha hapa nchini katika maeneo mbalimbali nchini na kusababisha uharibifu wa mazao, nitoe wito kwa wakulima kujielekeze katika kilimo cha mazao yanayoendana na hali ya hewa pamoja na kufuata maelekezo ya maafisa ugani walioko katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Maafisa Ugani wafuatilie kwa karibu taarifa za mara kwa mara za mwenendo wa hali ya hewa nchini. Hii itawawezesha kuwa na wigo mpana wa kuwashauri wakulima mazao yanayofaa kulimwa katika maeneo yao pindi yanapotokea mabadiliko ya hali ya hewa.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kuwasisitiza wananchi kuhifadhi chakula cha kutosha na kuepuka matumizi ya chakula na yasiyokuwa ya lazima kutokana na uharibifu mkubwa wa mazao yaliyopo mashambani uliosababishwa mafuriko.

Mheshimiwa Spika, naielekeza Wizara ya Ujenzi kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* na Ofisi ya Rais - TAMISEMI kupitia Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini *(TARURA)* kuendelea kujipanga na kuwa na utayari wa kukabiliana na changamoto za kukatika kwa mawasiliano ya barabara kutokana na mvua hizi kubwa zinazoendelea kunyesha hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, aidha, ziendelee kuzingatia taarifa za utabiri wa hali ya hewa kadri zinavyoendelea kutangazwa na Mamlaka ya Hali ya Hewa, lakini vilevile Jeshi la Polisi liendelee kusimamia usalama wa barabara zetu na kuongoza vyombo vya moto ili kuepusha changamoto zinazoweza kujitokeza kwenye barabara zinazoharibiwa na mvua. Madereva nao wachukue tahadhari ya kutosha na kuwa na subira wanapoona maji yamefunika barabara na madaraja ili wasije kutumbukia kwenye maeneo yaliyomomonyoka.

Mheshimiwa Spika, naomba kuzungumzia maandalizi ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa; nitumie fursa hii kuielekeza Ofisi ya Rais - TAMISEMI ishirikiane na wadau mbalimbali katika maandalizi ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Wasimamizi wa maboresho ya daftari la mpigakura wahamasishe umma na kutoa elimu ya mpigakura kwa makundi yote katika jamii, lengo likiwa kuwafikia wananchi wote na kuwawezesha kuelewa sheria, kanuni, taratibu za mchakato mzima wa uchaguzi, wajibu wao na umuhimu wa kushiriki kwao katika uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa suala la elimu ni muhimu katika kuongeza idadi ya wananchi watakaojiandikisha katika daftari la mpigakura na hatimaye kuwa na sifa ya kupiga kura wakati uchaguzi, nitumie fursa hii kutoa rai kwa Watanzania wote kushiriki katika hatua hii muhimu. Watanzania wenzangu jitokezeni kwa wingi katika vituo vitakavyowekwa, jiandikisheni ili msipoteze haki yenu na baadaye muweze kupiga kura.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sekta ya michezo; sina shaka Waheshimiwa Wabunge wenzangu mtakubaliana nami kuwa nchi yetu imeendelea kupata mafanikio makubwa sana katika sekta ya utamaduni, sanaa na michezo. Tumekuwa tukishuhudia ushiriki wa mtu mmoja mmoja, vilabu au timu zetu za Taifa zikifanya vizuri na kukonga nyoyo za washabiki wa Watanzania kwa ujumla wake. Hongereni sana wachezaji wote kwa kuwakilisha vema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mpira wa miguu tumeshuhudia vilabu vyetu vikizidi kung'ara katika mashindano mbalimbali ndani na nje ya nchi. Aidha, timu zetu za Taifa nazo

zimeendelea kufanya vema. Kama mtakumbuka, kwa mara ya kwanza timu zetu zote za Taifa za mpira wa miguu za wanaume na wanawake, *Taifa Stars* na *Twiga Stars* zilifanikiwa kufuzu Mashindano ya Mataifa ya Afrika; *AFCON 2023* na *WAFCON 2024*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba *Taifa Stars* ilishindwa kusonga mbele kwenye hatua ya mtoano, lakini ilionesha kiwango cha hali ya juu hususan kwenye michezo miwili ya kundi *F* lililohusisha timu za Morocco, DR Congo, Zambia na Tanzania. Ninawapongeza sana wachezaji wote, walimu wao na kila mmoja aliyeshiriki kwa namna moja au nyingine katika hatua zote za mafanikio ya timu zetu za Taifa. Ninaamini timu zetu zitaendelea kujifua na kufanya vema, kuwapa burudani Watanzania na kuliheshimisha soka la nchi yetu kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niliombe Shirikisho la Soka nchini kuendeleza mshikamano baina yake na wadau wa michezo, wachezaji na mabenchi ya ufundi na timu zetu zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya Timu zetu za Taifa yanahitaji uwekezaji mkubwa upande wa rasilimali fedha. Kama mtakumbuka, mnamo tarehe 10 Januari, 2024 nilimwakilisha Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika zoezi la harambee kwa ajili ya kukusanya fedha za kuzigharamia timu zetu za Taifa zinazotarajia kushiriki mashindano ya kimataifa. Nitumie fursa hii kuwashukuru sana wadau wote wa michezo, Taasisi za Serikali, Wakuu wa Mashirika na Makampuni waliojitokeza kuchangia fedha na hatimaye kuweza kukusanya fedha zisizopungua shilingi bilioni 4,700,000,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii pia kuwasihi sana Watanzania wote kuendelea kuchangia timu zetu za Taifa, zoezi la harambee bado linaendelea, Watanzania wote mnapewa wito wa kuchangia timu zetu kupitia namba zitanazotangazwa kupitia vyombo vya habari. Wizara ya Michezo bado inaendelea kuratibu zoezi la uchangiaji na kama wahenga walivyosema umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu, tuunganishe nguvu za

pamoja ili tuweze kufanikiwa na kuliheshimisha Taifa letu kupitia Sekta ya Michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na kwenye eneo hili, tumeamua kuwachagua wasanii maarufu kuwa wahamasishaji wa uchangiaji wa timu za Taifa, nao ni Baba Levo, Mwijaku na msanii mwenye michezo ya kuchekesha anaitwa Joti. Hawa popote watakapoonekana wakihamasisha wapokelewe na ujumbe wanaoutoa ni kwa niaba ya Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa shukurani na mwisho nitoe hoja kuahirisha Bunge, nikiwa naelekea kuhitimisha hotuba yangu, naomba sasa niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kazi kubwa mliyoifanya ya kuchangia katika mijadala inayoendeshwa katika kipindi hiki cha Bunge. Mmetoa ushauri na maoni ambayo yamechangia kwa kiasi kikubwa kufanya maboresho katika utendaji wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kadhalika ninawashukuru Katibu wa Bunge pamoja na watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa huduma zote walizotupatia katika kuhakikisha Mkutano huu unaendeshwa kwa mafanikio makubwa na kwa kuzingatia ratiba iliyopangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee nivishukuru vyombo vya ulinzi na usalama kwa kuendelea kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge na watendaji wengine usalama na amani wakati wote wa mkutano huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile niwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri pamoja na watendaji wote wa Serikali kwa kazi nzuri ya kuratibu shughuli zote zinazofanywa na sekta zetu kwa kutolea ufafanuzi hoja za Waheshimiwa Wabunge, lakini pia kufanyia kazi masuala muhimu ambayo yamekuwa yakijitokeza katika mijadala mbalimbali ilipokuwa inaendeshwa. Aidha, ninawashukuru wanahabari ambao wakati wote wamekuwa wakihakikisha Watanzania wanapata habari kuhusu mwenendo wa utekelezaji wa shughuli zote za Bunge letu Tukufu kuanzia siku liliopoanza hata leo tunapoelekea kuhitimisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitawashukuru madereva wetu ambao wamefanya kazi kwa uadilifu mkubwa katika kipindi chote cha Mkutano huu. Pia ninawashukuru sana watu wote waliotoa huduma kwa namna moja au nyingine wakati Bunge hili likiendelea hapa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kuwatakia waumini wa Kikristo, mfungo mwema wa Kwaresma na sherehe njema ya sikukuu ya Pasaka. Aidha, niwatakie Watanzania wote sherehe zenye amani na utulivu wakati wote wa mapumziko ya siku ya Pasaka. Kadhalika ninawatakia waumini wa Kiislamu maandalizi mema ya mfungo wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Nitoe rai kwa wafanyabiashara wote kutopandisha bei za vyakula kiholela ili kuwezesha mahitaji yote muhimu yakiendelea kutolewa na wananchi waweze kunufaika na biashara hiyo ya bidhaa zote muhimu kwa ajili yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa ninapenda kutoa hoja kuwa Bunge lako Tukufu liahirishwe hadi siku ya Jumanne, tarehe 2 Aprili, 2024 saa 3.00 asubuhi litakapokutana tena katika ukumbi huu hapa Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, wachache tu naona ndio wanataka kubaki hapa Dodoma. *(Kicheko)*

Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa wasilisho hilo na ahsanteni sana, Waheshimiwa Wabunge, na kwa utaratibu wetu sasa nitawahoji hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuahirisha Bunge mpaka siku na tarehe aliyoitaja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hoja hiyo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ya kuahirisha Bunge na mimi kuwahoji, sasa tunaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI**

**SPIKA:** Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Afrika Mashariki.

*(Hapa Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ziliimbwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaweza kuketi kidogo.

Kwanza nitumie fursa hii kukamilisha jambo moja, halafu tutahitimisha. Jambo lenyewe linahusu hoja ambayo nilisema nitaisoma ili wote tuwe tumeelewa maamuzi, lakini pia nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu japokuwa nitasema baadaye kwa kuwa ameshasema kwenye taarifa hili Azimio ambalo limepitishwa leo na Bunge. Kwa hiyo, Taarifa zetu Rasmi za Bunge, kuhusu Azimio hili ili likae sawa litakuwa linasomeka kwa namna hii.

Kwa kuwa, Jeshi la Kujenga Taifa na Jeshi la Kujenga Uchumi, hayana uwezo wa kumudu kuwapokea na kuwafundisha vijana wote wanaohitimu kidato cha nne na cha sita;

Na kwa kuwa, upo uwezekano wa vyombo vya ulinzi na usalama kuwapeleka JKT na JKU vijana watakaokuwa wameajiriwa kwa kukidhi masharti ya msingi ya ajira husika;

Na kwa kuwa, wapo vijana wenye sifa uwezo na wanaoweza kutimiza masharti ya ajira kwenye vyombo vya ulinzi na usalama, isipokuwa sharti la kupitia mafunzo ya JKT na JKU;

Sasa basi, Bunge linaazimia kwamba vijana wote wapewe fursa sawa katika ajira pale ambapo wanakuwa wametimiza masharti mengine yote yanayohusika na nafasi ya ajira husika isipokuwa cheti cha JKT na JKU hadi pale ambapo Serikali itakapokuwa na uwezo wa kuwapokea na kuwapa mafunzo ya JKT na JKU vijana wote wanaohitimu kidato cha nne na cha sita. *(Makofi)*

Ahsanteni sana, Kwa hiyo, Taarifa zetu Rasmi za Bunge, zitasoma kwa sura hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hoja ambayo ameitoa hapa na kwa kweli ameeleza mambo kwa kifupi yale ambayo Bunge limeweza kuyafanya, kwa hiyo, tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kazi nzuri ya usaidizi anayoifanya. Pia, Wenyeviti wa Bunge, Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, lakini pia Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, ahsanteni sana kwa kazi nzuri, tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Nitumie pia fursa hii kuwashukuru sana Wenyeviti wa Kamati zote na Makamu Wenyeviti, mmefanya kazi nzuri ya kuzisimamia Kamati zenu na pia mmefanya kazi kwa karibu sana na Serikali katika maeneo mbalimbali. Taasisi mbalimbali zimekuja mbele yenu, tunawashukuru sana kwa kazi nzuri na sasa Wajumbe wote wa Kamati hizi, ahsanteni sana kwa kazi nzuri mliyoifanya kwa kushirikiana na Wenyeviti wa Kamati zenu na Makamu Wenyeviti, mmefanya kazi kubwa ambayo imeonesha namna ambavyo mnafuatilia maamuzi ambayo Bunge inayachukua na namna Serikali inavyoyafanyia kazi. Kwa hiyo, ninawapongeza na kuwashukuru sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa upande wa Serikali, Mawaziri, Naibu Mawaziri, tunawashukuru sana kwa ushirikiano ambao mmeuonesha wakati mwingine maswali yanakuwa mengi zaidi hapa mbele, lakini mmeonyesha utayari wa kuyajibu. Kwa hiyo, tunawashukuru sana kwa ushirikiano ambao mmeuonesha

ukiacha maswali kwa ngazi ya Kamati, wengi wenu mmejitahidi sana kuhudhuria Kamati, Mawaziri, Naibu Mawaziri na wakati mwingine Kamati zingine huwa zinahitaji Maafisa Masuuli na wao wameenda huko. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunawashukuru sana kwa ushirikiano mliouonesha katika Bunge hili na tunaamini tutaendelea kufanya hivyo kwa sababu sote nia yetu ni njema kuhakikisha nchi yetu inapata maendeleo.

Waheshimiwa Wabunge, nitumie pia fursa hii kumshukuru sana Katibu wa Bunge na wataalam wote wa Ofisi ya Bunge, wanafanya kazi nzuri, Katibu wa Bunge, ahsante sana na wasaidizi wako wote kwa maana hizi kazi zote tunazozifanya zingekuwa ngumu sana bila ninyi kufanya kazi yenu kwa weledi na kwa uaminifu mkubwa sana. Kwa hiyo, tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Baada ya hayo, niwashukuru wananchi wote ambao wamepata nafasi ya kututembelea hapa Bungeni wakati tukifanya kazi, karibuni sana Bungeni, hili ni Bunge lenu na wale ambao mmeshuhudia leo wakati tunamaliza shughuli zetu, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunayo bendi yetu ambayo huwa inatusaidia hapa kwenye kufungua na kufunga Bunge, tunawashukuru sana kwa ushirikiano mkubwa ambao huwa mnatupa, tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mwisho kabisa ni wadau wote ambao wanashirikiana kwa karibu sana na sisi hasa katika kipindi ambacho tunakuwa tunatunga sheria, wadau wengi sana wamejitokeza, na hiyo ni kuonesha dhahiri kwamba wao wanao utayari wa kushirikiana na Bunge kuhakikisha Bunge linafanya kazi yake ya kuishauri Serikali, lakini na kuisimamia Serikali.

Kwa hiyo, niwaombe wadau wetu pamoja na shukrani hizo muendelee kutoa ushirikiano kwa Bunge na sisi tutaendelea kuyasikiliza maoni yenu ambayo ni ya kwetu sisi sote kwa sababu Bunge ni la kwenu na sisi ni wawakilishi wenu. Kwa hiyo, pale

mnapopata nafasi ya kuja kushirikiana na wawakilishi wenu ili kuhakikisha tunafanya kazi mliyotutuma basi msisite kufanya hivyo nasi tutawasikiliza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo mnafahamu kwamba Bunge letu kwa kawaida la mwezi wa pili huwa ni la wiki mbili, Bunge kwa maana ya humu ndani na wiki mbili Kamati, lakini safari hii kwa sababu ya shughuli tulizokuwa nazo nyingi tulipeleka maombi kwa upande wa Serikali na wakatukubalia.

Kwa hiyo, nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutuongezea wiki moja ya kukaa hapa Dodoma ili tufanye kazi yetu ya Kibunge kwa ukamilifu. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu upo hapa utupelekee salamu hizo kwa Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo sasa naahirisha shughuli za Bunge, mpaka tarehe 2 Aprili, 2024 saa 3.00 asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 7.16 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 2 Aprili, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*